

**CHANGAMOTO NA MANUFAA YA KUTAFSIRI  
KISWAHILI KATIKA MIKTADHA YA WINGILUGHA NAROK KASKAZINI**

**NA**

**WAWERU DAVID MWANGI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA SANAA KATIKA CHUO KIKUU CHA**

**NAIROBI**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

---

Sahihi

---

Tarehe

Waweru David Mwangi

C50/67014/2013

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.

---

Sahihi

---

Tarehe

Dkt. Zaja Omboga

(Mhadhiri, idara ya Kiswahili

Chuo kikuu cha Nairobi).

---

Sahihi

---

Tarehe

Dkt. Ayub Mukhwana

(Mhadhiri, idara ya Kiswahili

Chuo kikuu cha Nairobi).

## TABARUKU

Tasnifu hii ninawatabarukia wazazi wangu niwapendao kwa dhati na walionitangulia, baba mpendwa John Waweru na mama mpendwa Mary Waweru. Tabaruku nyingine ni kwa mke wangu mpendwa, Esther Mwangi na mtoto wetu tumpendae, Abramo Makiell, nawapenda. Mungu awabariki kwa kuwa mhimili maishani mwangu. Nawatakia kila la heri maishani.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kutoa shukrani zangu zisizo na kifani kwa mwenyeni Mungu kwa kutujalia uhai na neema maishani. Ninamshukuru Mungu kwa sababu kama si yeye, kamwe kazi hii haingewezekana wala kukamilika. Sifa na utukufu na shukrani zimrejeele Mungu mwenyeni. Ningependa kuchukuwa fursa hii kuwashukuru wasimamizi wangu; Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Ayub Mukhwana. Mwongozo na ushauri wao ulinifaa sana katika kutafitia na kuandika tasnifu hii. Walinipa muda wao kila wakati nilipowahitaji. Pasipo kujitolea kwao kazi hii ngumu haingefanikiwa. Nawashukuru pia wahadhiri wote kutoka idara ya Kiswahili ambao waliniandaa vilivyo na kunipa ujuzi na kuniwezesha kufaulu katika masomo yangu ya shahada ya uzamili: Prof. Mutiso wa Kineene, Prof. John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Amir Swaleh, Dkt.P.Jerono, Prof. Mwenda Mbatia na Dkt. Jefwa Mweri, shukran za dhati.Nawashukuru wazazi wangu waliogharamia masomo yangu tangu nilipojiunga na chuo kikuu kwa shahada yangu ya kwanza, dada yangu mpendwa Ann aliyenipa motisha katika masomo yangu. Namshukuru mke wangu Esther kwa kusimama nami kwa wakati mgumu wa kutafiti na kuandika tasnifu hii, mchungaji wangu Lemayian Ayotunde kwa maombi yake ya dhati.Nawashukuru wanafunzi wote waliokuwa wa darasa langu wa mwaka wa 2013. Tulishirikiana na kuhimizana tangu tulipokutana hadi kumaliza. Mungu na awakumbuke milele.Wakaazi wa wilaya ya Narok kaskazini nawashukuru wote; wote waliojitokeza wakati wa mahojiano; wafanyakazi na wasimamizi wa hospitali ya Narok level 5, wachungaji wa makanisa mbali mbali, walimu wote na wanafunzi wa mashule tulizozuru twawashukuru. Freshia shukrani kwa kazi yako nzuri ya kupiga chapa. Orodha ni ndefu, hatuwezi kuwataja wote, lakini tunawatambua na kuwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine. Mungu awabariki nyote.

## IKISIRI

Katika utafiti wetu tumeangazia changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Tulichagua hii mada ili kuweka wazi changamoto zinazokumba shughuli za kutafsiri . Vile vile tulitaka kubainisha manufaa yanayotokana na kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Ili kufikia malengo yetu tuliongozwa na nadharia ya mawasiliano katika tafsiri iliyoasisiwa na Peter Newmark (1982). Nadharia hii ilitufaa kwa sababu, kwa ujumla inaangazia suala la kuimarisha na kufanikisha mawasiliano katika mchakato wa kutafsiri. Baadhi ya changamoto ambazo tuliweza kugundua katika utafiti wetu ni changamoto zinazosababishwa na mifanyiko ya kitamaduni. Tumetoa mifano ya baadhi ya tamaduni hizi kwa mfano; aina ya vyakula, aina ya mavazi na mapambo, majina ya kurejelea wapendwa katika jamii, kuzawadiana katika jamii na kadhalika. Tumetoa mifano katika lugha ya Kimaasai na kulinganisha na lugha ya Kiswahili. Tuliteua lugha ya Kimaasai kwa sababu ndio lugha inayotumika na wengi na pia ndio lugha ya wenyeji wa maeneo yetu ya utafiti ya wilaya ya Narok Kaskazini. Pia katika kuangazia changamoto katika kutafsiri, tuligundua changamoto zinazosababishwa na tofauti za miundo ya lugha na tumetoa mifano maridhawa. Pia katika utafiti wetu, tumegundua licha ya kuwa kuna changamoto ya kutafsiri kuna manufaa pia. Tumeangazia manufaa hayo kwa kutoa mifano mwafaka. Tuliteuwa sekta muhimu katika maeneo yetu ya utafiti ambazo ni sekta za elimu, dini na sekta ya afya au matibabu. Tuligundua kwamba tafsiri inachangia pakubwa katika kuimarisha mawasiliano katika sekta hizi muhimu. Tumetamatisha kazi yetu kwa kutoa mapendekezo manne. Kwanza, tulipendekeza manufaa ya kutafsiri yachunguzwe katika sekta ya biashara kwa sababu sekta hii ni muhimu sana na inahusisha watu wengi katika jamii yoyote ile. Pili, tulipendekeza kwamba, kwa sababu tumejikita katika maeneo ya Narok Kaskazini, maeneo mengine yatafitiwe. Pia tumependekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusu tafsiri ili kupendekeza na kuthibitisha umuhimu wa kuanzisha somo la tafsiri katika shule za msingi na za upili na suala hili lichukuliwe kuwa suala nyeti. Hatimaye tumependekeza kando na nadharia ya mawasiliano katika tafsiri, nadharia zingine zitumiwe katika tafiti zingine za tafsiri ili kubainisha manufaa na changamoto katika mchakato wa kutafsiri.

## MASWALI YA MAHOJIANO

Baadhi ya maswali tuliyowauliza wahojiwa katika sekta za elimu, afya, dini na maswali ya jumla.

Maswali ya jumla:

- 1) Je unazungumza lugha ngapi?
- 2) Umesoma hadi kiwango kipi?
- 3) Una umri wa miaka mingapi?
- 4) Je wewe ni mwenyeji wa wilaya ya Narok Kaskazini?
- 5) Umeishi katika wilaya ya Narok Kaskazini kwa muda gani?
- 6) Tueleze jinsi unavyowasiliana na watu wengine katika shughuli zako za kila siku.

Maswali yaliyojikita katika sekta ya elimu.

Maswali yaliwalenga washikadau katika sekta ya elimu:

- 1) Wanafunzi wako wanatoka katika jamii gani?
- 2) Kama wanafunzi wanatoka jamii tofauti tofauti wanawasiliana vipi?
- 3) Wewe kama mwalimu unawasiliana vipi na wanafunzi kutoka jamii tofauti tofauti shuleni?
- 4) Je unakumbana na matatizo gani ya kimawasiliano baina yako na wazazi, wafanyakazi na washikadau wa shule yako.
- 5) Kama kuna matatizo unayashughulikia vipi?

Maswali yaliyojikita katika sekta ya afya.

Maswali haya yaliwalenga washikadau katika sekta ya afya:

- 1) Umehudumu katika hospitali hii kwa muda gani?
- 2) Je wewe ni mwenyeji wa wilaya ya Narok Kaskazini?
- 3) Je unawasiliana vipi na wagonjwa na wafanyakazi wengine wasiofahamu Kiswahili?
- 4) Tueleze kuhusu suala la mawasiliano kwa jumla katika shughuli zako.
- 5) Kama kuna matatizo za kimawasiliano mnatatia vipi?

Maswali yaliyojikita katika sekta ya dini.

Maswali haya yaliwalenga washikadau katika sekta ya dini:

1)Je unahubiri kwa kutumia lugha gani?

2)Je washirika wako wote wanafahamu lugha unayotumia kuhubiria?

3)Kama washirika wako wote hawaelewi lugha unayotumia katika mahubiri unatumia mbinu gani kufanikisha mawasiliano?

4)Tueleze kwa jumla jinsi unavyokabiliana na tatizo la mawasiliano katika shughuli zingine za kidini.

## YALIYOMO

Mada.....	(i)
Ungamo.....	(ii)
Tabaruku.....	(iii)
Shukrani.....	(iv)
Ikisiri.....	(v)
Maswali ya mahojiano.....	(vi)
Yaliyomo.....	(viii)

## SURA YA KWANZA

1.1	Utangulizi.....	1
1.2	Tatizo la utafiti.....	5
1.3	Madhumuni ya utafiti.....	6
1.4	Maswali ya utafiti.....	6
1.5	Sababu za kuchagua mada.....	6
1.6	Upeo na mipaka ya utafiti.....	7
1.7	Msingi wa kinadharia.....	7
1.8	Yalioandikwa kuhusu mada.....	11
1.8.1	Dhima ya Tafsiri.....	11
1.8.1.1	Mawasiliano.....	11
1.8.1.2	Utamaduni.....	13
1.8.1.3	Tafsiri kama nyenzo ya kufundisha lugha.....	15
1.8.1.4	Kuimarisha tabia ya kusoma na utafiti.....	16
1.8.1.5	Kuziba mapengo ya kimaana au kimsamiati baina ya lugha.....	17
1.8.1.6	Dhima ya Tafsiri katika uchumi.....	18
1.8.1.7	Kutafsiri kama kiliwazo.....	18



1.8.2	Vikwazo ya kutafsiri.....	19
1.8.2.1	Tofauti za miundo ya lugha.....	19
1.8.2.2	Tofauti za mitindo ya lugha.....	21
1.9	Njia za utafiti.....	23
1.10	Hitimisho.....	24

## SURA YA PILI

### CHANGAMOTO KATIKA KUTAFSIRI ZINAZOSABABISHWA NA MIFANYIKO YA KITAMADUNI

2.1	Utangulizi.....	25
2.2	Changamoto zinazosababishwa na tofauti za kitamaduni.....	25
2.2.1	Aina ya vyakula vya kitamaduni katika jamii ya Wamaasai.....	25
2.2.2	Hali ya kubadilishana au kuzawadiana kuimarisha uhusiano katika jamii.....	26
2.2.3	Majina ya kurejelea wapendwa.....	27
2.2.4	Aina ya mavazi na mapambo.....	28
2.2.5	Dhana ya Ekolojia.....	29
2.2.6	Rika na umri katika jamii.....	30
2.2.7	Koo au mbari katika jamii.....	31
2.2.8	Uvumbuzi wa kisayansi na teknolojia.....	31
2.2.9	Imani kama changamoto katika kutafsiri.....	32
2.2.10	Semi kama changamoto katika kutafsiri.....	32
2.2.10.1	Methali.....	33
2.2.10.2	Nahau.....	33
2.2.10.3	Misimu.....	33
2.2.10.4	Vitendawili.....	33
2.2.10.5	Misemo.....	33

2.2.11	Dhana zingine za kitamaduni ambazo hutatiza tafsiri.....	34
2.3	Hitimisho.....	34

### SURA YA TATU

#### CHANGAMOTO ZINAZOSABABISHWA NA TOFAUTI ZA MIUNDO YA LUGHA

3.1	Utangulizi.....	36
3.2	Kauli ya uambishaji kama changamoto katika kutafsiri.....	37
3.3	Kauli ya uambatanishaji kama changamoto katika kutafsiri.....	41
3.4	Viambishi vya masharti kama changamoto katika kutafsiri.....	42
3.5	Muundo wa viunganishi kama changamoto katika kutafsiri.....	43
3.6	Vivumishi vya pekee na visisitizi kama changamoto katika kutafsiri.....	44
3.6.1	Vivumishi vya pekee.....	44
3.6.2	Vivumishi Visisitizi...../.....	45
3.7	Changamoto za kutafsiri zinazotokana na hali ya wingi na kimo .....	46
3.8	Dhana ya jinsia ya kike na kiume kama changamoto katika kutafsiri .....	47
3.9	Usemi wa taarifa na usemi halisi kama changamoto katika kutafsiri.....	48
3.10	Vielezi (viulizi) kama changamoto katika kutafsiri.....	49
3.11	Mpangilio wa kiima na kiarifu katika sentensi kama changamoto katika kutafsiri.....	50
3.12	Dhana ya “kuzima” kama changamoto katika kutafsiri .....	51
3.13	Hitimisho .....	51

### SURA YA NNE

#### MANUFAA YA KUTAFSIRI KATIKA SEKTA ZA ELIMU, AFYA NA DINI

4.1	Utangulizi .....	53
4.2	Manufaa ya kutafsiri katika sekta ya elimu .....	53
4.2.1	Kujifunza Kiswahili katika kiwango cha chekechea na madarasa ya chini ya shule za msingi.....	54

4.2.2	Kuimarisha elimu ya watu wazima.....	58
4.2.3	Lugha za kwanza (Kimaasai) kujikuza kimsamiati .....	61
4.2.4	Kufanikisha mawasiliano baina ya shule na washikadau wengine.....	63
4.3	Manufaa ya tafsiri katika sekta ya matibabu/ afya .....	64
4.3.1	Maelekezo kwa wanaotembelea vituo vya matibabu/afya .....	64
4.3.2	Tahadhari dhidi ya magojwa hatari .....	65
4.3.3	Kampeni ya nyumba hadi nyumba dhidi ya magojwa ya watoto.....	68
4.3.4	Kuimarisha huduma za kliniki za wanawake wajawazito na waliojifungua .....	69
4.3.5	Uhamasishaji wa umma kuhusu afya bora .....	72
4.4	Manufaa ya tafsiri katika sekta ya dini .....	72
4.4.1	Tafsiri ya Biblia ya kimaasai kutoka tafsiri ya Kiswahili .....	73
4.4.2	Tafsiri za nyimbo za kusifu.....	77
4.4.3	Kanisa katika ibada za Jumapili .....	81
4.4.4	Mabango ya kutangaza mikutano ya injili na vibao vya kuelekeza watu .....	82
4.4.5	Mahubiri ya hadharani na mikutano ya wachungaji .....	86
4.5	Hitimisho.....	87

## SURA YA TANO

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1	Utangulizi .....	88
5.2	Muhtasari wa utafiti .....	88
5.3	Hitimisho na matokeo ya utafiti .....	90
5.4	Mapendekezo .....	90
	Marejeleo .....	92

## **SURA YA KWANZA**

### **1.1 UTANGULIZI**

Wingilugha ni dhana katika miktadha ya kimawasiliano na matumizi lugha inayoweza kueleweka kwa njia mbalimbali, na kwa hivyo, hushurutisha ufasiri na ufafanuzi wa aina nyingi. Wingilugha ni uhalisia unaoweza kujibainisha katika misingi ya mtu binafsi-yaani watu walio na uwezo wa kujieleza na kutumia lugha zaidi ya moja. Mifano ni katika hali zinazohusu watu waliohamia na kufanya makazi katika sehemu mpya ambao hulazimika kutumia lugha moja, kwa mfano shuleni, lugha nyingine katika shughuli anuwai nje ya miktadha ya familia na lugha nyingine katika miktadha ya kifamilia. Wingilugha unaweza pia kufafanuliwa katika misingi ya kijamii pale ambapo lugha mbalimbali hutekeleza majukumu dhahiri katika jamii, kwa mfano, lugha moja katika shughuli rasmi, nyingine katika shughuli za kibiashara na nyingine katika shughuli za kitamaduni. Wingilugha unaweza kujibainisha katika misingi ya kitaasisi pale taasisi fulani inaweza kuwa inatumia lugha zaidi ya moja katika shughuli zake.

Wingilugha, kwa hivyo, ni hali ya matumizi ya zaidi ya lugha moja, ambapo hudhihirika umilisi unaotofautiana katika misingi ya mtu binafsi au jamii mahususi. Hii ina maana ya mtu au watu wanaotumia lugha moja nyumbani na lugha nyingine (zaidi ya moja) nje ya miktadha ya nyumbani. Hii inaweza pia kuwa na maana ya watu walio na uwezo au wanaoshurutika kutumia lugha mbili au zaidi katika miktadha tofauti ya kimawasiliano. Hali hii vile vile inarejelea jamii zinazotumia lugha mbalimbali katika hali na miktadha inayotofautiana. Kimsingi, wingilugha una maana ya kuishi miongoni mwa lugha nyingi katika miktadha sawia. Kwa njia nyingine wingilugha ni uwezo wa watu binafsi, taasisi, makundi au jamii kuwa na maingiliano ya siku hadi siku kwa kutumia zaidi ya lugha moja. Wingilugha unaweza kufafanuliwa kuwa ni uwepo wa lugha nyingi mahali pamoja pasina kuwepo ulazima kwamba watu wanaokaa au wanaowasiliana katika mahali hapo wana umilisi sawia wa lugha hizo. Katika kiwango kingine, wingilugha unaweza kuwa ni uhalisi unaorejelea zaidi jamii kuliko watu binafsi.

Kuna uwezekano kwamba katika miktadha ya wingilugha, lugha zinazohusika zinaweza kuwa na hadhi zinazotofautiana kwa misingi ya kijumla au katika shughuli fulani mahususi.

Kwa mfano, katika Wilaya ya Narok Kaskazini, hadhi hizi zinajidhihrisha kwamba Kimaasai kina hadhi kubwa katika shughuli za kijamii na kitamaduni, Kiswahili katika shughuli za kikazi na kibiashara, Kiingereza katika shughuli rasmi za kiserikali na lugha zingine katika shughuli za kifamilia. Lugha tofauti zinaweza kuwa na heshima na fahari zinazotofautiana. Hali hizi zinaweza kujitokeza katika miktadha rasmi au isiyo rasmi ambapo matokeo yake yanakuwa ni kuibuka kwa lingua franka—lugha ya kiutekelezi itumiwayo kuwezesha mawasiliano kati ya watu wasiotumia lugha moja. Licha ya kwamba hali hizi za wingilugha zinaweza kuchukuliwa kuwa ni shida na tatizo katika mawasiliano, zinaweza kuwa na faida pia. Kwa mfano, katika misingi ya mtu binafsi faida za umilisi wa wingilugha ni pamoja na uwezo mkubwa wa kiutambuzi, uimarishaji wa uwezo wa kutekeleza shughuli mbalimbali kama zile za kiusomi, upataji maarifa kutoka vyanzo vingi, n.k. Katika miktadha ya kijamii, manufaa haya yanaweza kujumuisha manufaa ya kiuchumi kama vile kushiriki katika biashara kwa kutumia lugha nyingi, kupata huduma za kijamii. Lakini pamoja na kuwepo kwa manufaa haya, kuna pia matatizo kama vile uwezekano wa kukosa kuelewana.

Vinginevyo ni kwamba wingilugha unaweza kuibua mifanyiko tata ya lugha na uhamishaji lugha kwa njia bainifu na nyingine zisizokuwa bainifu. Kwa mfano, matumizi ya lugha mchanganyiko katika miktadha isiyo rasmi—miktadha ya nyumbani na ujirani. Kwa upande mwingine, uhalisi huu unaweza kujibainisha katika miktadha rasmi. Miktadha hii ya wingilugha inapoibuka ua kudhihirika pale ambapo watu tofauti tofauti kutoka jamii tofauti tofauti hujumuika pamoja na kutangamana, upo uwezekano wa kuibuka kwa changamoto za kimawasiliano na kuelewana kwa jumla. Ujumuijaji na utangamano huu wa watu unaleta pamoja tajiriba, uzoefu na mionoulimwengu inayotofautiana katika eneo fulani na katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano, uwezekano wa kutokuelewana katika shughuli za kijamii kama za kitamaduni, shughuli za kidini, kielimu, kibiashara, miongoni mwa shughuli zingine. Mawasiliano yanayojibainisha katika miktadha ya wingilugha mara nyingi hukumbwa na changamoto zinazotatiza kuelewana. Changamoto hizi zinaweza kusababishwa na mambo kadha, kwa mfano, mifanyiko ya kitamaduni inayohusishwa na jamii moja na isiyoeleweka au kuzoeleka na jamii nyingine.

Mifanyiko hii ya kitamaduni huathiri lugha kwa njia anuwai, ikikumbukwa kwamba lugha hufungamana na utamaduni fulani na mifanyiko hiyo huibua mifumo tata ya kimawasiliano.

Mifanyiko hii ya kitamaduni ni kama vile sherehe za kuzaliwa kwa watoto, sherehe za jando au unyago, mazishi, harusi na matambiko ya aina mbalimbali. Mifanyiko hii inaweza kuhusu misingi ya vifaa vya jamii kwa mfano katika ujenzi, mavazi, vyakula, usafiri na kadhalika. Mifanyiko hii ya kijamii inaweza kuwa ya miundo na mipangilio ya kijamii. Kwa mfano, mahusiano ya kifamilia, vikundi vya kijamii kama rika tofauti tofauti katika jamii na koo au mbari tofauti tofauti katika jamii. Mifanyiko hii ya kitamaduni pia huingiliana na kuhusiana na mazingira, maumbo ya nchi na majira tofauti tofauti kama majira ya mvua, kumea kwa nyasi, kiangazi na kadhalika. Hali hizi au majira haya huelezwa kwa njia tofauti tofauti kulingana na utamaduni husika. Vitengo hivi vya mifanyiko ya kitamaduni vinaibua mifumo changamano ya lugha ambayo inaweza kueleweka tu na watu wanaotoka au waliowazaliwa wa utamaduni husika. Katika miktadha ya wingilugha watu wa tamaduni tofauti tofauti huja pamoja na kutangamana. Kwa sababu ya tofauti zao za kitamaduni ambazo zimefungamana na lugha zao, mawasiliano hutatizika. Mawasiliano pia hutatizwa na miundo ya lugha. Kila lugha huwa na muundo wake. Mtu asiyelewa muundo wa lugha fulani hawezi kuelewa lugha hiyo husika. Watu wa lugha tofauti tofauti wanapokuja pamoja kama ilivyo katika muktadha wa wingilugha, mawasiliano hutatizika kutokana na miundo tofauti tofauti ya lugha tofauti tofauti husika. Miundo hii yote ya lugha husika huwa haieleweki kwa watu walio katika muktadha wa wingilugha. Jambo hili hupelekea kutatizwa kwa mawasiliano.

Hali kama hii inadhihirika katika wilaya ya Narok Kaskazini ambayo ndiyo sehemu tuliyoiteua kama maeneo yetu ya utafiti. Miongoni mwa lugha zinazozungumzwa katika wilaya ya Narok Kaskazini, Kiswahili kimeibuka kuwa lugha ya pekee inayotumika na watu wengi katika kuwasiliana. Hata hivyo, si watu wote walio na uwezo wa kuwasiliana kupitia Kiswahili hususan wenyeji kutoka jamii ya Wamaasai. Ili kufanikisha mawasiliano katika shughuli tofauti tofauti ambapo baadhi ni za lazima, kutafsiri kumekuwa njia ya pekee ya kukabiliana na tatizo la mawasiliano. Kutafsiri kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili na kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza.

Kuibuka kwa muktadha wa wingilugha na changamoto za kimawasiliano yanayotokana na hali hii, imetuchoea kutaka kudadisi jinsi wanaowasiliana wanavyokabiliana na changamoto za kimawasiliano zinazochochewa na muktadha wa wingilugha.

Hali kadhalika katika kulidadisi suala hili, kuna haja kukadiria nafasi ya tafsiri katika kutatua changamoto za kimawasiliano na wakati huo huo kuimarisha mawasiliano. Kwa hivyo, tumeangazia manufaa yanayotokana na kutafsiri katika sekta za elimu, dini, na sekta ya afya, hususan uhamasishaji juu ya masuala ya kiafya na utolewaji wa huduma za matibabu. Tumeangazia jinsi hizi sekta zinavyonufaika kwa njia mbalimbali kupitia tafsiri. Katika kuangazia changamoto na manufaa ya kutafsiri katika muktadha wa wingilugha, tumetoa mifano kutoka lugha ya Kimaasai na kulinganisha na kulinganua na mifano kutoka lugha ya Kiswahili. Tumetumia mifano ya Kimaasai kwa sababu Kimaasai ndiyo lugha ya wenyeji, inatumiwa na watu wengi zaidi ya lugha zingine na jamii zingine zinazohamia wilaya ya Narok Kaskazini zinajifunza Kimaasai. Ili kufanikisha utafiti wetu tumeongozwa na nadharia ya mawasilino katika tafsiri.

Masuala yanayohusiana na tafsiri yameshughulikiwa na wasomi na watafiti mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Tafiti juu ya tafsiri hazijakuwa za aina moja, kuna uanuwai mkubwa katika tafiti. Kwa mfano, katika miaka ya 1990, Mzee (1990) alishughulikia mahusiko na tafsiri za sajili tofauti tofauti katika tafsiri za makala magazetini na jinsi sajili zinavyoathiri sio tu lugha itumiwavyo bali pia njia za kutumia hiyo lugha. Miaka kadhaa badaye, Kaviti (2005) alitafiti juu ya makosa ya kisintaksia katika tafsiri za makala magazetini-hasa sintaksia ya Kiingereza na Kiswahili. Mtafiti huyu ameshughulikia matatizo ya kisintaksia na jinsi yanavyoathiri upokeaji na upitishaji wa ujumbe kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Otwere Samson (2012), amedadisi suala la usonde katika tafsiri-hasa kwa kutathmini usonde katika mafundisho ya Biblia katika shule ya Sabato kwa watu wazima. Ameangazia usonde kama kipengele kimojawapo kinachoathiri maana. Amezingatia ulinganifu wa maana baina ya makala asilia na makala pokezi. Naye Moraa Lydia (2013), ameshughulikia matatizo yanayodhihirika katika matini tafsiri za kimatibabu kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

Muhtasari huu wa tafiti za tafsiri zilizofanywa katika Kiswahili, unabainisha dhahiri kwamba suala la kuitafiti tafsiri katika miktadha ya wingilugha halijashughulikiwa kwingineko vilivyo. Kwa uelewa wetu, nyingi ya tafiti hizi zimekuwa zikikitwa katika misingi ya uwili lugha, lugha chanzi hadi lugha lengwa, si hoja masuala mahususi yaliyohusika.

Hata hivyo, hapana tafiti ambazo zimeshughulikia tafsiri katika kiwango cha kukadiria manufaa ya tafsiri katika miktadha ya wingilugha hasa kutokana na changamoto za kimawasiliano katika miktadha ya wingilugha. Hili ni suala na eneo la kiusomi ambalo linahitaji kuangaliwa na kufanyiwa utafiti.

## **1.2 TATIZO LA UTAFITI**

Katika utafiti wetu suala letu kuu lilikuwa ni kutafitia changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Shughuli mbalimbali huleta watu pamoja. Mara nyingi wanaoletwa pamoja katika shughuli hizi, kwa mfano, shughuli za kibiashara, kielimu, kidini na kitamaduni huwa ni watu wanaozungumza lugha tofauti tofauti. Jambo hili linapofanyika mazingira ya wingilugha huibuka. Katika muktadha wa wingilugha, inatarajiwa kwamba watu watapata ujuzi wa kutumia lugha zinazozungumzwa miongoni mwao na kuwasiliana na kisha kufanikisha shughuli zao. Lakini uhalisia ni kwamba katika mazingira kama haya watu wengi hawafanikiwi kupata ujuzi wa kutumia lugha zinazowazingira kikamilifu. Jambo hili linapelekea kuwa na matatizo ya kuwasiliana katika mazingira au muktadha wa wingilugha.

Hali kama hii ya tatizo la mawasiliano linapojiri kwa sababu ya mazingira ya wingilugha lazima masharti fulani yatimie ili kukabiliana na tatizo la kuwasiliana katika muktadha wa wingilugha. Lazima pawepo na angalau lugha moja ambayo inafahamika ama inayoweza kuleta watu wengi pamoja kimawasiliano. Wilaya ya Narok kaskazinia ambayo ndiyo tumeteua kama kielelezo cha utafiti wetu, imedhihirika kama muktadha wa wingilugha. Katika maeneo tunayotafitia, lugha ya Kiswahili inauwezo mkubwa wa kuleta watu wengi pamoja kimawasiliano.

Kwa kupitia kutafsiri kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili na kutoka Kiswahili hadi hizo lugha, ufanisi umepatikana katika kukabili tatizo la mawasiliano katika wilaya ya Narok Kaskazini iliyoko katika muktadha wa wingilugha. Licha ya kuwepo kwa manufaa ya kutafsiri kupitia Kiswahili, ni dhahiri kwamba kuna changamoto katika kutafsiri Kiswahili kwenye muktadha wa wingilugha. Mambo haya yalitupeleka katika mada yetu na kutupa msukumo wa kutafitia na kuweka wazi;changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha wilayani Narok Kaskazini.



### **1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI**

Katika utafiti wetu tulikusudia kufikia malengo yafuatayo:

- i) Kubainisha changamoto zinazodhihirika katika shughuli za kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha wilayani Narok Kaskazini.
- ii) Kubainisha manufaa yanayotokana na kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha katika wilaya ya Narok Kaskazini.
- iii) Kubainisha mchango wa tafsiri katika kuimarisha mawasiliano katika sekta za elimu, dini na afya wilayani Narok Kaskazini.

### **1.4 MASWALI YA UTAFITI**

Katika huu utafiti tulizingatia maswali yafuatayo:

- i) Je kuna changamoto zinazodhihirika katika shughuli za kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha wilayani Narok Kaskazini?
- ii) Je kuna manufaa yanayotokana na kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha wilayani Narok Kaskazini?
- iii) Je tafsiri ina mchango katika kuimarisha mawasiliano katika sekta za elimu, dini na afya wilayani Narok Kaskazini?

### **1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Tafsiri ni taaluma muhimu ambayo imekuwa ikiendeleza mawasiliano na kutatua shida nyingi za mawasiliano. Tafsiri inaweza kuleta manufaa katika shughuli nyingi. Hata hivyo kuna hali tofauti tofauti ambazo huweza kuibua changamoto katika mchakato wa kutafsiri. Tumekwisha kudokezea swala la muktadha wa wingilugha kama mfano. Tulichagua hii mada ili kuchunguza na kutathmini changamoto na manufaa katika kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Swala la manufaa yanayotokana na kutafsiri kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili na kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza katika muktadha wa wingilugha halijawai kushughulikiwa hasua kwa kuzingatia manufaa haya katika sekta muhimu kama ya elimu, dini na afya. Vile vile swala la changamoto zinazokumba mchakato wa tafsiri katika kutafsiri Kiswahili hadi lugha za kwanza na kinyume chake katika muktadha wa wingilugha halijashughulikiwa kikamilifu.

Hivyo kuna pengo lililoachwa kwa sababu hii mada hijawai kushughulikiwa vilivyo kwingineko. Tulinuia kuziba hili pengo. Tunaamini hii kazi itatoa mchango katika hazina ya tafiti zilizofanywa kuhusu tafsiri. Utafiti huu utawafaa wasomi na watalamu wa tafsiri kwa sababu utapanua uelewa wao wa manufaa na changamoto zinazokumba taaluma ya tafsiri.

### **1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI**

Katika utafiti huu tulijishughulisha na changamoto na manufaa katika kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Katika kutafitia changamoto tulijikita katika maeneo ya tofauti za kitamaduni na tofauti za miundo ya lugha. Hatukuzingatia changamoto zingine kando na maeneo haya. Katika kutafitia manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha, tulizingatia maeneo yafuatayo; maeneo ya kielimu, kidini na kimatibabu. Halikuwa jukumu letu kushughulikia sekta, taasisi au asasi zingine kando na hizo ambazo tumetaja. Katika utafiti huu tulitumia mifano kutoka lugha ya Kimaasai na kulinganisha na Kiswahili katika kuchanganua changamoto na manufaa ya kutafsiri ili kuokoa muda, na, kwa sababu Kimaasai ndio lugha inayozungumzwa na wengi na pia ndio lugha ya wenyeji wa eneo letu la utafiti. Hatukutoa mifano kutoka lugha zingine. Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya mawasiliano katika tafsiri (P. Newmark 1982). Hatukutumia nadharia nyingine. Tuliteua wilaya ya Narok Kaskazini kama utafiti kielelezo chetu. Hatukushughulikia maeneo mengine nje ya hapa; Narok Kaskazini.

### **1.7 MSINGI WA KINADHARIA**

Ili kufikia malengo ya utafiti huu, tuliongozwa na nadharia ya mawasiliano katika tafsiri iliyosisiwa na mtaalamu Peter Newmark mnamo mwaka wa 1982. Peter Newmark, katika nadharia yake anashikilia kauli kwamba suala la mawasiliano ndilo muhimu katika tafsiri yoyote ile. Kulingana na mtaalamu huyu lengo kuu la tafsiri ni kufanikisha mawasiliano kikamilifu. Kauli hii ilitufaa sana katika utafiti wetu kwa sababu tulinuia kuonyesha jinsi tafsiri inavyoweza kufanikisha mawasiliano hata kama kuna changamoto kadha ambazo huibuka katika kutafsiri. Mwasisi wa nadharia hii anaelezea kuwa mawasiliano ni utaratibu wa kuhamisha ujumbe kutoka kwa mwasilishi hadi kwa mpokezi. Ingawa kuna mitazamo mingi ya mawasiliano, tafsiri hurejelea mtazamo wa kitamaduni. Kulingana na mtazamo huu utaratibu wa mawasiliano hufuma vigezo vitano vya kimsingi:

mwasilishi, mpokezi, ujumbe, chombo na vikwazo. Mwasilishi ni mwandishi au msemaji, msisitizo umo katika mtazamo wake. Mpokezi ni msomaji au msikilizaji, msisitizo huwekwa katika tajiriba yake. Ujumbe husisitiza dhamira ya mwasilishi. Chombo ni lakabu ya lugha; ya maandishi, mazungumzo au ishara. Vikwazo hurejelea matatizo mintarafu muktadha wa mawasiliano na utamaduni. Mtazamo huu husisitiza uwakilishi, upokezi, uthamini na ukubalifu wa ujumbe kwa hadhira ya tafsiri.

Utaratibu huu wa mawasiliano kama ulivyofafanuliwa na mwasisi wa nadharia ya mawasiliano katika tafsiri, ulitufaa kabisa haswa tukizingatia vigezo vyake vitano vya kimsingi; mwandishi, mpokezi, ujumbe, chombo na vikwazo. Ni dhahiri kwamba vigezo hivi vitano ndivyo nguzo kuu ya mchakato wowote wa kutafsiri. Katika utafiti wetu tulipata mwelekeo kwa sababu tulizingatia na kushughulikia suala la mwasilishi wa ujumbe ambaye ndiye mwandishi, msemaji au mtafsiri. Kwa sababu msisitizo upo katika mtazamo wake, tuliweza kuona jinsi kauli hii inavyoweza kuadhiri tafsiri na kisha mawasiliano. Mpokezi ambaye ndiye msomaji au msikilizaji wa ujumbe anatazamiwa kufaidika. Jambo hili lilitusaidia tulipoangazia manufaa ya kutafsiri katika Kiswahili.

Chombo ambacho kimeelezewa kama lugha ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu suala la tafsiri liko katika misingi ya lugha zinazohusishwa. Hivyo, kuelewa lugha husika na mifumo ya lugha hio ni muhimu kulingana na utafiti wetu. Vikwazo ni kigezo muhimu sana katika utafiti wetu. Kulingana na mwasisi wa nadharia hii ya mawasiliano katika tafsiri, mtalamu Peter Newmark, vikwazo hurejelea matatizo mintarafu muktadha wa mawasiliano na utamaduni. Katika utafiti huu vikwazo hivi ndivyo tumevirejelea kama changamoto.

Suala hili la vikwazo na muktadha lilitusaidia kwa sababu mbali na kuangazia manufaa ya kutafsiri katika Kiswahili, suala letu kuu vile vile lilikuwa ni kuchunguza changamoto/vikwazo katika kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Mtazamo huu wa P. Newmark husisitiza uwasilishi, upokezi, uthamini, na ukubalifu wa ujumbe kwa hadhira ya tafsiri. Mtazamo huu umekuwa muhimu katika utafiti wetu kama tulivyoona.

Mahitaji ya utaratibu huu yashirikisha nguzo sita za mawasiliano:

- (i) Kanuni za muundo na matumizi ya lugha zote mbili
- (ii) Mifumo ya tamaduni zote mbili

- (iii) Mitindo na sajili za matini husika
- (iv) Dhamira ya matini au mwandishi
- (v) Tajiriba za kijamii na kitamaduni za mpokezi.
- (vi) Matarajio ya mpokezi

Katika utafiti huu- changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha, tulifaidika na nguzo hizi sita za mawasiliano kwa sababu katika utafiti wetu, ili kuafikia malengo yetu ilitubidi tutafitie kanuni za muundo na matumizi ya lugha kulingana na muktadha wa kutafsiri katika wingilugha. Tuliangazia pia mifumo ya tamaduni za lugha zilizohusika. Aidha tulizingatia dhamira ya mwasilishaji wa ujumbe, tajiriba za kijamii na kitamaduni za wanaopokea ujumbe na matarajio ya jumla ya mpokezi.

Mawasiliano katika tafsiri ni mtazamo muhimu zaidi uliojaribu kukosoa mitazamo ya kiisimu. Mtazamo huu wa kiisimu kwa hivyo, haujisimamii ila umerejelea nadharia za kiisimu na kutoa mapendekezo ya kuboresha tafsiri. Mapendekezo hayo hupewa hadhi ya nadharia. Nadharia ya mawasiliano katika tafsiri yatanguliza mapendekezo yake kwa kushambulia nadharia ya kiisimu. Lawama kubwa inayotolewa ni kule kutegemea muundo na utamaduni wa lugha chanzi. Lawama ya pili imo katika kule kusisitiza tafsiri za sarufi na leksia. Lawama hizi mbili yaani muundo na utamaduni wa lugha chanzi na usisitaji wa tafsiri za sarufi na leksia zilitusaidia katika kutafitia changamoto za kutafsiri.

Kulingana na mtazamo wa wamasiliano, nadharia za kiisimu zinafanana licha ya tofauti za msisitizo. Mfano huu wajitokeza katika viwango vitatu:

- i) Mtafsiri hujifunga zaidi na mitindo ya lugha chanzi pia hujaribu kuwasilisha maana kwa kurejelea zaidi muktadha wa lugha chanzi.
- ii) Tafsiri hujijenga katika utamaduni wa lugha chanzi, yaani kiini cha uhalisia wa maana ni sura za utamaduni wa lugha chanzi.
- iii) Tafsiri huthamini zaidi mitindo ya mwasilishi asilia kuliko mahitaji ya hadhira. Kwa jumla, tafsiri mawasiliano yashuku kule kulemewa katika sura za muundo, mtindo na utamaduni wa lugha chanzi. Hivyo hiki ndicho chanzo cha upotovu wa maana kwa vile upotovu wa maana huletwa na mikinzano ya mitindo, lugha na utamaduni.

Nadharia za kiisimu kwa hivyo, hazina uwezo wa kufasiri maana. Hata hivyo kwa upande wetu udhaifu huu wa nadharia za kiisimu ulitusaidia katika kutambua na kuthibitisha changamoto/ vikwazo ambavyo huibuka katika kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Kulingana na nadharia ya mawasiliano katika tafsiri, nadharia za kiisimu badala ya kufasiri maana, zaonekana kama zamwelekeza mtafsiri kulazimisha maana. Ili tuweze kufasiri maana, twahitaji kubaini ujumbe na dhamira ya mwandishi kisha tuwakilishe ujumbe huo katika tafsiri kwa kurejelea tajiriba ya msomaji wa tafsiri.

Mawasiliano katika tafsiri inajiimarisha katika mihimili yake kwa kuzingatia hoja nne ambazo zilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa jumla. Mihimili yenyewe ni kama ifuatayo:

- i) Chochote ambacho hueleweka pia kina uwezo wa kufasiriwa na hivyo kutafsirika.
- ii) Hamna visawe vya kudumu katika hali ya mabadiliko.
- iii) Tunatafsiri usemi, sio lugha. Usemi ni lugha inavyotumiwa katika hali halisi ya mawasiliano. Maneno ni ishara na viwakilishi vya maana, sio maana yenyewe.
- iv) Tunatafsiri ili kumridhisha mpokezi wa tafsiri. Tunabidiika kujifunga na muundo, mtindo na utamaduni wa lugha lengwa.

Mihimili hii minne imekuwa na umuhimu katika utafiti wetu kwa sababu ilituelekeza kwa kauli kwamba tafsiri inauwezo wa kutatua matatizo ya mawasiliano na kuleta manufaa. Mathalan, twadokezewa kwamba hamna visawe vya kudumu katika hali ya mabadiliko. Hivyo hata kama hamna visawe vya maneno katika lugha zinazohusika katika tafsiri, bado tafsiri ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano. Kisha, katika mihimili hii tuliona licha ya tofauti za lugha zinazohusika katika tafsiri, kuna uwezo kupitia tafsiri kufanikisha mawasiliano kwa kutafsiri usemi wala sio lugha na hatimaye kumnufaisha mpokezi wa tafsiri. Mihimili hii kwa jumla, ilituelekeza kwa kauli kwamba tafsiri ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano hivyo kulete manufaa. Katika utafiti wetu tulishughulikia manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Bila shaka mihimili hii minne iliweka msingi thabiti wa utafiti huu kama jinsi ambavyo tumeona.

## **1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

Katika sehemu hii tuliteua mada mahususi ambazo tuliona zitatufaa katika utafiti wetu. Tumeangazia maoni ya watalamu kadhaa ambao wameshughulikia mada hizi, jinsi walivyosema kuhusu mada zao, jinsi mada zao zilivyoingiana na utafiti wetu, na jinsi utafiti wetu ulivyonufaika kutokana na mchango wa watalamu husika. Aidha tulitathmini kauli zao, tukazilinganisha na kuzilinganua na makusudi na malengo ya utafiti wetu. Tumeangazia mada hizi: Dhima ya tafsiri, mawasiliano, utamaduni, tafsiri kama nyenzo ya kufundishia lugha, kuimarisha tabia ya kusoma na utafiti, kuziba mapengo ya kimaana au kimsamiati baina ya lugha, dhima ya tafsiri katika uchumi na tafsiri kama kiliwazo.

### **1.8.1 Dhima ya Tafsiri**

Mshindo (2010) ameelezea kwamba tafsiri hulaumiwa kwa wingi wa kasoro zake kuliko kusifiwa kwa faida zake. Kutokana na kaida hii tungetarajia watafsiri wafe moyo na kujitenga na shughuli za tafsiri. Mbali na hayo, wasomi wanaendelea kujitahidi kutafsiri zaidi. Hii ni ishara ya dhima kuu ya tafsiri. Kulingana na wataalamu hawa; Mwansoko na wenzake (2006) na Mshindo (2010) miongoni mwa dhima au majukumu ya tafsiri ni pamoja na:

#### **1.8.1.1 Mawasiliano**

Wataalamu hawa Mwansoko (2006) na Mshindo (2010), wanadai kwamba mawasiliano ni nguzo kuu ya uhai, maelewano na maendeleo ya jamii. Karibu mataifa yote yanatambua umuhimu wa jamii ya kimataifa. Nayo jamii ya kimataifa imetekeleza maazimio mengi kuhusu tabia, hali na maendeleo ya watu, kama vile haki za kibinadamu, haki za watoto na umuhimu wa mazingira ya ulimwengu. Maazimio haya yametafsiriwa kwa lugha zinazozungumzwa kwa wingi ili kufikia watu wengi iwezekanavyo. Watawala wa kimataifa binafsi wanahakikisha arifa muhimu kwa jamii yote zimetafsiriwa kwa lugha inayoeleweka na raia wengi, ili waweze kujisomea au kusomewa na wenzao. Katika nchi nyingi, kwa mfano Kenya na Tanzania, makala mengi ambayo hapo awali yalikuwa yameandikwa kwa Kiingereza yametafsiriwa au kufanyiwa mpango wa kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka na wengi. Makala hayo ni kama vile katiba ya nchi husika.

Makala mengine ni kama mafunzo kuhusu mikasa kama vile ugonjwa hatari wa ukimwi,mafunzo muhimu kama vile huduma ya kwanza na taarifa za habari.

Ni jambo muhimu kwa kila mtu kuelewa sheria ambazo hutawala haki zake na pia wajibu wake kama raia wa nchi yake.Mtu mwenye hekima hupenda kuelewa njia za kulinda afya na uhai wake,pamoja na ule wa watu wengine.Kwa mfano, nchini Kenya watu wengi hupenda kusoma gazeti la *Taifa Leo* ambalo huwa na makala tofauti tofauti yaliyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili,kwa kutaka kujua yale mambo muhimu yanayotukia nchini na kwingineko.Wasomi wa lugha changa za mafunzo hubidiika kutafsiri taarifa nyingi za kinadharia kutoka lugha zilizoimarika zaidi kiakademia. Msomi wa Kiswahili,kwa mfano,anajikuta akitafsiri maelezo kutoka Kiingereza au Kifaransa.Anatafsiri kwa sababu anahitaji taarifa zilizoandikwa kwa lugha hizi ili aweze kuwasilisha na kutetea hoja zake. Katika sehemu hii tumeona jinsi watalamu Mwansoko H.J. na wenzake (2006) na Mshindo (2010) wanavyoshughulikia suala la dhima ya tafsiri katika mawasiliano .

Mada hii imetufaa katika utafiti wetu kwa sababu pana uwiano kati ya mada hii na suala letu la utafiti. Kwanza, watalamu hawa, kama ilivyo kwetu wamejikita katika taaluma ya tafsiri na pili, wanaangazia dhima ya tafsiri au umuhimu wa tafsiri. Kwa upande wetu tuliangazia manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha .Tulinuia kuchunguza jinsi tafsiri inavyoweza kuleta manufaa katika maeneo ya kielimu, kimatibabu au kiafya na maeneo ya kidini. Bila shaka katika maeneo haya ili pawe na mafanikio lazima wote wanaoshiriki katika sekta hizi waweza kuwasiliana.

Katika utafiti huu tulijikita katika muktadha wa wingilugha ambapo watu tofauti tofauti wanaohusika katika sekta tulizotaja hapo juu wanazungumza lugha tofauti. Ili kufanikisha mawasiliano katika mazingira kama haya ya wingilugha tafsiri ina umuhimu mkubwa. Wataalamu hawa Mwansoko H.J na wenzake (2006) na Mshindo (2010) wameelezea jinsi tafsiri inavyoweza kuimarisha mawasiliano. Mada hii imetusaidia katika utafiti wetu kwa sababu tumetafitia jinsi tafsiri inavyoweza kuimarisha mawasiliano katika muktadha wa wingilugha- kutafsiri kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili na kutoka Kiswahili hadi lugha hizo za kwanza. Tafsiri hii ikifanyika, tumeangalia jinsi sekta za elimu, afya na sekta ya dini zilivyoimarika na kuleta manufaa katika hizi sekta.

Hata hivyo, ingawaje tumeona mada hii ya dhima ya tafsiri katika mawasiliano imetufaa katika utafiti wetu, suala hili limezungumziwa kwa ujumla sana. Suala la mawasiliano ni pana sana kwa sababu kuna mawasiliano katika nyanja nyingi sana. Kwa mfano, katika sekta za uhandisi, sayansi na teknolojia, muziki na burudani na kadhalika. Wataalamu wahusika hawakuweza kuegemea maeneo mahususi na kuelezea kwa kina. Aidha mifano waliotoa ni chache na haikuelezewa kwa kina. Kwa upande wetu tuliziba pengo hili kwa kujikita katika sekta za elimu, dini na sekta ya afya. Tulichunguza jinsi sekta, hizi zilivyonufaika kupitia tafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza na lugha za kwanza hadi Kiswahili. Tulizingatia muktadha wa wingilugha, na kujikita katika maeneo mahususi ya wilaya ya Narok kaskazini. Katika sehemu hii tumeona jinsi wataalamu Mshindo (2010) na Mwansoko na wenzake (2006) walivyoelezea suala la tafsiri katika kuimarisha mawasiliano. Kwa maoni yetu tulitambua ufanisi wao lakini kwa kiasi tu. Kwa jumla wameweza kuelezea suala la tafsiri na jinsi tafsiri inavyoweza kuimarisha mawasiliano. Hawakuweza kujikita katika maeneo mahususi na kuelezea kwa kina. Pia tumeona wametoa mifano kwa uchache, kwa kijumla na kijuujuu hivyo kuwacha mapengo. Hata hivyo uchunguzi wao ulitupa msingi wakuendeleza utafiti wetu kama tulivyoelezea.

### **1.8.1.2 Utamaduni**

Wataalamu hawa: Mwansoko na wenzake (2006) na Mshindo(2010) wamezungumzia suala la dhima ya tafsiri katika kupitisha utamaduni. Wamedokeza kwamba utamaduni unahusu masuala mengi ya maisha ya jamii. Hapa wameangazia zaidi falsafa za maisha zilivyoenezwa kupitia matumizi ya lugha na fasihi. Ngano na tanzu zingine za fasihi ni hifadhi za tamaduni za lugha zake. Tunapotafsiri fasihi, tunafuma baadhi ya vipengele vya utamaduni wa lugha chanzi kwa utamaduni wa lugha pokezi. Mafunzo yanayopatikana katika tafsiri za lugha za Kiafrika-fasihi simulizi sasa ni amali ya Kiswahili. Tafsiri za Kiarabu, Kingereza na lugha zingine pia zimechangia ujenzi wa lugha ya Kiswahili. Tunapotafsiri pia tunajenga lugha pokezi. Lugha pokezi inamotishwa kukua na wakati wake na kumiliki nyenzo za kuhimili miradi ya kijamii. Dini ni nguzo muhimu inayohimili jamii nyingi. Katika kusambaza utamaduni na imani za Kikristo, Wamishenari walitafsiri Biblia na mafunzo mengi kwa lugha nyingi kote ulimwenguni. Vile vile Waisilamu walitumia mbinu kama hiyo na kutafsiri Koran na mafunzo kama hadithi kwa lugha nyingi.



Ni jambo rahisi zaidi kufikia roho ya mtu kwa lugha yake kuliko ile ya wageni. Bila tafsiri dini nyingi hazingesambaa kadiri zimekuja kufanikiwa. Ikumbukwe, dini hizi zilisambaa sawia elimu ya mwegemeo wake. Katika sehemu hii watalamu tuliwarejelea wameweza kuonyesha jinsi tafsiri inavyoweza kuhamisha au kusambaza utamaduni wa jamii fulani hadi nyingine. Wamefafanua jinsi lugha pokezi inavyoweza kumotishwa na kuimarishwa na utamaduni wa lugha chanzi kupitia tafsiri. Wametuonyesha jinsi dini na imani zinavyoweza kutoka jamii moja hadi nyingine kwa kupitia tafsiri.

Mada hii kama ilivyojidhihirisha imeingiana na mada yetu ya utafiti. Kama tulivyokwisha elezea hapo awali tulinuia kuonyesha jinsi tafsiri inavyoweza kuimarisha mawasiliano katika muktadha wa wingilugha ambapo watu huletwa pamoja na shughuli mbalimbali na watu hawa huzungumza lugha tofauti tofauti. Tilitaka kuonyesha manufaa yatakayodhihirika katika sekta za elimu, dini, na sekta ya matibabu kwa kupitia kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza haswa Kimaasai, na vile vile kutafsiri kutoka lugha hizi za kwanza hadi Kiswahili.

Mada hii imetusaidia kuweka msingi haswa tulipokuwa tukitafitia jinsi sekta ya dini inavyoweza kunufaika kupitia kwa kutafsiri kwa Kiswahili hadi lugha za kwanza na kinyume chake katika mazingira ya wingilugha kama ilivyo katika maeneo yetu ya utafiti- wilaya ya Narok kaskazini. Wataalamu hawa kwa jumla wamezungumzia suala la utamaduni na jinsi unavyoweza kupitishwa kutoka lugha chanzi hadi lugha pokezi kupitia tafsiri. Suala la utamaduni limitumiwa kama dhima mojawapo ya tafsiri. Suala hili lilielekea kukinzana na mada yetu ya utafiti haswa tunapozingatia manufaa za kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Hii ni kwa sababu kila jamii ina tamaduni zake.

Tamaduni hizi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Tamaduni zingine huwa ni changamano sana na itabidi mtu awe ametoka katika jamii ambamo tamaduni hizo zipo ili kuzielewa fika. Hivyo, tafsiri imeweza kutatizika pale ambapo mtafsiri hana tajiriba na uelewa wa utamaduni husika. Watalamu hawa Mwansoko na wenzake (2006) na Mshindo(2010) wameangalia utamaduni kama dhima mojawapo ya tafsiri. Kwa upande wetu, kwa sababu za totauti ambazo tumezungumzia hapo juu, utamaduni umejitokeza kama changamoto katika kutafsiri hivyo kukinzana na kauli ya watalamu hawa. Hata hivyo ukinzani huu umekuwa wa manufaa kwetu kwa sababu tofauti zilizoko katika tamaduni tofauti zilitusaidia kutambua changamoto zilizoko katika kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha.

Kwa mfano, tofauti za kidini na kiimani ambazo zimejadiliwa na wataalamu hawa zimetuwekea msingi wa kutafitia changamoto za kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha haswa tukizingatia changamoto za kidini. Kwa jumla kama tulivyoona mada hii, ya utamaduni kama dhima ya tafsiri itametufaa katika utafiti wetu.

### **1.8.1.3 Tafsiri kama Nyenzo ya Kufundishia Lugha.**

Mshindo (2010:26) Anasema ili kuweza kupata mawazo au kuvijua vipengee vya lugha nyingine huna budi kutumia taluma ya tafsiri ili uweze kuyatambua mawazo yaliyomo katika lugha chanzi na kuyapeleka katika lugha lengwa. Ameeleza kuwa kwa mfano, katika miaka ya hamsini (1950) na sitini (1960) Kiswahili kilitumika kufundishia lugha ya Kingereza katika shule za sekondari za Zanzibar. Mbinu iliyotumika ni; wanafunzi kupewa miundo ya Kiswahili na kuitafsiri kwa Kingereza au kupewa miundo ya Kingereza aitaafsiri kwa Kiswahili. Kutokana na dhima hii ni muhimu kwa mtafsiri kujifunza miundo ya lugha zote husika, yaani lugha chanzi na lugha lengwa.

Katika sehemu hii mtaalamu Mshindo (2010) ameelezea jinsi tafsiri inavyoweza kuwa nyenzo ya kujifundishia lugha. Kulingana na maelezo ya mtaalamu huyu ni kwamba kupitia taluma ya tafsiri mtu anaweza kujifunza miundo na vipengee vya lugha zingine. Ametoa mfano jinsi Kiswahili kilivyotumiwa huko Zanzibar kujifunzia Kingereza kwa kuzingatia miundo na vipengee vya lugha hizi mbili, yaani Kiswahili na Kingereza. Mada hii ya Mshindo ilitufaa katika utafiti wetu tulipokuwa tukitafitia manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha pale ambapo tulipojikita katika sekta ya elimu. Hii ni kwa sababu katika muktadha wa wingilugha watu huzungumza lugha tofauti tafauti. Kwa mfano, katika shule za chekechea na za msingi kuna wanafunzi wasioelewa Kiswahili wala Kingereza bali wanaelewa tu lugha zao za kwanza. Mada hii imetuekea msingi ambao tumeweza kujengea: manufaa ya kutafsiri kama nyenzo ya kufundishia lugha kama alivyoelezea Mshindo (2010). Kauli hii ilitufaa katika uchunguzi wetu wa jinsi sekta ya elimu inavyoweza kunufaaika kutokana na kutafsiri Kiswahili katika mazingira ya wingilugha. Kama tulivyoona vile vile kulingana na mtaalamu huyu, tofauti za miundo ya lugha na vipengee tofauti vya lugha kama ilivyojadiliwa ilitusaidia tulipokabiliana na suala la changamoto katika kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha, kama tulivyoona mada hii vile vile, ina mchango wake japo mdogo, katika kuimarisha utafiti wetu.

#### **1.8.1.4 Kuimarisha Tabia ya Kusoma na Utafiti**

Katika taaluma ya tafsiri,mtafsiri analazimika kukusanya kwa kusoma visawe vingi na miundo mingi ya lugha zitakazo msaidia katika kazi yake ya kutafsiri ,haya ni kulingana na Mshindo (2010).Anadokeza kwamba kusoma kunamsukuma mtafsiri kutafiti kwa kina juu ya visawe ,utamaduni wa lugha chanzi na lugha lengwa na kukusanya msamiati .Kwa kufanya hivyo mtafsiri anakuwa na uwanja mpana wa kumudu kazi yake ya kutafsiri. Zaidi ya hayo ,mtafsiri sharti azingatie taluma zingine ambazo zinahusiana na taluma ya tafsiri .Taluma ya tafsiri imeingiana na kufumbata taluma nyingi.Mtafsiri, hivyo, hutafiti kuhusu na kusoma kuhusu taluma kama hizo.Mshindo anatupa mifano ya taluma ambazo zinahusiana na taluma ya tafsiri na kutuonyesha jinsi zinavyohusiana.Miongoni mwa taluma ambazo anaangazia ni taluma za:isimulinganishi ,simujamii,semantiki/pragmatiki, elimu mitindo na taluma ya mantiki.

Mshindo (2010) anaeleza kuwa ikumbukwe tu kuwa hakuna jukumu ya kazi bila ya kuwa na data sahihi ,hivyo ili jukumu iweze kuwa na uhakika wa kazi yake,Mshindo anafafanua kwamba ukweli ni kwamba hakuna mtafsiri ambaye hafanyi utafiti,japo mdogo, katika shughuli ya kutafsiri.Hulazimika kupekuwa katika nyanja mbalimbali ili kujua maana ya maneno,usuli wa mambo,na historia ya matukio .

Katika sehemu hii mtaalamu husika-Mshindo (2010) ametufafanulia jinsi tafsiri inavyotupa ari ya kusoma na kutafiti.Pia ameelezea jinsi taluma tofauti tofauti zinavyohusiana na kuingiana na taluma ya tafsiri.Hata hivyo, hajaonyesha jinsi taluma hizi zinavyoweza kunufaika kutokana na tafsiri hivyo kuwepo kwa pengo katika utafiti wake.Licha ya upungufu huu mada ya Mshindo itametufaa kwa sababu, kwanza imetupa motisha wa kuendeleza utafiti wetu na kuweza kukusanya data sahihi.Pili Mshindo ameangazia jinsi taluma ya tafsiri inavyohusiana na taluma zingine. Katika utafiti wetu pia tuliangalia jinsi tafsiri inavyoweza kuhusiana na sekta za elimu, dini na sekta ya afya. Ili kuziba pengo lililojitokeza kama tulivyoelezea hapo juu, tulizingatia kuonyesha jinsi sekta tulizozitaja hapo juu zitakavyo nufaaika kutokana na taluma ya tafsiri.Hivyo basi mchango huu wa Mshindo umetufaa katika utafiti wetu.

### **1.8.1.5 Kuziba Mapengo ya Kimaana au Kimsamiati Baina ya Lugha**

Kutafsiri huziba mapengo ya kimsamiati au kimaana baina ya lugha. Maneno mengi hukumbwa na athari za kitamaduni ,kiisimu na kihali.Kutokana na athari hizi mtafsiri hulazimika kutafuta maana ya maneno yatakayoeleweka vizuri kwa watumiaji wa lugha lengwa. Hii hutokana na tofauti ya matumizi katika baadhi ya maneno ambapo katika jamii nyingine yana maana tofauti na ile ya lugha chanzi.Kwa mfano ,Mshindo(2010) anasema katika mazingira ya rushwa neno mchicha ,amabalo maana iliyozoeleka ni aina ya mboga ya majani ,haliwezi kukidhi haja kwa maana hiyo iwapo mtafsiri hakulifafanua katika tafsiri yake na kumwezesha msomaji wake kuelewa kwamba katika muktadha huo lina maana ya rushwa.Pia katika mazingira mengine neno wimbo husimama badala ya rushwa kwani kuna baadhi ya watuhumiwa ambao huambiwa kuwa ,ili waweze kushinda kesi zao hawana budi kuimba wimbo wao.

Katika sehemu hii tumeelezewa jinsi tafsiri inavyoweza kutumiwa kuziba mapengo ya kimsamiati na kimaana baina ya lugha.Tumeoneshwa, kwa mifano, jinsi maneno yanavyoweza kutumika katika miktadha ingine kumaanisha maana tofauti na maana yake ya kawaida.Mada hii imetusaidia kwa sababu tumeangalia lugha katika miktadha tofauti tofauti. Kwa mfano, sekta tulizozingatia kama sekta ya elimu ,afya na sekta ya dini ni sajili tofauti. Kuna msamiati maalum na njia maalum ya utumiaji lugha. Katika miktadha ya wingilugha kila jamii ina mazoea yao ya kutumia maneno fulani,na labda maneno hayo kuwa na maana zisizo za kawaida kutegemea miktadha tofauti. Mada hii hivyo amechangia katika utafiti wetu wakati tulipokuwa tukitafitia changamoto za kimsamiati na kimaana katika sekta tulizotaja wakati wa kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha.Bila shaka mada hii imetuwekea msingi katika utafiti wetu kwa sababu ya mwingiliano baina ya mada hii na mada yetu ya utafiti .Hii ni kwa sababu mapengo ya kimsamiati na kimaana baina ya lugha ni changamoto katika kutafsiri. Mshindo (2010) ameangalia kauli hii kama dhima ya kutafsiri lakini kwa upande wetu kauli hii ilijitokeza kama changamoto.

### **1.8.1.6 Dhima ya Tafsiri katika Uchumi**

Wataalamu Mwansoko na wenzake (2006) na Mshindo (2010) wamejadili umuhimu wa tafsiri katika kuimarisha uchumi. Wameelezea kwamba uchumi wa nchi mara nyingi huangaliwa kwa kugegemea bidhaa za viwanda na biashara za mashirika ya kimataifa. Hizi ni zama za biashara za kimataifa ambazo huongozwa na mikataba ya maelewano. Mikataba hii kwa kawaida hutafsiriwa kwa lugha rasmi au lugha za mawasiliano ya mataifa yanayoshirikiana. Wanasema kuwa ni muhimu kuelewa lugha ya mkataba unaofunga, iwapo utafanikiwa kutathmini ipasavyo manufaa ya mkataba bayana kwa shirika lako. Mikataba mingi ya wafanyabiashara wa nchi kama Kenya au Tanzania kwa mfano, ingalitafsiriwa kwa Kiswahili, labda uchumi wa nchi hizi ungekuwa kwa haraka zaidi. Mada hii imezungumzia jinsi tafsiri inavyoweza kuimarisha uchumi wa nchi mbali mbali kwa kutafsiri mikataba ya kimaielewano ya kiuchumi katika lugha za mawasiliano.

Mada hii imekuwa na mchango katika utafiti wetu kwa sababu katika utafiti wetu tulitafitia manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha huku tukilenga sekta za afya, dini na elimu kama sekta ambazo zitapata manufaa. Katika maeneo yetu ya utafiti; Wilaya ya Narok Kaskazini, kuna aina nyingi za biashara ambazo hutekelezwa na watu mbali mbali ambao huzungumza lugha tofauti. Biashara hizi zina uhusiano na sekta ambazo tulizozitafitia. Kwa mfano, kuna mashule za kibinafsi ambazo ni za kulipiwa. Pia kuna hospitali na kliniki ambazo huduma zake hulipiwa. Iliwenye biashara kama hizi waweze kuwasiliana na kufanikisha biashara zao lazima waletwe pamoja na lugha inayoeleweka na wengi (lugha ya mawasiliano kama inavyoelezewa na wataalamu tunaowazungumzia). Katika muktadha wetu lugha husika ni Kiswahili. Tafsiri hapa ina jukumu kuu ya kupitisha ujumbe kutoka hizo lugha hadi Kiswahili na hivyo kuimarisha mawasiliano. Suala la dhima ya tafsiri katika uchumi basi lilitufaa sana katika utafiti wetu kwa sababu uchumi na biashara huenda sambamba.

### **1.8.1.7 Kutafsiri kama Kiliwazo**

Mwansoko na wenzake (2010) wameeleza kwamba katika kazi ya kutafsiri wapo baadhi ya watafsiri ambao huifanya kazi hii kama kiliwazo cha nafsi zao. Katika dhima hii kazi zinazoshughulikiwa ni kazi za kishairi.

Kutafsiri huku si kwa lengo lingine lolote lile bali kujiburudisha na kujiliwaza. Kazi hizi huwa kiliwazo cha mtafsiri kwa sababu tu mtafsiri huwa na amani hasa pale anapofanikiwa kuitafsiri kazi ambayo ilikuwa inampa shida kubwa akilini mwake. Mwansoko na wenzake (2006) wanaeleza kuwa tafsiri humfanya mtafsiri aburudike na kuridhisha nafsi yake kadiri anavyotatua matatizo yake ya kutafsiri. Kauli hii ya kutambua na kufurahia kazi ya kutafsiri, hakuvingiana moja kwa moja na mada yetu ya utafiti. Hata hivyo, kwa sababu imetumiwa kama moja wapo wa dhima za tafsiri, imetuwekea msingi ambao tumejengea manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Japo kwa kiwango kidogo tunaweza kusema mada hii imechangia katika utafiti wetu.

### **1.8.2 Vikwazo vya Tafsiri**

Katika sehemu hii tuliangalia maoni ya wataalamu; Duff A. (1981) na Biguenet J. na Schulte R. (1989). Tulingalia mchango wao, jinsi ulivyoingiliana na utafiti huu na jinsi utafiti huu ulivyoweza kunufaika na mada hii kulingana na wataalamu hawa. Wataalamu hawa: Duff A. (1981) na Biguenet J. na Schulte R. (1989) wamejadili na kutoa maoni yao kuhusu suala la vikwazo vya tafsiri chini ya mada ndogo zifuatazo;

(i) Tofauti za miundo ya lugha

(ii) Tofauti za mitindo ya lugha

Wataalamu hawa wamesema mitazamo tofauti ya nadharia ya tafsiri yaafiki kuwa mtafsiri anakumbwa na vikwazo vingi. Mtafsiri anapaswa kujihadhari na vikwazo hivi ili atafakari njia za kuvikabili. Lawama kubwa zaidi ya tafsiri ni upotovu wa maana. Upotovu wa maana huletwa na vikwazo vya tafsiri. Kikwazo ni kigezo chochote ambacho huletwa na vikwazo vya tafsiri. Kikwazo ni kigezo chochote ambacho hutatiza ufanisi wa kazi mahususi. Hebu tuangazie mada hizi.

#### **1.8.2.1 Tofauti za Miundo ya Lugha**

Kulingana na wataalamu hawa, viwango vya lugha kwa kuzingatia muundo wa lugha ni: grafolojia, fonolojia, leksia na sarufi.

Viwango muhimu katika mjadala huu ni vya leksia na sarufi. Tafsiri nyingi hutatizika kupitia mivutano ya mifumo ya leksia na kanuni za kisarufi. Katika kuangalia mifumo ya leksia inazingatiwa mahusiano na matumizi ya maana msingi.

Kwa kawaida, lugha hutofautiana kwa namna ambavyo zawasilisha maana msingi. Baadhi ya tofauti kati ya Kiswahili na Kingereza zajitokeza katika matini hizi:

**Kiswahili:** Nimevunjika mkono

**Kiingereza:** I have broken my arm/hand

Matini hizi zaonyesha tofauti za lugha hizi jinsi mbili;Kwanza,maana za Kingereza zimebainishwa zaidi ya zile za Kiswahili. Pale ambapo Kiingereza kina leksia mbili ‘arm’ na ‘hand’ Kiswahili kinatumia moja, ‘mkono’ mtafsiri wa Kingereza hajui kama atumie ‘hand’ au ‘arm’ kwa maana ya ‘mkono,’ pili kuna ukinzani wa mwelekeo wa dhana ya ‘kuumia’ kauli ya Kiswahili yaashiria kuwa mtu kamili ameumia sio mkono tu, kama ilivyo katika usemi wa Kingereza.Tofauti ya mwelekeo kuhusu maana inajitokeza katika falsafa ya ndoa. Katika Kiswahili, mwanamume huoa naye mwanamke huolewa. Kingereza hukubalia wote wawili kuo. Kwa matumizi haya maana hii imefumbata uwanda mpana zaidi. Lakini maana za Kingereza zimejitofautisha zaidi kwa upande mwingine. Hebu zingatia tafsiri;

**Kiingereza**

**Kiswahili**

He married his sister

Alimwoa nduguye

She married her brother

Aliolewa na nduguye

Isipokuwa pale msemaji arejelea ndugu mkubwa, yaani dada au kaka, leksia ya Kiswahili haitofautishi jinsia hata katika matumizi ya viwakilishi.Katika sehemu hii tumefafanuliwa vikwazo vya tafsiri kwa kuzingatia tofauti za miundo ya lugha. Mada hii imeingiana na mada yetu ya utafiti kwa sababu tumetafitia changamoto za kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Kupitia kwa mifano tumeona jinsi mifumo ya kileksia na kanuni za kisarufi zinavyozua ukinzani na kulete vikwazo katika kutafsiri lugha moja hadi nyingine. Kauli hii imekuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu imetupa mwelekeo katika kuangazia changamoto za kutafsiri.

Katika utafiti wetu tulihusisha Kiswahili na lugha zingine hususan Kimaasai ambayo ndiyo lugha ya wenyeji wa maeneo yetu ya utafiti- Wilaya ya Narok Kaskazini. Kama tulivyoelezea hapo awali maeneo yetu ya utafiti yako katika muktadha wa wingilugha. Lugha tofauti tofauti zinazozungumzwa bila shaka zina mifumo tofauti za kileksia na kanuni tofauti za kisarufi.

Kwa sababu tumetafitia changamoto za kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza na kutafsiri kutoka lugha hizo za kwanza hadi Kiswahili, mada hii imetuekea msingi utakao imarisha utafiti wetu.

### **1.8.2.2 Tofauti za Mitindo ya Lugha**

Wataalamu Duff(1981) na Biguenet J. na Schulte R. (1989) wanasema kuwa mitindo ya lugha pia ni sajili za lugha. Dhana ya sajili huhusika iwapo matumizi ya mtindo wa lugha hulingana na mahitaji ya taluma bayana, kama vile isimu, fasihi, sheria, matibabu na uhandisi miongoni mwa sajili zingine. Sajili vile vile hueleza sura bainifu za muktadha pana wa mawasiliano na mtagusano wa mawasiliano na wa kijamii. Baadhi ya miktadha pana ni mazungumzo ya kawaida, mazungumzo ya biashara na mafunzo ya dini. Sajili ya lugha hubainika kupitia mbinu tatu za matumizi ya lugha. Mbinu hizi ni uteuzi wa msamiati, muundo na maumbo ya sentensi na muwala wa matini. Muundo wa sentensi unahusu sheria za sarufi na ukubalifu, nayo maumbo hueleza mahusiano ya vishazi vya tungo moja. Mtiririko wa matini nao hufuma maana ya ujumbe. Kupitia ukinzano wa mitindo ya lugha, wataalamu hawa wamebainisha vikwazo vinne vya tafsiri; istilahi, majina ya kudumu, unukuzi na mafumbo na semi za lugha.

Katika sehemu hii wataalamu husika tuliowataja wamezungumzia kuhusu vikwazo vya tafsiri wakijikita katika tofauti za mitindo ya lugha. Wameangazia suala la sajili mbali mbali na kutaja jinsi lugha inavyo husiana na sajili husika katika jamii. Mada hii ina uhusiano na mada yetu ya utafiti kwa sababu, tulitafitia maeneo tofauti tofauti kama vile sekta za elimu, dini, na afya, sekta hizi zilibainika kama sajili tofauti tofauti. Hivyo mada hii ya tofauti ya lugha kulingana na sajili tofauti imekuwa mwafaka katika utafiti wetu. Katika jamii yoyote ile hapakosi vikundi mbali mbali ambavyo huletwa pamoja na shughuli au mambo mbalimbali, kwa mfano umri, kazi, biashara, uraibu na kadhalika. Makundi kama haya huwa na mitindo yao ya kuwasiliana, na msamiati teule unaojikita katika makundi mahususi hutumika. Hivyo basi kama mtu si wa kikundi fulani huenda akakosa kuelewana na kikundi kama hicho.

Hali kama hii yaweza kuadhiri au kuwa kikwazo cha mchakato wa kutafsiri haswa katika muktadha wa wingilugha. Katika utafiti huu kwa sababu tulishgulikia suala la wingilugha, suala la sajili bila shaka liliibuka.



Tumeona jinsi suala la sajili linavyoweza kuwa kikwazo katika tafsiri. Kauli hii imetusaidia katika kutafitia changamoto za kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Ingawaje wataalamu hawa tuliowarejelea katika utafiti huu hawakushughulikia suala hili la sajili kwa kina na kwa umahususi na kuzua pengo, tumefidia kwa kujikita katika sajili malum katika maeneo yetu ya utafiti kwa mfano maeneo ya kielimu, kidini na kiafya na kuelezea kwa kina jinsi changamoto zilivyojitokeza katika sajili hizi zilivyoadhiri mchakato wa kutafsiri kwa Kiswahili hadi lugha zingine za kwanza na kinyume. Hivyo mada hii kwa kiasi ilituekea msingi tulioendelezea utafiti wetu.

Kwa jumla katika sehemu hii yote tumeona jinsi mada ya dhima ya tafsiri ilivyojadiliwa na wataalamu Mwansoko na wenzake (2006) na Mshindo(2010). Kilicho dhihirika katika mjadala wao ni kwamba tafsiri ina umuhimu katika kuimarisha mawasiliano katika jamii. Nao wataalamu: Duff A.(1981) na Biguenet J. na Schulte R. (1989) wameangazia suala la vikwazo vya tafsiri. Wametuonyesha jinsi vikwazo hivi vinavyodhihirika kwa kupitia tofauti za miundo ya lugha na tofauti za mitindo ya lugha.

Kulinga na uelewa wetu kuhusiana na utafiti wao na mada yao, ni kwamba wamepitisha ujumbe kwamba katika mchakato wa kutafsiri kuna vikwazo ambavyo huibuka na kutatiza shughuli ya kutafsiri. Kama tulivyoelezea katika sehemu ambazo zimetangulia mada hizi mbili kuu: Vikwazo vya tafsiri na dhima ya tafsiri kwa njia moja au nyingine zimeingiana na mada yetu ya utafiti kwa sababu tumetafitia changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Katika manufaa ya tafsiri kwa mfano, tuliangazia sekta za elimu, afya na dini. Katika changamoto katika kutafsiri tuliangazia changamoto zinazoibuliwa na tofauti zakitamaduni na tofauti za miundo ya lugha.

Kwa jumla tunaweza kusema kuwa wataalamu waliojadili na kutafitia mada hizi mbili kuu ambazo tumezjadili wamefikia ufanisi kiasi. Kuna upungufu ambao amedhihirika. Watafiti wote wameelezea mada zao kijuujuu na kwa ujumla tu. Katika maelezo waliyoyatoa kulingana na tafiti zao kuhusiana na mada zao, hatukuweza kubainisha ama hawajabainisha wamejikita katika nadharia gani. Hata hivyo mada zao zimetuekea msingi ambao uliendeleza utafiti wetu. Ili kufidia mapengo ambayo tumeelezea, mada zetu zimeelezewa kwa kina, kimahususi na wazi. Ili kufidia suala la kinadharia utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya mawasiliano katika tafsiri na mtaalamu Peter Newmark mwaka wa 1982.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Katika utafiti wetu, tulinuwia kupata data mwafaka na za kuaminika. Ili kuafikia malengo haya tuliteua mbinu mwafaka za kimsingi. Miongoni mwa mbinu za kimsingi ni pamoja na: Mahojiano-tulifanya mahojiano miongoni mwa watu kutoka asasi mbalimbali na tabaka mbali mbali. Tuliwahoji watu katika sekta za elimu, dini na Katika sekta ya afya. Katika kila sekta tuliwahoji watu kati ya kumi na watano hadi ishirini ili kupata sampuli mwafaka. Data tulizokusanya zilijikita katika msamiati wa lugha za Kimaasai na Kiswahili. Msamiati uliegemea maeneo ya aina ya vyakula, aina ya mavazi na mapambo, mipangilio katika jamii kama aina za semi, imani, mazingira na uvumbuzi wa kisayansi na teknolojia, majina ya kurejelea wapendwa, umri na rika, koo na mbari na hali ya kuzawadiana katika jamii. Tuliwahoji watu wa umri tofauti tofauti kati ya miaka kumi na kuendelea ili kupata uwakilishi wa watu wote (watoto na watu wazima). Kikundi hiki kilikuwa na uwezo wakujieleza na kujibu maswali ya mahojiano. Katika mbinu za kimsingi pia, tulihusisha mbinu ya kutazama au kuchunguza. Tuliingia maeneo mbalimbali na kuchunguza jinsi watu wanavyotangamana na kuwasiliana katika shughuli zao. Katika kutazama na kuchunguza tulizingatia jumbe katika mabango, maandishi katika kuta za mashule, hospitali, na maeneo ya kuabudu. Tulizingatia pia maandishi kwenye vibao vya kuelekeza watu mashuleni, hospitalini na maeneo ya kuabudu. Katika utafiti wetu pia, data za upili zilitufaa. Tulisoma makala za kiusomi zilizohusu tafsiri, miundo ya lugha katika viwango vya grafolojia, fonolojia, leksia, sarufi na tulitafitia pia miundo ya lugha tunganishi na lugha ambishi. Tulitembelea maktaba na kusoma tasnifu, vitabu, majarida na maandishi mengine kuhusu tafsiri na ambayo yalifaa utafiti wetu. Tulifanya utafiti kwenye mtandao pia. Tulitembelea tuvuti mbalimbali za mashirika na taasisi tofauti ili kupata data zaidi. Tulikusanya data zetu kwa kuziandika na kuzihifadhi kwenye daftari. Tumezungua data kulingana na maeneo ya ukusanyaji na kuziwasilisha kwa kuziorodhesha katika makundi ya maeneo na pia katika jedwali. Tumezichanganua data kwa kufafanua na kuelezea.

## **1.10 HITIMISHO**

Katika sura hii ya kwanza tumetanguliza kwa kuangazia dhana ya wingi lugha kulingana na mada yetu. Tumeona jinsi wingi lugha unavyoibuka na matokeo yake. Tumeangalia mchango wa wataalamu wengine na kuonyesha pengo lililoibuka. Tatizo la utafiti limeelezwa kikamilifu. Madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti yamefafanuliwa. Utafiti huu umeweka bayana sababu za kuchagua mada na kuonyesha upeo na mipaka ya utafiti. Msingi wa kinadharia na yaliyoandikwa kuhusu mada pia yaliangaziwa kikamilifu. Hatimaye njia za utafiti zimeelezwa na kufafanuliwa kwa kina.

## **SURA YA PILI**

### **CHANGAMOTO KATIKA TAFSIRI ZINAZOSABABISHWA NA MIFANYIKO YA KITAMADUNI**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii tumeangazia changamoto ambazo zimeibuka na kutatiza shughuli na mchakato wa kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza (tuliteua lugha ya Kimaasai kuwakilisha lugha za kwanza) na vile vile kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili inavyoweza kutatizwa. Taaluma ya tafsiri imechangia pakubwa katika kuimarisha mawasiliano baina ya lugha moja hadi lugha nyingine. Kwa mfano, hali ambapo watu kutoka jamii tofauti wanaozungumza lugha tofauti na kukosa kuelewana. Tafsiri hutumika kuhawilisha taarifa, ujumbe, tahadhari na mambo mengine mengi kutoka lugha moja hadi lugha nyingine kupitia kwa maandishi au lugha ya usemi. Hata hivyo, ingawaje taaluma ya tafsiri imefanikiwa kuimarisha mawasiliano, taaluma hii imekumbwa na changamoto kadhaa. Changamoto hizi zimechochewa na tofauti zilizopo baina ya lugha tofauti tofauti. Katika utafiti wetu katika hii sura tumeangazia changamoto ambazo zimesababishwa na mifanyiko ya kitamaduni.

#### **2.2 Changamoto Zinazosababishwa na Tofauti za Kitamaduni**

Kila jamii ina utamaduni wake. Tamaduni hizi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Jamii tofauti tofauti huwa na mitazamo tofauti kuhusu mambo na dhana tofauti na hali hii ni kulingana na itikadi, imani, mila na desturi za jamii husika. Lugha ni mfano wa dhana ambayo imemilikiwa, imefungamanishwa na kuzaliwa kutoka utamaduni fulani. Hii inamaanisha kuwa ili mtu kuelewa lugha fulani na dhana zinazohusishwa na hiyo lugha, itabidi awe mzawa wa utamaduni husika ama awe na tajiriba ya utamaduni huo. Hivyo, utamaduni umekuwa changamoto katika shughuli ya kutafsiri. Hebu tuzingatie mifano ifuatayo:

##### **2.2.1 Aina za Vyakula vya Kitamaduni katika Jamii ya Wamaasai.**

- i) Madida – Aina ya chakula, kati ya ugali na uji, hupikwa kwa kutumia unga wa mahindi, huongezwa ladha kwa chumvi kidogo, sukari na mafuta.

- ii) Munono – Aina ya chakula ambacho huundwa kwa nyama ya mbuzi au kondoo. Hukatwakatwa vipande vidogo sana kisha hukaushwa kwa kukaangwa na mafuta na kisha kuchanganywa na damu.
- iii) Orketutu – Aina ya ugali mgumu sana, hukaushwa hadi kuwa chenga chenga, huongezwa mafuta na chumvi. Huliwa pamoja na chai wakati wa kiangazi wakati ambapo maziwa yameadimika.
- iv) Orpurda – Aina ya nyama haswa ya mbuzi au kondoo. Huandaliwa kwa kukaangwa kwenye mafuta mengi hadi kukauka. Nyama zenyewe huachwa kupoa na kushikamana na mafuta. Huweza kuhifadhiwa kwenye mafuta hadi mwezi mmoja. Huliwa haswa na akina mama waliojifungua na vijana waliopashwa tohara.

Itakuwa vigumu kutafsiri aina hivi ya vyakula katika lugha ya Kiswahili kwa sababu hamna visawe vyake katika Kiswahili. Majina kama haya ya aina ya vyakula ambavyo vimejikita katika utamaduni wa jamii ya Wamaasai huleta changamoto kwa mtafsiri anapotaka kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili. Vile vile kuna vyakula ambavyo si maarufu miongoni mwa jamii ya Wamaasai na ambavyo ni maarufu katika jamii zingine na hurejelewa kwa Kiswahili. Mifano ni kama:

- i) Pilau
- ii) Biriani
- iii) Makande
- iv) Viazi karai
- v) Mshikaki

Vyakula hivi havina visawe vyake katika lugha ya Kimaasai na pia havina mashikilio katika utamaduni wa Kimaasai. Hivyo changamoto huzuka katika kutafsiri majina haya ya vyakula kutoka Kiswahili hadi Kimaasai.

### **2.2.2 Hali ya Kubadilishana au Kuzawadiana Kuimarisha Uhusiano katika Jamii.**

Katika jamii ya Wamaasai kuna hali ambapo watu hutoa zawadi haswa wanyama. Hii ni ishara ya kudumisha uhusiano mwema na urafiki. Kuna majina ambayo hutumika kurejelea jinsi watu huitana kutegemea mtu alizawadiwa mnyama gani.

Kama mtu amezawadiwa mnyama fulani basi mtu huyo atamwita aliyemzawadia kwa jina fulani. Aliyetoa zawadi ya mnyama fulani pia atamwita aliyempa zawadi kwa jina hilo hilo. Kwa mfano katika jamii hii, utasikia watu wakiitana:

- i) Pasikiria- ni zawadi ya punda
- ii) Esupen – zawadi ya mbuzi wa kike ambaye hajazaa.
- iii) Pakishu – ng’ombe ametolewa kama zawadi.
- iv) Pakuo – mwanambuzi ametolewa kama zawadi.
- v) Pakine – mbuzi wa kike aliyezaa ametolewa kama zawadi.
- vi) Paker – kondoo wa kike ametolewa kama zawadi.
- vii) Pakiteng’ – fahali ametolewa kama zawadi.
- viii) Paashe – ndama ametolewa kama zawadi.

Mtu aliyetoa zawadi na aliyepokea zawadi huitana kwa majina hayo tuliyoorodhesha. Itakuwa ni changamoto kutafsiri majina kama haya kutoka Kimaasai hadi Kiswahili kwa sababu hayana visawe na pia hayaingiani na utamaduni wa Kiswahili. Kama mtafsiri hatoki katika utamaduni wa Kimaasai au hana tajiriba ya utamaduni huu, itakuwa ni changamoto kwake kutafsiri majina au maneno hayo ya Kimaasai hadi Kiswahili.

### **2.2.3 Majina ya Kurejelea Wapendwa**

Katika jamii ya Wamaasai, kuna majina ambayo wazee na wanawake walio na umri mkubwa hutumia kuwaitia watoto wao, wajukuu wao na watu wa umri mdogo katika jamii. Jambo hili hufanyika ili kuonyesha upendo kutoka kwa wazee na wanawake wakongwe na kuwapa shime watoto wao na kizazi kichanga. Tuangalie baadhi ya majina ambayo hutumika:

<b>Kimaasai</b>	<b>Kiswahili</b>
i) Osikiria lai:	Punda wangu
ii) Enkoshoke ai:	Tumbo langu
iii) Enkutuk ai:	Mdomo wangu
iv) Enkaji e yieyio:	Nyumba ya mama
v) Enkaina ai:	Mkono wangu
vi) Nkonyek ainei:	Macho yangu

- vii) Enkeju ai: Mguu wangu
- viii) Enkarna ai: Jina langu
- ix) Enkiteng ai: Ng'ombe wangu

Ingawaje majina haya ya Kimaasai yana visawe katika lugha ya Kiswahili, yana maana tofauti kando na maana yake yakimsingi iliyozeleka. Majina yaliyotumika katika kuwarejelea wapendwa ni majina ya wanyama na majina ya sehemu za mwili. Majina haya hayarejelei wanyama au sehemu za mwili, bali yanasisitiza upendo na ile hali ya mshikamano katika jamii. Kwa hivyo, iwapo mtafsiri hana uelewa wa utamaduni huu wa Kimaasai, anapotafsiri majina haya hadi Kiswahili basi atasababisha upotovu wa maana na kutatiza mawasiliano.

#### **2.2.4 Aina za Mavazi na Mapambo**

Kama ilivyo katika tamaduni zingine, jamii ya Wamaasai ina aina ya mavazi na mapambo kulingana na utamaduni wao. Mavazi kama haya na aina mbalimbali ya mapambo hurejelewa kwa majina maalum. Tuangalie baadhi ya majina yanayorejelea aina ya mavazi na mapambo:

- i) Elokesea – vazi la kina mama la kuvaliwa chini – aina ya sketi ya shuka.
- ii) Enchoriba – aina ya vazi la ngozi nyororo ambalo huvaliwa na wazee.
- iii) Enkarewa – aina yapambo lililotengezwa kwa shanga na ngozi. Huvaliwa shingoni na huning'inia hadi miguuni. Huvaliwa na akina mama na wasichana.
- iv) Enkatar – aina yapambo ambalo hutengenezwa kwa kutumia nyaya nyembamba na shanga na ambazo huvaliwa kwa kuviringishwa miguuni.
- v) Orkatar – aina ya pambo ambalo hutengenezwa kwa kutumia waya nyembamba na shanga. Huvaliwa shuingoni na wanawake kwa waume.
- vi) Enkirina – aina ya bangili ambayo hutengenezwa kwa kutumia aina fulani ya mpira au ngozi na shanga. Huvaliwa mkononi kama pambo.
- vii) Enkishili – aina ya pambo la bibi harusi ambalo hutengezwa kwa ngozi na shanga na huvaliwa kichwani.
- viii) Orkeliai – aina ya pambo, hutengenezwa kwa shanga, ngozi au mipira. Huvaliwa shingoni na wanaume na wanawake.
- ix) Imuna – pambo ambalo hutengezwa Kwa shanga na waya ambalo huvaliwa masikioni na wazee na wanawake.

- x) Enkitati – aina ya mshipi mpana uliotengezwa kwa ngozi ya ng’ombe. Huvaliwa na wanawake.

Mavazi haya na mapambo yana majina maalum kulingana na utamaduni wa Wamaasai. Ni vigumu kupata visawe vya majina haya katika lugha ya Kiswahili. Kuelezea majina haya kutoka lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili, itabidi mtafsiri awe na ujuzi wa kitamaduni ya Wamaasai ama awe ametoka katika jamii hii. Hali hii inapelekea kuwa na changamoto katika kutafsiri. Vile vile kuna mavazi ambayo si maarufu katika jamii ya Wamaasai na ambayo hurejelewa kwa majina ya Kiswahili. Mifano ni pamoja na:

- i) Kanzu
- ii) Kitenge
- iii) Kikoi
- iv) Rinda
- v) Kizibao
- vi) Kabuti
- vii) Kaptula
- viii) Surupwenye
- ix) Buibui
- x) Kanchiri

Ni changamoto kwa mtafsiri kutafsiri na kuelezea majina kama haya kutoka Kiswahili hadi Kimaasai kwa sababu hamna visawe vyake katika lugha ya Kimaasai na vile vile hayashikamani na utamaduni wa Kimaasai.

### **2.2.5 Dhana ya Ekolojia**

Ekolojia hurejelea suala la tabia za kijiografia, mazingira, tabia nchi, hali ya hewa na kadhalika. Tabia na hali kama hizi kwa kawaida zinaweza kutofautiana kati ya utamaduni wa jamii moja na jamii nyingine. Kwa mfano tuzingatie aina zifuatazo za mandhari:

- i) Ufuo / ufuko (wa bahari)
- ii) Theluji
- iii) Volkano



Mandhari kama haya hayapatikani au hayahusiki moja kwa moja na utamaduni wa jamii ya Wamaasai. Kuleta dhana kama hizi kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kimaasai itakuwa ni changamoto kwa mtafsiri wa Kiswahili kutafsiri hadi Kimaasai. Vile vile, tunapoangazia mazingira fulani tunapata, kwa mfano, mimea fulani ambayo inahusishwa na tamaduni za jamii fulani. Kwa mfano:

- i) Mnazi
- ii) Mparachichi
- iii) Muarobaini
- iv) Makuti

Majina haya ambayo yanarejelea aina ya mimea, ni maarufu miongoni mwa Waswahili wanaoishi mwambao wa pwani. Majina haya ambayo yamerejelewa katika lugha ya Kiswahili yanaleta changamoto yanapotafsiriwa hadi lugha ya Kimaasai. Sababu kuu ya changamoto hizi ni kwamba mimea hii haihusiani na utamaduni wa Kimaasai.

#### **2.2.6 Rika na Umri katika Jamii**

Katika utamaduni wa jamii ya Wamaasai kuna swala la rika na umri ambayo hupewa kipaumbele na kuheshimiwa. Katika jamii hii kuna majina ambayo hurejelewa kutofautisha makundi mbali mbali katika jamii. Makundi haya hujumuishwa kulingana na umri na wakati (mwaka) ambapo mwanamume alipashwa tohara. Majina haya hivyo husimamia watu katika jamii na ambao ni wa rika moja kwa misingi ya kiumri na wakati wa kupashwa tohara. Rika hizi hubuniwa kila baada ya miaka kumi hadi miaka kumi na tano. Baadhi ya rika hizi katika jamii hii husika ni pamoja na:

- i) Iiterito
- ii) Inyangusi
- iii) Iseuri
- iv) Irambauni
- v) Irkishili
- vi) Irmeshuki

Ili mtafsiri aweze kutafsiri ama kuelezea makundi haya kutoka lugha ya Kimaasai hadi lugha ya Kiswahili, itabidi mtafsiri awe na uelewa wa utamaduni huu. Hii ni changamoto katika kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili.

### **2.2.7 Koo au Mbari katika Jamii**

Katika jamii hii ya Wamaasai kuna majina maalum ambayo yanatumwa kurejelea ukoo au mbari fulani. Koo hizi ni familia pana zinazounda jamii moja ya Wamaasai. Walio katika ukoo mmoja hushimiana sana, huonana kama ndugu na hawawezi kuoana. Mifano ya koo au mbari hizi ni pamoja na:

- i) Ilmakesen
- ii) Ilmolelian
- iii) Ilukumai
- iv) Iltaaroserero
- v) Ilkerin – ingishu
- vi) Ilmeponi.

Majina haya ya Kimaasai ambayo yanarejelea koo au mbari, hayana visawe vyake katika lugha ya Kiswahili. Dhana kama hii ya koo ama mbari inapojitokeza katika kutafsiri Kimaasai hadi Kiswahili inazua changamoto. Changamoto yenyewe inasababishwa na tofauti za kitamaduni baina ya lugha ya Kimaasai na Kiswahili.

### **2.2.8 Uvumbuzi wa Kisayansi na Teknolojia**

Uvumbuzi na ubunifu wa kisayansi na teknolojia umeathiri sana utamaduni wa lugha hasa katika mataifa ya nchi zinazoendelea. Utamaduni wa nchi zilizoendelea umepitishwa hadi katika tamaduni zingine. Hali hii husababisha wanaotafsiri kushindwa kupata visawe mwafaka kwa baadhi ya maneno katika utamaduni wa nchi zilizoendelea. Lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha ya mawasiliano katika maeneo yetu ya utafiti pia imeathiriwa na kuishia kutohoa maneno kama hayo kutoka lugha husika ya mataifa yalioendelea na kuyarekebisha tu kisarufi na kimatamshi. Inakuwa ni changamoto kutafsiri maneno kama haya kutoka Kiswahili ( maneno yaliyotoholewa) hadi lugha ya Kimaasai. Kwa mfano:

**Kiswahili****Kimaasai**

i) Redio	_____
ii) Kemikali	_____
iii) Dijitali	_____
iv) Telefaksi	_____
v) Hadiwea	_____
vi) Softiwea	_____
vii) Kamera	_____
viii) Maikrowevu	_____
ix) Dekoda	_____
x) Memori (kadi)	_____

**2.2.9 Imani kama Changamoto katika Kutafsiri**

Utamaduni wa Waswahili umeathiriwa kwa kiasi fulani na utamaduni wa lugha ya Kiarabu ambayo waumini wake wengi ni Waislamu. Kuna majina mengi ambayo yanarejelewa katika lugha ya Kiswahili ambayo yamejikita katika imani ya Kiislamu. Inakuwa ni vigumu kutafsiri majina kama haya kutoka Kiswahili hadi Kimaasai kwasababu hamna visawe vyake katika lugha ya Kimaasai. Changamoto hii inaletwa na tofauti kubwa iliyoko ya utamaduni unaofungamanisha imani na itikadi. Hivyo panazuka changamoto katika kutafsiri maneno au majina yafuatayo kutoka Kiswahili hadi Kimaasai:

- i) Kadhi
- ii) Hijabu
- iii) Mikabu
- iv) Sheikh
- v) Muktadh

**2.2.10 Semi kama Changamoto katika Kutafsiri**

Semi ni tungo au kauli fupi fupi za kisanaa zenye lugha ya mafumbo ambazo hukusudia kuleta mafunzo kwa jamii husika. Semi ni moja wapo ya vipengele vigumu katika kufanyia kazi ya kutafsiri. Hii inasababishwa na tofauti kati ya utamaduni wa jamii moja na nyingine.

Semi hizi zinaweza zikatumika katika jamii moja na jamii nyingine zisitumike semi hizo. Kwa hivyo itakuwa changamoto kutafsiri semi za Kiswahili zifuatazo hadi lugha ya Kimaasai:

#### **2.2.10.1 Methali**

- i) Ndondondo si chururu, chururu si ndondondo.
- ii) Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma.
- iii) Afadhali wahed shika, kuliko kenda nenda rudi.

#### **2.2.10.2 Nahau**

- i) Mkono mrefu (mwizi)
- ii) Zunguka mbuyu (toa rushwa)
- iii) Kupata jiko (kuoa)
- iv) Piga maji (kunywa pombe)
- v) Ramba kisogo (kusengenywa)

#### **2.2.10.3 Misimu**

- i) Amenitoanisha (nimempa fedha)
- ii) Mpango wa kando (kutoka nje ya ndoa)
- iii) Amejaa upepo (amekasirika)
- iv) Mambo ni London (maisha ya juu)

#### **2.2.10.4 Vitendawili**

- i) Kuku wangu anatagia mibani (nanasi)
- ii) Popo mbili zavuka mto (macho)
- iii) Parr hadi Meka (utelezi)
- iv) Mwaarabu mweupe husimama kwa mguu mmoja ( uyoga)

#### **2.2.10.5 Misemo**

- i) Mtu ni afya ( kuzingatia usafi)
- ii) Maji ni uhai (kulinda vyanzo vya maji)
- iii) Miti ni mali (kulinda misitu au kuhifadhi mazingira)

iv) Mtoto ni mamake (malezi bora)

### **2.2.11 Dhana zingine za Kitamaduni ambazo Hutatiza Tafsiri**

(i) Dhana ya Utajiri

Kulingana na utamaduni wa Kimaasai, utajiri huhusishwa na wanaume pekee. Mwanamume anayehesabiwa kuwa tajiri anaangaliwa kwa misingi ya idadi ya wake aliyooa, idadi ya mifugo aliyonao na ukubwa na idadi ya mashamba aliyonayo. Hivyo hata ikiwa mtu ana fedha nyingi, kazi ya kifahari na mijengo, kama hana mifugo na wake wengi, kulingana na utamaduni wa kimaasai, mtu kama huyo ni fukara. Suala la utajiri hivyo, linapotafsiriwa kutoka Kiswahili hadi Kimaasai kwa misingi ya jinsi utajiri unavyoeleweka katika misingi ya Kiswahili, basi patakuwa na upotovu wa maana.

ii) Dhana ya Jinsia.

Katika utamaduni wa Kimaasai, mwanamke huhesabiwa au huchukuliwa kama mtoto. Katika lugha ya Kimaasai neno 'Enkerai' – hurejelea mtoto, na katika muktadha mwingine, mwanamke au mke. Hivyo, katika hali ya kujuliana hali ama salamu, maneno yafuatayo hutumiwa: kejaa enkerai ( habari ya watoto), ambapo kauli hii inamaanisha habari ya familia, yaani mke na watoto. Kauli kama hii inazua changamoto katika kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili. Iwapo mtafsiri haelewi utamaduni huu wa Kimaasai basi anaweza kutafsiri visivyo kutoka Kimaasai hadi Kiswahili.

### **2.3 HITIMISHO**

Katika sura hii ya pili tumeangalia changamoto zinazoibuka katika kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Tumeangazia changamoto hizo wakati ambapo tafsiri inapotekelezwa kutoka Kimaasai (lugha ambayo tumetumia kuwakilisha lugha zingine katika muktadha wa wingilugha) hadi Kiswahili na vile vile kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kimaasai. Tumeweza kubainisha tofauti ambazo zinatofautisha lugha ya Kiswahili na ya Kimaasai. Tumebainisha jinsi tamaduni za lugha hizi mbili zinavyotofautiana katika maeneo yafuatayo: Mavazi na mapambo, aina za vyakula, dhana ya rika katika jamii, dhana ya koo/mbari katika jamii, majina ya kurejelea wapendwa katika jamii kwa kurejelea Wamaasai na Waswahili.

Tumeona katika tamaduni hizi, ya kwamba kuna majina na maneno maalum ambayo hutumika. Majina na maneno kama haya huwa yamefungamana na utamaduni husika. Tumeona ya kwamba mtafsiri asipokuwa na uelewa wa tamaduni husika basi atakumbwa na changamoto katika kazi yake ya kutafsiri. Tumetoa mifano maridhawa kutoka lugha ya Kimaasai na pia kutoka lugha ya Kiswahili ili kuthibitisha jinsi changamoto katika kutafsiri zinavyosababishwa na tofauti za kitamaduni.

## SURA YA TATU

### CHANGAMOTO ZINAZOSABABISHWA NA TOFAUTI ZA MIUNDO YA LUGHA

#### 3.1 Utangulizi

Kakika sura ya pili tumeona jinsi tafsiri inavyokumbwa na changamoto zinazohusishwa na mifanyiko ya kitamaduni. Katika sura hii ya tatu tumeendeleza changamoto zinazokumba mchakato wa kutafsiri katika muktadha wa wingilugha. Tumeangazia changamoto ambazo zinaibuliwa na tofauti za miundo ya lugha. Muundo wa lugha kimsingi hubainishwa kwa viwango vinne:

##### (i) Grafolojia

Grafolojia ni taaluma ya mwandiko, yaani uwakilishi wa maandishi, maandishi na sifa za mfumo wa hati andishi. Tafsiri grafolojia, kwahivyo ni uwakilishi wa hati za mfumo bayana kwa hati linganifu za mfumo tofauti.

##### (ii) Fonolojia

Fonolojia ni mfumo wa sauti za lugha. Taluma ya fonolojia inazingatia muundo, sifa na ruwaza za sauti zinavyotumika katika mfumo wa sarufi bayana na lugha kwa jumla. Tafsiri fonolojia huwakilisha sauti na ruwaza za sauti za lugha chanzi kwa zile linganifu za lugha pokezi.

##### (iii) Leksia

Leksia ni mfumo wa maneno yenye maana ya kimsingi ya lugha moja. Mfumo wa maana za kimsingi pamoja na maumbo ambayo huwakilisha maana hizo, zote huitwa leksia. Tafsiri leksia ni uwasilishi wa maana za kimsingi za lugha chanzi kwa visawe vya lugha pokezi.

##### (vi) Sarufi

Sarufi ni mfumo wa sheria unaotawala maumbo ya maneno na muundo wa sentensi. Maumbo na muundo ni vipengele vya sarufi ambavyo hulingana na taaluma za morfolojia na sintaksia. Tafsiri sarufi, hata hivyo inarejelea maneno ya kimuundo yaani maneno ambayo hutumika kwa kuunda sentensi bila yenyewe kubeba maana za kimsingi.

Kwa kuzingatia kigezo cha sarufi na leksia, lugha za Kimaasai na Kiswahili ni tofauti. Tofauti hii husababishwa na sababu za kimaeno na shughuli za kujikimu kimaisha. Uainishaji wa lugha kimuundo ni kigezo ambacho hutumiwa zaidi ya vigezo vingine kwa sababu hurejelea muundo wa lugha yenyewe na kwa sababu hii huonekana kuwa na uhalisia zaidi. Wanaisimu huzigawa lugha kimuundo kwa kuzingatia vigezo viwili:

(i) Lugha tetanishi

Katika kigezo hiki maneno katika lugha ambazo ziko katika kikundi hiki hayakubali kunyambuliwa au kuambishwa. Lugha kama hizi zina maneno yenye mofu moja tu na ambayo huwakilisha mofimu moja.

(ii) Lugha ambishi

Katika lugha ambazo ziko katika kikundi hiki maneno ya lugha hizi huongezwa viambishi mbalimbali ambavyo hubeba maana tofauti tofauti. Katika lugha hizi viambishi na mizizi huwa hivichanganyiki kwa hivyo inawezekana kutofautisha mizizi na viambishi.

### **3.2 Kauli ya Uambishaji kama Changamoto katika Kutafsiri**

Kulingana na maelezo hayo hapo juu kuhusu lugha tetanishi na lugha ambishi; lugha ya Kimaasai ni lugha tetanishi ambapo maneno mengi tu katika lugha hii hayawezi kuongezewa viambishi kwenye mizizi yake au kunyambuliwa. Kiswahili kwa upande wake ni lugha ambishi. Maneno ya Kiswahili yanaweza kuongezewa viambishi mbali mbali kwenye mizizi yake au kunyambuliwa. Tuangalie mifano ifuatayo:

Mzizi;

-pig-pig-a, pig-ana, ali-pig-ania, ana-pig-wa

-chez- mchez-aji, chez-ea-chez-eana, wana-chez-esha

-som- ana-som-a, wana-som-eshana, ana-som-a-som-a, ali-som-ewa

-lim-wana-lim-iana, ana-lim-ishwa, lim-iwa, -lim-ishiana, lina-lim-ika



Sifa hii ya uambishaji inawezesha vitenzi vya Kiswahili kunyambuliwa katika kauli tofauti tofauti kwa mfano;

i)Kauli ya kutenda

Piga

Choma

Sema

Ruka

Lala

ii) Kauli ya kutendea

Pigia

Lalia

Rukia

Chukulia

Kimbilia

iii)Kauli ya kutendwa

Pigwa

Semwa

Chomwa

iv)Kauli ya kutendeka

Imbika

Semeka

Kimbilika

v) Kauli ya kutendesha

Limisha

Tobolesha

Bebesha

Jengesha

Ogesha

vi) Kauli ya kutendana

Pendana

Chomana

Pigana

Katana

Patana

vii) Kauli ya kutendama

Funga- fungama

Ganda-gandama

viii) Kauli ya kutendata

Fumba – fumbata

Katika lugha ya Kimaasai vitenzi haviwezi kunyambulia katika kauli nyingi kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili, tuzingatie mifano ifuatayo;

**(i) Kiswahili**

<b>Kitenzi</b>	<b>Kauli ya kutendesheana</b>
Lima	Limishiana
Endesha	Endesheana
Panda	Pandishiana
Cheka	Chekesheana
Lia	Lilishiana
Lipa	Lipishiana
Soma	Somesheana

**Kimaasai**

<b>Kitenzi</b>	<b>Kauli ya kutendesheana</b>
Iremo	_____
Terewa	_____
Takedo	_____
Takuenia	_____

Inchira	_____
Talaa	_____
Isuma	_____

---

**ii) Kiswahili**

<b>Kitenzi</b>	<b>Kauli ya kutendesheka</b>
Pika	Pikishika
Cheza	Chezesheka
Sema	Semesheka
Cheka	Chekesheka
Soma	Somesheka
Endesha	Endesheka
Lima	Limishika

<b>Kimaasai</b>	
<b>Kitenzi</b>	<b>Kauli ya kutendesheka</b>
Teiara	_____
Tadalayu	_____
Tejo	_____
Takuenia	_____
Isuma	_____
Terewa	_____
Iremo	_____

Katika mifano iliyopo hapo juu, vitenzi vya Kiswahili vinapata tafsiri ya Kimaasai. Vitenzi hivyo hivyo vya Kiswahili vinaponyambuliwa katika kauli ya kutendesheka na kutendesheana, vinakosa tafsiri ya lugha ya Kimaasai. Vile vile vitenzi vya Kimaasai haviwezikunyambuliwa katika kauli ya kutendama na kauli ya kutendua miongoni mwa kauli zingine.

Hii ni kwa sababu lugha ya Kimaasai si lugha ambishi bali ni lugha tunganishi kama tulivyoelezea hapo awali.Changamoto inazuka wakati wa kutafsiri vitenzi kama hivi vya Kiswahili ambavyo vimenyabuliwa katika kauli tofauti tofauti. Kwa mfano; itakuwa ni vigumu kutafsiri vitenzi vifuatavyo kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kimaasai:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
i) Gandama	_____
ii) Fumbata	_____
iii) Chekesheana	_____
iv) Chezesheka	_____
v) Zibua	_____
vi) Tandua	_____

### **3.3 Kauli ya Uambatanishaji kama Changamoto katika Tafsiri**

Uambatanishaji nimfanyiko ambao leksimu ambatano huundwa kutokana na leksimumbili au zaidi zilizo sahili. Neno linalotokana na muundo huu huitwa neno ambatano. Dhana ya uambatanishaji ni mbinu moja wapo ya kuundia maneno katika lugha ya Kiswahili.Mbinu hii ya uambatanishaji haitumiki katikakuundia maneno katika lugha ya Kimaasai.Katika mbinu hii maneno mawili au zaidi huletwa pamoja na kuunda neno moja ambatano. Maneno yanayotumiwa katika mbinu hii yanaweza kutoka katika kategoria moja ya maneno ama kategoria tofauti kwa mfano;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
i) Nomino na Nomino	_____
Baba - Sukari	_____
Mwana – Hewa	_____
Kiruka – Njia	_____
Kichwa - Ngumu	_____
Mali –Ngumu	_____
ii) Nomino na Kivumishi	_____

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
Sura – Mbaya	_____
iii) Kivumishi na Kivumishi	_____
Cheupe - Chekundu	_____
iv) Kitenzi na Nomino	_____
Piga - Maji	_____

Katika kutumia maneno ya mbinu hii, kuelewa neno upweke upweke haimaanishi kuelewa maana ya neno ambatano. Kwa mfano;

- i) Kichwangumu –haimaanishi kichwa kigumu
- ii) Kirukanjia – haimanishi kuruka njia
- iii) Babasukari – haimaanishi baba wa sukari/ anayehusishwa na sukari

Ni changamoto kutafsiri maneno ambatano kutoka Kiswahili hadi Kimaasai bila kuelewa maana hasa ya neno ambatano. Maneno kama haya yasipoaangaliwa kwa makini, upotevu wa maana hutokea. Kwa mfano, ni changamoto kutafsiri maneno ambatano kama;

- i) Malingumumpendaraha
- ii) Mpendarhamalimoto
- iii) Chaurembocheusi

### **3.4 Viambishi vya Masharti kama Changamoto katika Kutafsiri**

Katika lugha ya Kiswahili viambishi vya masharti hutumika katika kauli ya kuyakinisha na ya kukanusha. Viambishi vinavyotumika ni pamoja na;

-nge-

-ngali-

-ngeli-

Tuangualie mifano katika sentensi;

- i) Hali yakinishi  
-Angeenda dukani angenunua sukari

- Angalinunua gari angalitubeba
- Angelisoma kwa bidii angelifaulu mtihani

ii) Hali kanushi

- Asingeenda dukani asingenunua sukari
- Asingalinunua gari asingalitubeba
- Asingelisoma kwa bidii asingeli faulu mtihani

Ni nadra sana kupata viambishi vya masharti vikitumika katika lugha ya Kimaasai. Itakuwa ni changamoto kutafsiri sentensi tulizoandika hapo juu katika hali yakinishi na hali kanushi kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kimaasai.

### **3.5 Muundo wa Viunganishi kama Changamoto katika Kutafsiri**

Viunganishi ni maneno yanayotumika kuunganisha maneno au mafungu ya maneno na sentensi . Lugha ya Kiswahili hutumia viunganishi vya aina nyingi sana ikilinganishwa na lugha ya Kimaasai. Ingawaje lugha zote mbili hutumia viunganishi, kuna baadhi ya viunganishi ambavyo hutumika katika lugha ya Kiswahili visivyoweza kutumika katika lugha ya Kimaasai. Yaani ni changamoto kutafsiri viunganishi kama hivyo. Tuangalie mifano katika sentensi:

- i) John alitia bidii masomoni kwa minajili ya siku za badaaye.
- ii) Lemayian alitunikiwa zawadi kochokocho, fauka ya hayo alilipiwa tiketi ya kwenda Urusi.
- iii) Juma anasoma ilhali Maria anapika chakula.
- iv) Mama anafagia nyumba huku akiimba.
- v) Anatembea akivalia shati pekee licha ya baridi kali.
- vi) Gari limeegeshwa mkabala wa ofisi za shule isitoshe limeegeshwa karibu na lango kuu.
- vii) Utaadhibiwa ukichelewa kufika mapema almuradi umekwisha onywa.
- viii) Wanakijiji walizingatia usafi kujikinga dhidi ya magonjwa.
- ix) Gorongo akija walau mwambie aniletee.
- x) Watahudhuria harusi wiki ijayo maadamu wataarifiwa mapema.

Kwa sababu ya upungufu wa aina za viunganishi katika lugha ya Kimaasai itakuwa ni changamoto kupata visawe vya viunganishi hivi kama vilivyotumiwa katika sentensi hapo juu;

-kwa minajili ya

-ilhali

-huku

-licha ya

-fauka ya hayo

-isitoshe

-almuradi

-dhidi ya

-walau

-maadamu

### **3.6 Vivumishi vya Pekee na Visisitizi kama Changamoto katika Kutafsiri**

Vivumishi hutumika kama maneno ambayo hutuelezea zaidi kuhusu nomino fulani, ama hutupa sifa za nomino hizo. Kategoria za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa kawaida huwa zimegawika katika vijishehemu vidogo vidogo vingi. Kwa mfano, tunapoangazia vivumishi chini yake kuna aina ya vivumishi kama: vivumishi vya sifa, vivumishi vya idadi, vivumishi viulizi na kadhalika. Katika lugha ya Kimaasai vivumishi huangaliwa kijumla bila kuainisha katika aina mbalimbali. Hali kama hii anapelekea kuwa na changamoto ya kutafsiri baadhi ya aina ya vivumishi ambavyo havitumiki katika lugha ya Kimaasai. Hebu tuangalie mifano:

#### **3.6.1 Vivumishi vya Pekee**

Vivumishi vya pekee ni maumbo ‘enye’ na ‘enyewe’ ambayo katika Kiswahili ndiyo tu huchanganya aina za viambishi vya upatanishi wa kisarufi vinavyojitokeza navyo kimatumizi. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mtu mwenye

(ii) Mti wenye

(iii) Miti yenye

(iv) Mtu mwenyewe

(v) Mti wenyewe

(vi) Miti yenyewe

Itakuwa ni changamoto kutafsiri sentensi zifuatazo kutoka Kiswahili hadi Kimaasai

(i) Mwenyewe amewasili

(ii) Wenyewe wamerudi

(iii) Chenye makali kitafaa

(iv) Vyenyewe ni vibovu

(v) Mwenye kiburi amefukuzwa

### **3.6.2 Vivumishi visisitizi**

Vivumishi visisitizi hutumika katika kusesitiza kuhusu nomino fulani. Hutumika kutilia mkazo, kuonyesha nomino inoyotajwa ndiyo inayozungumziwa na wala si nyingine. Kwa mfano:

(i) Mtu yuyu huyu

(ii) Maji yaya haya

(iii) Kiti kiki hiki

(iv) Watu wawa hawa

(v) Gari lili hili

Msisitizo kama huu haujitokezi katika lugha ya Kimaasai. Urudiaji kama huu haujitokezi katika mazungumzo wala katika maandishi katika lugha ya Kimaasai. Hivyo kutafsiri sentensi kama hizo katika lugha ya Kimaasai itakuwa ni changamoto. Labda tafsiri yenyewe ikifanywa ule msisitizo hautajitokeza katika sentensi za Kimaasai. Sababu mojawapo ya hali hii ni kwamba hizi ni lugha mbili tofauti kitaipolojia.



### 3.7 Changamoto za Kutafsiri zinazotokana na Hali ya Wingi na Kimo

Katika lugha ya kimaasai haswa katika kuzingatia wingi wa nomino zisizohesabika neno ‘sapok’ hutumika kuonyesha au kurejelea wingi. Vile vile katika muktadha mwingine neno hili hili ‘Sapok’ hutumika kurejelea ukubwa. Hebu tuzingatie mifano ifuatayo:

<b>Kimaasai</b>	<b>Kiswahili</b>
i) Enkare sapok -	Maji kubwa
ii) Enkurma sapok -	Unga kubwa
iii) Eshai sapok -	Chai kubwa
iv) Endaa sapok -	Chakula kubwa
v) Esukari sapok -	Sukari kubwa
vi) Enterit sapok -	Mchanga kubwa
vii) Eilata sapok -	Mafuta kubwa

<b>Kimaasai</b>	<b>Kiswahili</b>
i) Enkaji sapok -	Nyumba kubwa
ii) Enkari sapok -	Gari kubwa
iii) Olorika sapok -	Kiti kikubwa
iv) Enkiteng sapok -	Ngo’ mbe mkubwa
v) Olchani sapok -	Mti mkubwa
vi) Oreyiet sapok -	Mto mkubwa
vii) Olchampa sapok -	Shamba kubwa
viii) Elukungu sapok -	Kuku mkubwa

Maana msingi ya neno ‘sapok’ ni kubwa na neno hili ‘sapok’ hutumika kurejelea wingi wa vitu haswa nomino zisizohesabika kama tulivyoona katika mfano wa (a) hapo juu. Tafsiri ya moja kwa moja imeleta upotovu wa maana na kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Ingawaje neno ‘sapok’ linamaanisha kubwa tafsiri sahihi ya mfano wa (a) hapo juu itakuwa kama ifuatavyo:

### **Kimaasai**

### **Kiswahili**

- |                   |               |
|-------------------|---------------|
| i) Enkare sapok   | Maji mengi    |
| ii) Enkurma sapok | Unga mwingi   |
| iii) Eshai sapok  | Chai nyingi   |
| iv) Endaa sapok   | Chakula kingi |
| v) Eilata sapok   | Mafuta mengi  |

Katika mfano wa (b) hapo juu neno ‘sapok’ limetumika kurejelea kimo (ukubwa). Katika kauli hii, maana inachukuana na ile ya Kiswahili pasipo kupoteza maana kama ilivyo katika mfano wa kwanza wa (a). Kauli kama hii isipozingatiwa kwa makini, huweza kutatiza tafsiri. Kama tulivyoona, kauli hii ni changamoto katika kutafsiri kutoka lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili.

### **3.8 Dhana ya Jinsia ya Kike na Kiume kama Changamoto katika Kutafsiri**

Katika lugha ya Kimaasai, katika mazungumzo na maandishi kuna viambishi maalum ambavyo hutumiwa kurejelea jinsia ya kike naya kiume. Viambishi kama hivi havitumiki katika lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Kimaasai viambishi vifuatavyo hutumika kurejelea jinsia ya kike au ya kiume;

‘ene’ – jinsia ya kike

‘Ole’ – jinsia ya kiume

Tuangualie mifano katika sentensi.

- i) Ene Lerionka – inamaanisha anayerejelewa anatoka familia ya Lerionka na ni wa jinsia ya kike  
Ole Lerionka – inamaanisha anayerejelewa anatoka familia ya Lerionka na ni wa jinsia ya kiume. Katika Kiswahili ‘wa’ ingetumiwa kurejelea jinsia zote mbili;  
Wa Lerionka (jinsia ya kike au ya kiume)
- ii) Nena nanu (mimi hapa, jinsia ya kike)  
Lele nanu (mimi hapa, jinsia ya kiume)

‘nena’ inatumika kuonyesha anayejitambulisha kusema (“ndio huyu mimi”) ni wa jinsia ya kike

‘lele’ inatumika kuonyesha anayejitambulisha kusema (“ndio huyu mimi”) ni wa jinsia ya kiume.

iii) Noona yook (ndio hawa sisi, jinsia ya kike)

Noolo yook (ndio hawa sisi, jinsia ya kiume)

‘Noona’ inatumika kuonyesha wanaojitambulisha niwa jinsia ya kike

‘Noolo’ inatumika kuonyesha wanaojitambulisha niwa jinsia ya kiume.

iv) Nenekua (ndio wale, jinsia ya kike)

Lelekua (ndio wale, jinsia ya kiume )

‘Nene’ inatumika kuonyesha wanaoorejelewa ni wa jinsia ya kike

‘Lele’ inatumika kuonyesha wanaoorejelewa ni wa jinsia ya kiume

Katika lugha ya Kimaasai, katika maongezi na maandishi hali ya jinsia inazingatiwa kinyume na lugha ya Kiswahili ambapo jinsia haizingatiwi. Hali kama hii inaweza kusababisha changamoto katika kutafsiri kutoka lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili. Hii ni kwa sababu Kiswahili kinazungumzia watu kwa ujumla pasipokuzingatia aneyezungumziwa ama anayezungumza ni wa jinsia gani.

### **3.9 Usemi wa Taarifa na Usemi Halisi kama Changamoto katika Kutafsiri**

Katika lugha ya Kimaasai, hamna matumizi ya usemi wa taarifa haswa katika maongezi. Kama mtafsiri hataelewa jambo hili, basi patakuwa na upotovu wa maana pale ambapo lugha ya Kiswahili itapokea taarifa ya usemi kutoka lugha ya Kimaasai. Kwa mfano;

#### **Kimaasai**

Usemi halisi

‘Mikindoki aitanyamal kagira aisuma,’ etiaka Juma Maria.

Tafsiri

‘Ninasoma sitaki kusumbuliwa,’ Juma alimwambia Maria.

## **Kimaasasi**

Usemi wa taarifa

Etiaka Juma Maria kagira aisuma mikintoki aitanyamal.

Tafsiri

Juma alimwambia Maria ninasoma sitaki kusumbuliwa.

Katika taafsiri hii ya Kiswahili ya usemi wa taarifa inamaanisha anayetoa taarifa ndiye anayesoma na hataki kusumbuliwa na wala si Juma ambaye anasoma na hataki kusumbuliwa. Usemi wa taarifa katika Kimaasai unamaanisha Juma ndiye anasoma na hataki kusumbuliwa. Tunaona kwamba usemi huu wa taarifa ukitafsiriwa kwa Kiswahili jinsi ulivyo maana inapotea. Katika Kiswahili tafsiri sahihi ya usemi huo wa taarifa inafaa kuwa:

Juma alimwambia Maria kuwa anasoma na hataki kusumbuliwa.

Mtafsiri asipoelewa kwamba katika lugha ya Kimaasai hakuna usemi wa taarifa basi tafsiri yake itakuwa na upovu wa maana kila wakati atakapokuwa akitafsiri taarifa.

Hii hali ya usemi wa taarifa ni changamoto kwa anayetafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili.

### **3.10 Vielezi (Viulizi) kama Changamoto katika Kutafsiri**

Vielezi ni maneno ambayo hueleza zaidi juu ya kitenzi aghalabu vitenzi vya matendo au vielezi vingine au kivumishi. Vielezi viulizi huuliza juu ya tendo. Namna tendo lilivyo fanywa (vipi), wakati tendo lilipofanywa (lini), mahali tendo lilipofanyiwa (wapi), mtendaji wa tendo (nani) na Kitendwa/kitendewa cha tendo lililotendwa (nani/nini).

Katika lugha ya Kimaasai vielezi, haswa vielezi viulizi, huweza kutokea kabla ya vitenzi kwenye sentensi. Mpangilio huu huenda kinyume na mpangilio wa lugha ya Kiswahili. Jambo hili linaweza kusababisha changamoto katika shughuli ya kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili na Kiswahili hadi Kimaasai. Tuangalie mifano:

- i) Kajiko teneiteng'enisho ormualimui?
- ii) Kaji ewaki oltamoyiai?
- iii) Kanu eshukunye Nyambura?
- iv) Kajiko teneyierr Roza endaa?

Hebu tuangalie tafsiri ya Kiswahili kwa kufuata mpangilio wa maneno kama ulivyo katika lugha ya Kimaasai hapo juu:

- i) Vipi anafundisha mwalimu?
- ii) Wapi amepelekwa mgonjwa?
- iii) Lini alirudi Nyambura?
- iv) Vipi anapika Roza chakula?

Mpangilio huu wa maneno katika tafsiri ya Kiswahili unaweza kusababisha upotovu wa maana. Hali hii inasababishwa na jinsi vielezi katika lugha ya Kimaasai vinavyojitokeza katika sentensi. Hali hii inasababisha changamoto ya kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili.

### **3.11 Mpangilio wa Kiima na Kiarifu katika Sentensi kama Changamoto katika Kutafsiri.**

Kiima ni sehemu ya kwanza ya sentensi ambayo huelezwa na kiarifu. Sehemu ya kiima hukaliwa na nomino ama kiwakilishi chake. Kiarifu ni sehemu ya sentensi ambayo inatoa taarifa kuhusu kiima. Hapa ndipo kitenzi kikuu huwa. Katika sentensi za lugha ya Kimaasai, kiarifu hujitokeza kabla ya kiima. Mpangilio katika lugha ya Kiswahili ni kinyume cha kauli ya Kimaasai. Tuangalie mifano ifuatayo ya Kimaasai:

- i) Eyierita Juma endaa
- ii) Eloito Maria sokoni
- iii) Eiremo Mutinda olchamba
- iv) Eishirita enkerai

Tafsiri ya Kiswahili kama ilivyo hapo juu katika lugha ya Kimaasai ni ifuatavyo:

- i) Anapika Juma chakula
- ii) Anaenda Maria sokoni
- iii) Analima Mutinda shamba
- iv) Analia mtoto

Kulingana na tafsiri hii ya Kiswahili, katika lugha ya Kimaasai sehemu ya kiarifu inajitokeza kabla ya kiima. Katika lugha ya Kiswahili, kiima huja kabla kiarifu.

Hali kama hii ya mpangilio wa kiima na kiarifu katika sentensi inazua changamoto katika kutafsiri kutoka lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili. Hali hii pia inaenda kinyume na mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili, hali ambayo inaathiri maana katika Kiswahili pia.

### **3.12 Dhana ya ‘Kuzima’ kama Changamoto katika Kutafsiri.**

Katika lugha ya Kimaasai, dhana ya kuzima inatumika katika kuelezea hali ya kuzima moto, taa, stima na tochi. Neno ambalo hutumika katika kurejelea hali ya kuzima ni neno la Kimaasai ‘taara’ maana ya kimsingi ya neno ‘taara’ ikiwa ni ua / toa uhai. Tuangalie matumizi yake katika lugha ya Kimaasai:

- i) Taara oltaa – ua taa (zima taa)
- ii) Taara enkima – ua moto (zima moto)
- iii) Taara ositima – ua stima (zima stima)
- iv) Taara oltosh – ua tochi (zima tochi)

Tafsiri ya moja kwa moja kutoka Kimaasai hadi Kiswahili inakuwa kama hapo juu yaani:Ua taa, ua moto, ua stima, ua tochi. Katika usahihi kwa Kiswahili inastahili kuwa: zima taa, zima moto, zima stima, zima tochi. Dhana kama hii basi inazua changamoto katika kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili. Katika mwelekeo wa Kiswahili, viumbe wenye uhai ndio wanaoweza kuuwawa, na sio vitu kama taa,moto,stima na tochi.Ukinzani huu katika matumizi ya dhana ya ‘kuzima’kati ya lugha ya Kimaasai na Kiswahili ndio inazua changamoto ya kutafsiri.

### **3.13 HITIMISHO**

Katika sura hii ya tatu tumeangalia changamoto zinazoibuka katika kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Tumeangalia changamoto hizo wakati ambapo tafsiri inapotekelezwa kutoka Kimaasai (lugha ambayo tumeteua kuwakilisha lugha zingine katika muktadha wa wingilugha) hadi Kiswahili na vile vile kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kimaasai kwa misigi ya tofauti za miundo ya lugha. Tumeangalia jinsi tofauti za miundo ya lugha inavyoweza kusababisha changamoto katika mchakato wa kutafsiri. Tumeonyesha tofauti kati ya miundo ya lugha ya Kiswahili na Kimaasai. Tumezingatia tofauti za kisarufi ambapo tumeona tofauti katika mpangilio wa maneno kwenye sentensi, dhana ya utambulishi wa kijinsia na kwakupitia mifano tumeona dhana ambazo zipo kwenye lugha moja na hazipo kwenye lugha nyingine. Tumeona jinsi hali hizi zote zinavyosababisha changamoto katika kutafsiri.

Hatimaye katika sehemu hii ya tofauti za miundo ya lugha, tumezingatia tofauti za kileksika. Tumeona jinsi lugha hizi zinavyotofautiana kimaana kulingana na dhana tofauti tofauti. Kwa kupitia mifano tumeona jinsi dhana ya kileksika inavyosababisha changamotokatika kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili na kutoka Kiswahili hadi Kimaasai.

## SURA YA NNE

### MANUFAA YA KUTAFSIRI KATIKA SEKTA ZA ELIMU,AFYA NA DINI

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia manufaa yanayotokana na kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha. Kupitia tafsiri, tutaangalia jinsi sekta mbalimbali zinavyonufaika. Baadhi ya sekta ambazo tumeangazia ni pamoja na; sekta ya elimu, sekta ya matibabu na sekta ya dini. Sekta hizi ni muhimu sana katika maeneo yetu ya utafiti. Sekta hizi huleta watu ambao wanatoka katika jamii tofauti tofauti pamoja. Kwa sababu hii, panazuka shida ya mawasiliano na shughuli mbalimbali hutatizika. Tuliangulia kwa kusema kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo lughainayowaleta watu pamoja kimawasiliano. Hata hivyo tuliona kwamba katika maeneo yetu ya utafiti si watu wote walio na uwezo wa kuwasiliana kupitia lugha ya Kiswahili kikamilifu haswa watu kutoka jamii ya Wamaasai ambao ndio wenyeji. Ili watu waweze kutekeleza shughuli zao katika sekta ambazo tumetaja hapo juu, lazima pawe na mawasiliano. Nikupitia tafsiri ambapo mawasiliano haya yanaweza kufanikishwa – kutafsiri kutoka lugha za kwanza (Kimaasai) hadi Kiswahili na vile vile kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza. Licha ya kwamba taaluma ya tafsiri imekumbwa na changamoto na vikwazo kama tulivyoona katika sura ya pili na ya tatu, taaluma ya tafsiri imeweza kufanikiwa kuimarisha mawasiliano katika maeneo yetu ya utafiti. Tumeteua sekta muhimu ili kuthibitisha manufaa ya kutafsiri katika muktadha wa wingilugha. Hebu tuangalie jinsi sekta hizi zilivyonufaika kupitia tafsiri.

#### 4.2 Manufaa ya Kutafsiri katika Sekta ya Elimu

Katika maeneo yetu ya utafiti, kuna vitengo mbalimbali katika sekta ya elimu. Vitengo hivi vinahusisha taasisi zifuatazo:

- i) Shule za chekechea
- ii) Shule za msingi
- iii) Shule za upili
- iv) Vyuo na vyuo vikuu

Kupitia tafsiri mawasiliano yameimarishwa na sekta ya elimu kunufaika kwa njia moja ama nyingine kama ifuatavyo:



#### **4.2.1 Kujifunza Kiswahili katika Kiwango cha Chekechea na Madarasa ya Chini ya Shule za Msingi**

Katika shule za chekechea na madarasa ya chini ya shule za msingi lugha ya mawasiliano ni lugha inayozingira maeneo ya taasisi kama hizi. Katika maeneo mengi ya shule hizi, lugha ya Kimaasai hutumika kama lugha ya mawasiliano. Wanafunzi wengi wanaotoka maeneo haya huzungumza Kimaasai pekee. Inabidi wanafunzi hawa wajifunze Kiswahili kwa sababu ni somo la lazima katika shule za msingi na shule za upili. Vile vile lugha ya Kiswahili itawasaidia kuwasiliana na jamii zingine. Walimu wanaofunza katika shule hizi, wengi wao, wanatoka katika jamii ya Wamaasai na bila shaka wanafahamu Kiswahili. Wanapofunza wanatumia tafsiri kuelezea dhana tofauti tofauti za Kimaasai kwa Kiswahili. Kwa mfano; Kupitia kwa tafsiri ya neno kwa neno, ambapo tunapotafsiri maneno kwa mbinu hii, tunafanya tafsiri ya maneno ya lugha chanzi kwa kuzingatia maana za msingi za maneno katika lugha chanzi na kutafuta maneno hayo katika lugha lengwa. Kwa mfano:

##### **i)Tarakimu**

<b>Kimaasai</b>	<b>Kiswahili</b>
Nabo	Moja
Are	Mbili
Uni	Tatu
Ong'wan	Nne
Imiet	Tano
Ile	Sita
Naapishana	Saba
Isiet	Nane
Nauo	Tisa
Tomon	Kumi

## **ii)Majina ya wanyama**

### **Kimaasai**

Enkiteng'  
Enkine  
Enker  
Osikiria  
Oldie  
Orng'atuny  
Olowuaru Keri  
Olcharkuk  
Orng'ojine  
Olarro

### **Kiswahili**

Ng'ombe  
Mbuji  
Kondoo  
Punda  
Mbwa  
Simba  
Chui  
Twiga  
Fisi  
Nyati

## **iii)Sehemu za mwili**

### **Kimaasai**

Nkonyek  
Enkume  
Enkutuk  
Ilala  
Elukunya  
Enkeju  
Enkiok  
Irkimojik  
Irpapit  
Orgoo

### **Kiswahili**

Macho  
Pua  
Mdomo  
Meno  
Kichwa  
Mguu  
Masikio  
Vidole  
Nywele  
Kifua

## **iv)Rangi tofauti tofauti**

### **Kimaasai**

Olorok  
Olonyori  
Olodo

### **Kiswahili**

Nyeusi  
Kijani  
Nyekundu

Osikitoi  
Orpus  
Ormugie  
Ngiro

Manjano  
Samawati  
Huthurungi  
Kijivu

**v) Aina za wadudu**

**Kimaasai**

Orkedi Kedi  
Osamburimburi  
Ilorok  
Irkitende  
Orngencheri  
Ormasheri  
Emuyioo  
Nkalaok  
Orpidilai  
Elashei

**Kiswahili**

Buibui  
Kipepeo  
Nyuki  
Kumbikumbi  
Mende  
Kupe  
Siafu  
Sisimizi  
Kiroboto  
Chawa

**vi) Kuashiria**

**Kimaasai**

Ene  
Ende  
Shumata  
Abori  
Dukuya  
Siadi  
Kedienye  
Tatene  
Tidialo  
Enelakwa

**Kiswahili**

Hapa  
Pale  
Juu  
Chini  
Mbele  
Nyuma  
Kushoto  
Kulia  
Kando  
Mbali

### **vii)Hali tofauti tofauti**

#### **Kimaasai**

Emoyian

Enchipai

Aisinanu

Asioki

Akiti

Airut

Aure

Aing'asia

#### **Kiswahili**

Ugonjwa

Furaha

Huzuni

Haraka

Polepole

Kushtuka

Kuogopa

Kushangaa

### **viii)Aina ya vinywaji**

#### **Kimaasai**

Enkare

Kule

Imotorik

Kule Naoto

Shai

Enaisho

Oloshoro

#### **Kiswahili**

Maji

Maziwa

Supu

Maziwa ya mgando

Chai

Pombe

Uji

Kama tulivyoona, kutafsiri kutoka Kimaasai hadi Kiswahili kunaleta manufaa katika sekta ya elimu. Wanafunzi wa shule za chekechea na wanafunzi wa madarasa ya chini ya shule za msingi, wanaweza kujifunza lugha ya Kiswahili. Jambo hili linawawezesha kujiandaa na kuweka msingi bora ili kufanya vyema katika somo la Kiswahili katika madarasa ya juu ya shule ya msingi na vile vile kuweza kuwasiliana kwa Kiswahili na jamii zingine.

Hata hivyo ingawaje kuna manufaa katika sekta ya elimu kutokana na kutafsiri kuna viziwi ambavyo vinashuhudiwa. Kwa mfano, si maneno yote ya lugha ya Kimaasai yanapata visawe katika lugha ya Kiswahili wakati wa kufunza.

Pia inachukua muda mrefu kwa wanafunzi kujifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Hii ni kwa sababu wanafunzi hawa wanatumia lugha ya Kimaasai katika shughuli zingine zote manyumbani na kwingineko. Fursa ya pekee ya kutumia lugha ya Kiswahili ni wakati ambapo wanafunzi hawa wako shuleni.

#### **4.2.2 Kuimarisha Elimu ya Watu Wazima**

Kuna baadhi ya watu ambao hawakufanikiwa kupata elimu kwa wakati uliofaa. Wengine walikatiza masomo yao katika shule za msingi haswa katika madarasa ya chini. Baadaye watu kama hawa hujiunga na masomo ya watu wazima wakiwa na umri mpevu. Wanafunzi wanaojiunga na shule za watu wazima, idadi yao kubwa katika maeneo yetu ya utafiti, huzungumza lugha ya Kimaasai. Kwa sababu wanafunzi hawa hufunzwa Kiswahili ambacho wengi wao hawakielewi, tafsiri hutumika na dhana za Kiswahili hufafanuliwa kwa lugha ya Kimaasai. Vile vile dhana za Kimaasai hutolewa mifano ya Kiswahili.

Ili kuwawezesha wanafunzi hawa kusoma, irabu/vokali za Kiswahili hutumika na ambazo ni;

a, e, i, o, u

Maneno mafupi ya Kiswahili hubuniwa kutokana na irabu hizi. Maneno yanayobuniwa hutafutiwa visawe vyake katika lugha ya Kimaasai kupitia tafsiri. Kwa mfano:

ua (toa uhai) – aar

ua (mmea) – emauai

au – ashu

oa – ayam

Vile vile silabi za Kiswahili hutumiwa ili kujifunzia kusoma kama maendelezo ya irabu, silabi mbalimbali hupatikana. Kutokana na silabi maneno ya Kiswahili hubuniwa na kisha kuambatanishwa na visawe vyake katika lugha ya Kimaasai. Hebu tuone mifano:

ma    me    mi    mo    mu

ba    be    bi    bo    bu

ka    ke    ki    ko    ku

<b>Kiswahili</b>		<b>Kimaasai</b>
Mama	-	Yieyioo
Mimi	-	Nanu
Baba	-	Mpapa
Babu	-	Kakuyiaa
Bibi	-	Enkitok
Kaka	-	Olalashé
Kuku	-	Elukunku
Beba	-	Anap
Bubu	-	Orbubu
Kiboko (Mnyama)	-	Ormakau
Miba	-	Orkikwei
Kiboko (Fimbo)	-	Eng'udi

Kupitia irabu na silabi za Kiswahili, maneno mafupi mafupi ya Kimaasai huundwa pia. Maneno ya Kimaasai yaliyoundwa, kwa kupitia tafsiri ya moja kwa moja huambatanishwa na visawe vyake katika lugha ya Kiswahili.

Tuangelie mifano:

<b>Kimaasai</b>	<b>Kiswahili</b>
Yieyioo	Mama
Enkanashe	Dada
Enkima	Moto
Olorika	Kiti
Enkare	Maji
Endaa	Chakula
Enkurma	Unga
Taisere	Kesho
Tinakata	Sasa
Enkai	Mungu

Kwa kupitia tafsiri wanafunzi hawa wa shule za watu wazima,hujifunza kusoma kwa kulinganisha maneno ya Kiswahili na Kimaasai.

Baada ya kuimarika katika maneno ya Kiswahili na visawe vyake katika lugha ya Kimaasai, wanafunzi hawa hutunga sentensi fupi fupi sahili za Kiswahili au za Kimaasai na kuziandikia tafsiri yake kama ifaavyo kutegemea lugha walioandikia kwanza.

Kwa mfano:

- i) Mtoto analia
- ii) Mama anapika
- iii) Nataka maji
- iv) Njoo hapa
- v) Twende nyumbani
- vi) Kula chakula
- vii)Funga mlango

Tafsiri ya Kimaasai

- i) Ishirita enkerai
- ii) Egira yieyioo ayierisho
- iii) Agira ayau enkare
- iv) Wou ene
- v) Maape ang'
- vi) Inosa endaa
- vii)Inkeno emilango

Baada ya muda, wanafunzi hawa wa shule za watu wazima, hatua kwa hatua wanajiimarisha kimasomo kwa sababu, ingawaje kwa kiwango cha chini, wanaweza kujielezea kimaandishi na kiusemi katika lugha ya Kiswahili. Tafsiri inaimarisha elimu yao na wanaweza kuwasiliana na jamii isiyozungumza lugha ya Kimaasai. Kundi kama hili limekuwa la manufaa katika jamii kwasababu limeweza kulegeza au kupunguza kwa kiwango kikubwa vikwazo vya mawasiliano baina ya jamii ya Wamaasai wasiolewa Kiswahili na jamii zingine zisizoelewa lugha ya Kimaasai. Baada ya kupata msingi dhabiti ya kielimu baadhi ya wanafunzi wa shule hizi za watu wazima huendeleza elimu yao na hata kufanya mtihani wa kitaifa wa shule za msingi.

Kuna wale wanaofanikiwa na kujiunga na shule za upili na kuendeleza elimu yao hata zaidi. Tafsiri imechukuwa nafasi bora katika kuimarisha maendeleo haya ya elimu ya watu wazima. Licha ya ufanisi unaopatikana katika shule hizi za watu wazima, kuna matatizo ambayo yanaibuka. Wengi wa wanafunzi wa shule hizi huwa ni wa umri wa juu. Inakuwa ni vigumu kwao kujifunza lugha ng'eni kwa sababu uwelewa na tajiriba zao za miaka mingi zimefungamana na lugha zao za kwanza. Kuanzisha dhana mpya za Kiswahili wakati kama huu, inakuwa ni vigumu kueleweka kwa dhana kama hizo. Hali hii hutatiza tafsiri kwa sababu dhana mpya zinapotafsiriwa, hazileti maana kwa wanafunzi hawa kwa sababu hazieleweki.

#### **4.2.3 Lugha za Kwanza (Kimaasai) Kujikuza Kimsamiati**

Lugha ya Kiswahili imekomaa zaidi ikilinganishwa na lugha za kienyeji au lugha za kwanza. Hii ni kwasababu kando na lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya, Kiswahili ni lugha ya kimataifa. Lugha ya Kiswahili imekomaa na kuendelea kitaaluma na katika nyanja za kiteknolojia na sayansi. Vitabu vingi vimeandikiwa Kiswahili. Mambo haya yote yamepelekea Kiswahili kuwa na msamiati mpana sana tukilinganisha na lugha za kwanza ikiwemo lugha ya Kimaasai. Kuna maneno mengi au msamiati mwingi wa lugha ya Kiswahili ambao maana yake imehawilishwa hadi lugha za kwanza. Maneno au msamiati husika hutumika katika lugha hizi za kwanza na maana husalia kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano lugha ya Kimaasai imeweza kujikuza kimsamiati kutokana na msamiati wa Kiswahili.

Hebu tuangalie mifano:

i) Vyakula na vitu vinavyohusika na vyakula

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
Chumvi	Shumpi
Sukari	Esukari
Mboga	Mpuka
Kitunguu	Kitunguu
Nyanya	Irnnyanya
Mchele	Ormushele
Ugali	Orgali
Binzari	Bisali
Mandazi	Ormandasi



Mkate  
Machungwa

Emukate  
Ormashunkwai

ii) Vifaa vinavyotumika kwa njia mbalimbali

**Kimaasai**

Panga  
Kiberiti  
Simu  
Meza  
Kalamu  
Mshipi  
Kufuli  
Kioo  
Ufunguo  
Kabati  
Karatasi

**Kiswahili**

Orpanga  
Enkibiriti  
Esimu  
Emisa  
Enkalamu  
Emishipi  
Enkifuli  
Kiok  
Orfunguo  
Kabat  
Enkardasi

iii) Vyombo vinavyotumika nyumbani

**Kiswahili**

Kijiko  
Kikombe  
Sahani  
Kichungi  
Bakuli  
Karai  
Chupa  
Chungu

**Kimaasai**

Enkijiko  
Enkikombe  
Esaani  
Enkishushungi  
Embakuli  
Orkarai  
Oltupa  
Enyonko

Kwa kupitia tafsiri maneno / msamiati wa Kiswahili na maana yake, kama tulivyoona kwenye mifano imehamishwa hadi lugha ya Kimaasai. Msamiati huu hutumika katika lugha ya Kimaasai.

Tafsiri imeleta manufaa kwa sababu msamiati huu hutumika katika kuelimisha wanajamii katika nyanja mbalimbali haswa mashuleni na vyuoni. Hata hivyo changamoto inayojitokeza hapa ni kwamba Kiswahili pia kimekopa sana kutoka lugha zingine. Baadhi ya maneno yaliyokopwa huwa hayatumiki katika mazingira rasmi. Maneno kama haya yanapohamishwa hadi lugha nyingine yanaweza kusababisha upotovu wa maana.

#### **4.2.4 Kufanikisha Mawasiliano Baina ya Shule na Washikadau Wengine**

Hakuna shirika au taasisi yoyote ile inayoweza kufanikiwa upweke upweke pasipo kushirikiana na washikadau wengine katika jamii. Shule na hata vyo haviepuki swala hili. Kuna washikadau wengine kando na walimu na wanafunzi ambao mchango wao ni walazima kwa minajili ya kusaidia katika kufanikisha na kuendeleza shughuli za shule. Washikadau hawa kwa mfano, wanajumuisha bodi za shule katika shule za upili, wanakamati wa shule katika shule za upili na za msingi, wazazi, wawakilishi wa kidini wanao fadhili shule, viongozi kama machifu na wazee wa kijiji.

Ili kufanikisha maendeleo na shughuli za shule, washikadau hawa hujumuishwa katika vikao, mikutano, mijadala na mazungumzo ambayo aghalabu huandaliwa shuleni. Katika baadhi ya maeneo yetu ya utafiti, kuna shule ambazo washikadau wahusika si wasomi hivyo wanazungumza lugha ya Kimaasai pekee – wanaweza kuwa ni wazazi, wanachama wa kamati za shule ama wazee wa kijiji. Vilevile baadhi ya wasimamizi wa shule na walimu si wenyeji wa Umaasaini na hivyo hawaelewi lugha ya Kimaasai. Wakati vikao vinapoandaliwa baina ya shule na washikadau kama hawa, kwa kawaida mawasiliano hutatizwa kwa sababu makundi haya mawili hayawezi kuwasiliana moja kwa moja. Majadiliano katika vikao hivi ni muhimu na hayawezi kuepukwa.

Nyakati kama hizi tafsiri husaidia kutatua matatizo kama haya ya mawasiliano. Kwa kupitia misingi ya tafsiri, mkalimani hutumiwa, dhana, maelezo au maandishi hufafanuliwa katika lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili na vile vile kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kimaasai.

Mbinu hii pia hutumika katika siku muhimu katika kalenda ya shule. Kwa mfano, mikutano ya wazazi wa shule na walimu, mikutano ya maombi ya watahiniwa wa mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne, mikutano ya sherehe za kufunga shule na mikutano ya uhamasishaji kuhusu umuhimu wa elimu haswa kwa wasichana, miongoni mwa mikutano mingine.

Mikutano kama hii ni muhimu sana katika kuimarisha elimu shuleni na hata vyuoni. Tafsiri imeweza kufanikisha mawasiliano katika mikutano ambayo tumeelezea hapo juu na matokeo yake yamekuwa ni ya manufaa katika sekta ya elimu. Hata hivyo mawasiliano yameweza kutatizika kwa sababu mbali mbali. Kwa mfano, mawasiliano mengi yanayolenga taasisi za kielimu huwa ni kwa kupitia maandishi na huandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Inakuwa ni vigumu kwa mawasiliano kama haya kueleweka yanapoelezewa hadi lugha ya Kimaasai haswa kwa washikadau ambao si wasomi.

### **4.3 Manufaa ya Tafsiri katika Sekta ya Matibabu/ Afya**

Katika maeneo yetu ya utafiti kuna vituo vingi vya afya, ambavyo vingi ni vya umma ama vya serikali. Vile vile kuna vituo vya kibinafsi. Miongoni mwa vituo hivi vya afya hospitali kuu ya kaunti ya Narok level 5 ndio hospitali kubwa zaidi na ambayo watu hutumwa kuhudumiwa wakishindikana katika hospitali zingine katika kaunti ya Narok. Wahudumu wa hospitali hizi hutoka katika jamii tofauti tofauti. Wanaohudhuria hospitali hizi ili kupata huduma mbalimbali pia hutoka katika jamii tofauti tofauti za nchini Kenya. Kufuatia hali hii, wakati mwingine kunazuka matatizo ya mawasiliano baina ya wahudumu wa afya na wagonjwa. Kwa mfano, mgonjwa asiyelewa Kiswahili na anaelewa Kimaasai hawezi kuelewana na mhudumu wa afya. Tafsiri imeweza kuimarisha mawasiliano na kuleta manufaa katika sekta hii ya matibabu. Tuzingatie mifano ifuatayo:

#### **4.3.1 Maelekezo kwa Wanaotembelea Vituo vya Matibabu / Afya.**

Katika lango la kuelekea kwenye vyumba vya wagonjwa waliolazwa katika hospitali kuu ya Narok level 5 , masaa ya kuwatembelea wagonjwa yameandikwa kwa Kiswahili na kutafsiriwa kwa Kimaasai kama ifuatavyo:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
MASAA YA KUTEMBELEA WAGONJWA: ASUBUHI: SAA KUMI NA MBILI NA NUSU HADI SAA MOJA NA NUSU (6:30 – 7:30) MCHANA: SAA SITA NA NUSU HADI	ISAAI NAADWAREKI ILTAMOYIA TADEKENYA: SAA TOMON O ARE ONUSU OMETABAIKI SAA NABO ONUSU (6:30- 7:30) DAMA: SAA SITA ONUSU OMETABAIKI

SAA NANE (12:30 – 2:00) JIONI: SAA KUMI NA NUSU HADI SAA MBILI (4:30 – 8:00) WAGENI HAWARUHUSIWI KWENYE WODI WAKATI MWINGINE	SAA ISIET (12;30 – 2:00) TEIPA: SAA TOMON O NUSU OMETABAIKI SAA ARE (4:30 – 8:00) MENYORRARRI ILOMON TE WODI TOO NKULIE SAAI
--	--

Wanaohudhuria kliniki wanaelezwa kwa kuandikiwa siku na wakati, zaidi ya haya wanakumbushwa kubeba kadi ya kliniki. Kadi hizi zimeandikwa kwa Kiswahili na tafsiri yake ya Kimaasai:

**BEBA HII KADI KILA WAKATI UNAPOTEMBELEA KLINIKI**

Tafsiri ya Kimaasai:

**TANAPA ENA KADI ISAAI POOKIN NILO KLINIK**

Tafsiri inaimarisha na kurahisisha mawasiliano kwa wote wanaotembelea wagonjwa na pia wote wanaotafuta huduma za matibabu. Hali hii inasaidia kukabili utata au usumbufu wa kimawasiliano unaoweza kuzuka.

#### **4.3.2 Tahadhari Dhidi ya Magonjwa Hatari**

Katika kuta za hospitali haswa hospitali kuu ya Narok – level 5, kuna maandishi yalioandikwa kupitisha ujumbe unaolenga wote kuwaonya dhidi ya magonjwa hatari. Kuta hizi zimeandikwa kwa lugha ya Kimaasai na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<u>TAHADHARI DHIDI YA UKIMWI:</u> KUMBUKA UGONJWA WA UKIMWI HAUNA TIBA UKIMWI NI UGONJWA WA KUAMBUKIZA KWA KUPITIA VIRUSI	<u>TERETANAYU TIALO BIITIA</u> TADAMU AJO MEETA EMOYIAN EBIITIA EMBAATA ORE BIITIA NAA EMOYIAN NAITASUROI EIMU ENKEEYA <u>ORE ENKEEYA E BIITIA NEITASUROI</u>

VIRUSI VYA UKIMWI HUAMBUKIZWA

KWA NJIA ZIFUATAZO:

1. KUFANYA MAPENZI NA MTU ALIYEAMBUKIZWA VIRUSI VYA UKIMWI
2. KUTUMIA KIFAA KAMA SINDANO ILIYOTUMIWA NA MTU ALIYEAMBUKIZWA VIRUSI VYA UKIMWI
3. KUONGEZEWA DAMU ILIYO NA VIRUSI VYA UKIMWI
4. KUPITISHWA KUTOKA KWA MAMA HADI MTOTO WAKATI WA KUZALIWA

JKINGE DHIDI YA UKIMWI

1. KUWA MWAMINIFU KWA MPENZI WAKO
2. JIZUIE KUFANYA MAPENZI OVYO
3. KAMA HUWEZI KUJIZUIA TUMIA MPIRA WA KONDOM KILA WAKATI UNAPOFANYA MAPENZI
4. USITUMIE KIFAA KAMA SINDANO ILIYOTUMIWA NA MTU MWINGINE
5. AKINA MAMA WAJAWAZITO WANASHAURIWA KUJIFUNGULIA HOSPITALINI

TOO NKOITOI NAAPASHA:

1. AIRURA OLTUN'ANI LOOTA EMOYIAN E BIITIA
2. AITUMIA INTOKITING NAIJO OSINDANO NAITUMIA OLTUNG'ANI LOOTA EMOYIAN E BIITIA
3. AAPONIKI OSARGE LOLTUNG'ANI LOOTA BIITIA
4. ASHURTAKI NG'OTONYE ENKERAI EGIRA AIU

TORRIPO KEON TIALO BIITIA

1. TAA ESIPANI TOLONORR LINO
2. MIAS ELOLOITO ISAAI POOKIN
3. TENIMIDIM AIBOOI KEON, INTUMIA IMPIRAI E KODOM ENKATA POOKI NILOLOITO
4. MINTUMIA INTOKITING NAIJO OSINDANO NAITUMIA OLIKAE TUNG'ANI
5. ORE INTUAN, NEITANAPAKI PEE EISHO TE SIPITALI

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p style="text-align: center;"><b>MALARIA NI HATARI!</b></p> <p>KILA MWAKA MAMILIONI YA WATU HUFA ULIOMWENGUNI KUTOKANA NA MALARIA</p> <p><u><b>JIEPUSHE NA MALARIA:</b></u></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1. LALA CHINI YA NETI ILİYOTIBIWA</li> <li>2. HAKIKISHA MAZINGIRA YAKO HAYARUHUSU MBU KUZAANA</li> <li>3. MEZA TEMBE ZA KUZUUIA MALARIA KILA MARA UNAPOSAFIRI MAENEO YANAYOKUMBWA NA HATARI YA MALARIA</li> </ol>	<p style="text-align: center;"><b>EKEYAISHO MALARIA!</b></p> <p>EYE IMLIONINI OLTUNG'ANA TE NKOP TENKARAKI MALARIA</p> <p><u><b>TAPAASHARE MALARIA:</b></u></p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1. IRRAGA TIATUA ENETI NATABAAKI</li> <li>2. TONYUAA MINCHO ENKOJONG'ANI EISHO TE MANYISHO INO</li> <li>3. TOOKO IRKEEK LOIBOOYO MALARIA ENKATA POOKIN NILO ENKOP NATII MALARIA</li> </ol>

Maelezo kuhusu chanjo za watoto:

Maelezo kwa Kiswahili

**JE MTOTO WAKO AMEPOKEA CHANJO ZOTE?**

**TEMBELEA KLINIKI YAWATOTO LEO**

Maelezo kwa kimaasai:

**AMAA, KENOTO ENKERAI INO ISINDANONI POOKIN?**

**SHOMO KLINIK ONKERATAATA**

Tafsiri kama hii kutoka lugha ya kwanza hadi Kiswahili ama kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza ni muhimu sana kimawasiliano. Watu wote hunufaika kwa kupokea ujumbe kwa lugha wanazozielewa.

Sekta ya matibabu imenufaika kwa kufikia malengo yake ya kuhakikisha afya imedumishwa katika jamii na hata katika nchi nzima kwa jumla, afya njema itawawezesha wananchi kuendelezana kuimarisha sekta zingine. Licha ya kwamba mawasiliano yamepitishwa kutoka lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili na kutoka Kiswahili hadi Kimaasai, kuna matatizo kadhaa. Makosa hudhihirika katika tafsiri kama hizi kwa sababu wanaotafsiri mara nyingi huwa hawana ujuzi wa taaluma ya tafsiri. Pia maneno mengine ambayo yamejikita katika sajili ya kimatibabu, hayana visawe vyake katika lugha ya Kimaasai. Kwa mfano, maneno kama kipindupindu, malaria na ukimwi. Hali kama hizi hutatiza mawasiliano kupitia tafsiri.

#### **4.3.3 Kampeni ya Nyumba hadi Nyumba Dhidi ya Magonjwa ya Watoto.**

Kuna kampeni ambazozinaendelezwa na wizara ya afya kote nchini. Kampeni hizi hufanywa baada ya kipindi fulani baada ya utafiti kuhusiana na magonjwa ya watoto kufanywa. Kampeni hizi huteklezwa na wahudumu wa afya ambao lengo lao huwa ni kuwapa watoto wa umri fulani chanjo dhidi ya magonjwa ya watoto kama; polio, pepopunda, ukambi, rubela miongoni mwa magonjwa mengine ya watoto. Kampeni hizi haswa hulenga kuwafikia wanajamii wanaoishi mashambani mbali na vituo vya afya na pia watu wengine wasiotilia maanani ama wasiojua umuhimu wa chanjo za watoto.

Wakati wa kufanywa kwa kampeni kama hizi, mara kwa mara hali ya mawasiliano hutatizwa. Matatizo hutokea pale ambapo wahudumu wa afya hushindwa kuwasiliana na wenyeji kwa sababu za tofauti za lugha wanazozungumza. Kuna wenyeji wengi wa kutoka jamii ya Kimaasai ambao hawaelewi lugha ya Kiswahili ambayo ndio lugha ya mawasiliano miongoni mwa jamii zinazozungumza lugha tofauti. Tafsiri huwa ni ya manufaa sana hali kama hizi zinapoibuka. Wahudumu hawa wa afya huandamana na watu ambao huwa ni wenyeji wanaofahamu lugha za Kiswahili na Kimaasai. Wasaidizi hawa husaidia kufafanua maelezo kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kimaasai na vile vile kutoka lugha ya Kimaasai hadi Kiswahili. Tafsiri inafanikisha mawasiliano, kampeni dhidi ya magonjwa ya watoto inafanikiwa, wanajamii wanahamasishwa kuhusu umuhimu wa chanjo za watoto na hatimaye wanahiari kutembelea kliniki za watoto na kufuata ratiba ya chanjo za watoto. Hali hii imesaidia kukabiliana na vifo vya watoto katika jamii ya Kimaasai na nchi kwa jumla. Sekta ya afya na wizara ya afya, kwa jumla, zimenufaika kupitia tafsiri kuyafikia malengo ya kuimarisha na kulinda afya ya watoto. Hata hivyo, licha ya ufanisi huu kupatikana bado kuna changamoto.

Msamiati mwingi unaotumika kimaandishi na kimazungumzo huwa umejikita katika sajili ya kimatibabu. Inakuwa ni vigumu kwa wanajamii haswa wale hawajasoma kuelewa dhana zinazohusishwa na msamiati kama huu kupitia tafsiri.

#### **4.3.4 Kuimarisha Huduma za Kliniki za Wanawake Wajawazito na Waliojifungua**

Wanawake wajawazito na waliojifungua wana ratiba za kliniki ambazo huwaelekeza kuhusiana na tarehe na wakati wa kuhudhuria kliniki kwa mashauri na huduma zingine zikiwemo za watoto wao. Kabla ya kupata huduma, kuna kipindi cha kuwaelimisha na kuwahamasisha wanawake hawa kuhusu jinsi ya kujilinda kiafya, matumizi ya vyakula bora na kuzingatia afya ya watoto wao. Wakati wa kuendeleza vikao hivi mawasiliano hutatizika kutokana na tofauti za lugha. Kwa mfano, kuna wakati ambapo lugha ya Kimaasai ambayo ndiyo lugha ya wenyeji walio wengi, hutumika katika baadhi ya vituo vya afya. Hata hivyo, si wote wanahudhuria kliniki hizi wanaelewa Kimaasai.

Tafsiri imekuwa ikitumika kutatua matatizo kama haya. Muhudumu wa afya ikiwa anaelewa Kimaasai, hutoa maelezo kwa Kimaasai na baadaye hufafanua na kuelezea kwa lugha ya Kiswahili na kwa kufanya hivyo, ujumbe unawafikia wote. Pale ambapo mhudumu wa afya haelewi lugha ya Kimaasai mkalimani hutumika ambapo ujumbe kutoka Kiswahili hutafsiriwa kiusemi hadi lugha ya Kimaasai. Hali hii inapelekea wote kunufaika kutokana na ujumbe na mawaidha yanayotolewa na wahudumu wa afya. Kazi ya wahudumu wa afya inakuwa rahisi na malengo yao yanatimia kwa urahisi.

Vijitabu vya ratiba ya kuhudhuria kliniki, huwa na habari muhimu kwa wanawake wajawazito na waliojifungua. Vijitabu hivi huwa na habari kuhusu siku na wakati wa kuhudhuria kliniki, aina ya vyakula na kiwango cha chakula anachostahili kutumia mama mjamzito, aina ya chanjo anayostahili kupata mtoto, wakati wa kupata, na magonjwa yanayozuiwa na chanjo husika. Habari hizi ni muhimu sana na akina mama wajawazito na waliojifungua wanastahili kuzielewa vyema. Vijitabu hivi huwa vimeandikwa katika lugha ya Kingereza na Kiswahili. Kuna wale wasioelewa lugha ya Kiswahili au Kingereza wala kusoma. Tatizo hili hutatuliwa kwa njia ya tafsiri. Muhudumu wa afya anayeelewa lugha ya Kimaasai, hupitia ratiba yenyewe na kuelezea maelezo kwenye kijitabu hiki kwa kusoma kwa Kiswahili.



Baadaye muhudumu huyu wa afya anaelezea na kufafanua yote aliyosoma kwa Kiswahili kwa lugha ya Kimaasai hatua kwa hatua. Kwa kufanya hivyo, wote waliohudhuria kliniki wanapokea ujumbe barabara huku wahudumu wa afya wakinufaika kwa kutimiza malengo yao.

Tafsiri imezidi kuimarisha huduma za kiafya kwa akina mama wajawazito na waliojifungua – kuna machapisho mafupi ambayo yamechapishwa. Machapisho haya huonyesha aina ya vyakula na kueleza jinsi vyakula hivi vinavyosaidia mwili na kuimarisha afya.

Pia, machapisho haya huwa na maelezo mengine muhimu kwa afya ya akina mama hawa na watoto wao. Machapisho haya yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kutafsiriwa katika lugha ya Kimaasai. Hebu tuangalie mifano ya maelezo yaliyo katika machapisho kama haya.

Maelezo ya Kiswahili:

#### VYAKULA VYA KUJENGA MWILI:

- i) Maziwa
- ii) Nyama
- iii) Samaki
- iv) Mayai
- v) Maharagwe
- vi) Njugu

#### VYAKULA VYA KUONGEZA NGUVU

- i) Mahindi
- ii) Bidhaa za ngano (mkate, chapati)
- iii) Viazi
- iv) Ndizi za kupikwa
- v) Mchele
- vi) Ugali

#### VYAKULA VYA KULINDA MWILI

- i) Kila aina ya matunda kama: machungwa, maembe, mananasi, ndizi
- ii) Kila aina ya mboga kama: sukumawiki, kabeji, managu, spinach, terere, saageti

#### HAKIKISHA YA KWAMBA:

- i) Tumia vyakula hivi vyote kwa kiwango ulichoagizwa na muhudumu wa kliniki.
- ii) Kunywa maji safi kama ulivyoagizwa.
- iii) Wamama wajawazito wafanye mazoezi kama walivyoagizwa

iv) Watoto wanyonyeshwe bila kupewa chakula kingine hadi umri wa miezi sita.

LINDA AFYA YAKO NA YA MTOTO!

Maelezo haya kwa lugha ya Kimaasai:

INDAKIN NAASHET OSESEN

- i) Kule
- ii) Nkiri
- iii) Isingirr
- iv) Irmosorr
- v) Impoosho
- vi) Injugu

INDAIKIN NAAPONAA ENGOLON

- i) Irpaek
- ii) Intokitin enkano (emkate, bofulo)
- iii) Nkwashen
- iv) Ilmaisurin looyieri
- iv) Ormushele
- v) Orgali

INDAIKIN NAIRRITA OSESEN

- i) Impukunot pookin olng'anayio: irmashungwa, irmaembe, ormananasi, oo rmaisurin.
- ii) Impukunot pookin oo mbuka naijo: masaro, kapish, ormomoi, isipinach, interere o saaget.

TODUA AJO:

- i) Intumia kuna daikin pookin terisioroto nekitiaka orkitarri
- ii) Tooko enkare sidai enaa enikitiakaki
- iii) Ore intuaan neiteneneng iseseni enaa enatiakaki
- iv) Peitanaki inkera pookin ometabaiki ilapaitin ile eitu eishori enkae daa

TORRIPO BIOTISHO INO WENE NKERAI!

Katika kijisehemu hiki tumeona jinsi tafsiri inavyofanikisha mawasiliano na kuwanufaisha akina mama wajawazito, akina mama waliojifungua na watoto wao. Hata hivyo bado kuna changamoto. Viji tabu ambavyo huwa vimechapishwa mara nyingi huwa na makosa kwa sababu wanaofanya kazi ya kutafsiri hawana ujuzi wa taaluma ya tafsiri. Hali kama hii mara nyingi husababisha upotovu wa maana.

Pia kulingana na utamaduni wa Kimaasai kuna aina ya vyakula ambavyo haviliwi. Kwa mfano, samaki na aina za mboga kamama *nanagu, terere* na *saaget*. Hali hizi zote hulete utata katika mawasiliano.

#### **4.3.5 Uhamasishaji wa Umma Kuhusu Afya Bora**

Wahudumu wa afya hutembelea shule, makanisa, vijiji na maeneo mengine Umaasaini ili kuhamasisha umma kuhusu afya bora. Umma hufahamishwa jinsi ya kuzingatia usafi, namna ya kujilinda dhidi ya magonjwa ya kuambukizwa na kampeni ya kuangamiza magonjwa kama polio na ukambi nchini.

Wahudumu hawa wa afya huandaa mikutano katika maeneo mbalimbali ili kufikia idadi kubwa ya umma. Kutokana na muktadha au mazingira ya wingilugha, matatizo ya kimawasiliano huzuka. Katika mikutano kama hii inayoandaliwa na wahudumu wa afya, tafsiri husaidia sana. Kupitia tafsiri, ukalimani hufanikisha mawasiliano na umma hunufaika. Maelezo ya kimaandishi ambayo kwa wakati mwingi huwa yameandikwa katika lugha ya Kingereza, husomwa kisha kuelezewa umma na kufafanuliwa katika lugha za Kimaasai na Kiswahili. Huwa kuna vijatabu vidogo ambavyo hutolewa wakati wa mikutano kama hii na kuna vile vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili, Kimaasai au Kingereza. Viji tabu hivi vyote na lugha hizo mbalimbali, huwa na ujumbe sawa. Jambo hili limefanikishwa na tafsiri. Kama tulivyoona mengi yamefanikishwa na tafsiri katika sekta ya matibabu. Sekta ya matibabu imeimarika na kunufaika na wanajamii wameweza kupokea huduma bora.

#### **4.4 Manufaa ya Tafsiri katika Sekta ya Dini**

Katika sehemu hii tumeangazia jinsi tafsiri ilivyoweza kuimarisha mawasiliano katika sekta ya dini. Kuimarika kwa mawasiliano katika sekta hii ya kidini imepelekea kukua na kupanuka kwa sekta hii. Katika maeneo yetu ya utafiti, dini iliyoenea zaidi na kukomaa ni dini ya kikristo.

Hii ndiyo dini iliyo na waumini wengi walio wafuasi wa madhehebu tofauti tofauti katika sehemu mbalimbali. Waumini wa madhehebu haya ni wa matabaka tofauti tofauti kutoka jamii tofauti tofauti. Baadhi ya waumini wa madhehebu haya ni wenyeji kutoka jamii ya Wamaasai. Waumini wengine wanatoka katika jamii zingine zisizozungumza lugha ya Kimaasai.

Mara kwa mara, mawasiliano hutatizwa katika sekta hii ya kidini kutokana na jamii tofauti zinazozungumza lugha tofauti. Kwa kupitia tafsiri, tatizo la mawasiliano limeweza kukabiliwa na sekta hii ya kidini kunufaika. Hebu tuangalie jinsi tafsiri ilivyoweza kufanikiwa na kuleta manufaa katika sekta ya kidini katika viwango tofauti tofauti.

#### **4.4.1 Tafsiri ya Biblia ya Kimaasai Kutoka Tafsiri ya Kiswahili**

Biblia ndicho kitabu kitakatifu cha Wakristo. Wakristo wanaamini ya kwamba maneno yote yaliyo katika Biblia yametoka kwa Mungu aliyewaumba. Masomo yote wanayopata yana msingi wake kutoka kwenye Biblia. Mahubiri yote yanahubiriwa kwa misingi ya Biblia. Hivyo, Biblia ndiyo nguzo kuu au dira inayomwongoza Mkristo yeyote. Mafunzo yoyote ya kidini na maagizo yanaeleweka vyema kupitia lugha ambayo inaeleweka vyema na muumini wa dini fulani. Kwa mfano, mtu anayeelewa lugha ya Kiswahili vyema, imani yake inajengeka na kunawiri kutoka mafunzo yanayotolewa kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni sawa kwa mtu anayeelewa na kujimudu katika lugha ya Kimaasai. Jambo hili limefanikishwa pakubwa na taaluma ya tafsiri. Kupitia tafsiri, Biblia takatifu iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili imeweza kutafsiriwa katika lugha ya Kimaasai. Kwa ushirikiano wa “Bible Society of Kenya, Nairobi” na “Bible Society of Tanzania, Dodoma” tafsiri ya Biblia ya Kimaasai’ imeweza kuchapishwa.

Biblia takatifu imetafsiriwa kama **Biblia Sinyati**.

Hebu tuangalie kwa kupitia mifano, mambo muhimu katika Biblia na tafsiri yake kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kimaasai.

Mifano yote na nukuu za Kiswahili ni kutoka katika: *Neno Biblia Takatifu*(2009)

Mifano yote na nukuu za Kimaasai ni kutoka katika: *Biblia Sinyati*(1991)

#### **Kiswahili**

Agano la kale

Agano jipya

#### **Kimaasai**

Oсотua musana

Oсотua ng’ejuk

Mifano ya vitabu vya agano la kale:

**Kiswahili**

Mwanzo  
Kutoka  
Mambo ya walawi  
Hesabu  
Kumbukumbu la torati  
Waamuzi  
Wafalme  
Mambo Ya Nyakati  
Zaburi  
Mithali  
Mhubiri  
Wimbo Ulio Bora

**Kimaasai**

Enkiterunoto  
Enaidurra  
Ilawi  
Enkikena  
Enkigilata oo nkitanapat  
Ilarishak  
Ilaiguanak  
Intepen  
Olkerempe Le Ngai  
Ndung'et Erashe  
Olaikooni  
Osinkolio Le Solomon

Mifano ya vitabu vya agano jipya:

**Kiswahili**

Mathayo  
Matendo  
Warumi  
Wakorintho  
Wagalatia  
Waefeso  
Wafilipi  
Wakolosai  
Wathesalonike  
Waebrania  
Ufunuo

**Kimaasai**

Matayo  
Laasat  
Iroma  
Ilkorintio  
Ilgalatia  
Ile Efeso  
Ifilipi  
Ilkolosai  
Ilsesalonike  
Ilhebrania  
Embolunoto

Hebu tuangalie baadhi ya maandiko maarufu yanayotumika katika mafunzo:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p><b>Mwanzo 1:1 – 5</b></p> <p>Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena tupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; roho ya Mungu ikatulua juu ya uso wa maji. Mungu akasema, iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru yakuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza, Mungu akaita nuru mchana, na giza akaliita usiku. Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku moja.</p> <p><b>Mwanzo 1: 26 – 27</b></p> <p>Mungu akasema na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki na baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu. Alimuumba mwanamume na mwanamke aliwaumba.</p>	<p><b>Enkiterunoto 1:1 -5</b></p> <p>Ore apa tenkiterunoto, neitaa Enkai keper o nkop. Ore apa enkop nemeeta shoto, nemetii toki naa enaimin naati oriog o enguton, ore enkiyang’et Enkai nelo tioriong inkariak. Nejo Enkai; inchoo metijing’a ewang’an,nejing ewang’an. Nedol Enkai ajo aisidai ewang’an. Nerishu Enkai ewang’an arishie enaimin. Neipot Enkai ewang’an ajo endama, neipot enaimin ajo enkewarie. Neaku eetae enteipa entadekenya enklolong edukuya.</p> <p><b>Enkiterunoto 1: 26 – 27</b></p> <p>Nejo enkai emaitobira tung’ani tenkitanyaanyukoto aang onyaanyukie iyiook, nikincho ninche meitoria isinkirr le naiposha, o motonyi oloing’ang’e, o nkishu, o enkop pooki o pooki toki naiser’pepiari ten kop. Metaa eitayio enkai oltung’ani te nkitanyaanyukoto enye makewan. Tenkitanyaanyukoto enkai eitayio ninye ninche, olee o eng’oruo.</p>

Kiswahili	Kimaasai
<p><b>Zaburi 23</b></p> <p>BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapungikuwa kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji matulivu BWANA huniongoza. Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Naam nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji. Waandaa meza mbele yangu, na kikombe changu kinafurika. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu. Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele.</p> <p><b>Yohana 3: 16</b></p> <p>Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.</p>	<p><b>Olkerempe le Enkai 23</b></p> <p>Olaitoriani ninye olchekut lai, maang'oriki ninye nanu toki; aairragie ninye nanu too nkujit naanyori, naarirkoo ninye nanu te nkiopata oo nkariak naitirring'a neitagol ninye oltau lai. Naarikoo ninye nanu tenkoitoi oo sipat te nkarake enkarna enye. Tena napaji ninye kalo aim oerata lo loip le keeya nemaure entorroni amu itti iyie tenebo nanu; Eng'udi ino orinka lino ninche naitagol nanu. Ntobira iyie emisa te dukuya nanu, teine netii ilmang'ati lainei; nibukoki endukuya ai eilata, nipik enkikombe ai metaa kedooyo. Esipa aasuju esidano o ing'ur inkolong'I pooki e nkishui ai, naa kbik nanu ti atua enkaji o laitoriani ntarasi.</p> <p><b>Yohana 3: 16</b></p> <p>Amu etonyorra enkai enkop aiko nji o meishoru enkerai enye nabo, paa ore pooki ng'ae oiruk nemeimin kake netum enkishui nemeish.</p>

Kama tulivyoona tafsiri imenufaisha kwa kiwango kikubwa sekta ya dini.

Watu wengi wanaoelewa lugha zao za kwanza pekee wameweza kupokea mafunzo ya kidini, hivyo imani yao kukua na kumkaribia Muumba wao. Watu wameweza kuishi kwa uadilifu, uvumilivu na kiasi kwa kupitia mafunzo ya kidini. Watu wengi wameweza kusoma Biblia kwa lugha wanayoelewa zaidi, wasiojua kusoma pia wanapokea ujumbe kupitia lugha wanayoelewa vyema. Wahubiri wanaweza kufunza na kunukuu maandiko matakatifu kwa lugha ambayo wanaimudu vilivyo. Yote haya yamefanikishwa na tafsiri. Kwa jumla kama tulivyoona tafsiri imeleta ufanisi mkubwa katika sekta hii ya dini. Hata hivyo, mawasiliano yamekumbwa na utata kwa sababu ya mambo kadha. Biblia inatoa mifano nyingi sana ambayo inafungamana na utamaduni wa Kiyahudi. Kwa mfano aina ya vyakula vinavyorejelewa ni samaki na mkate. Majina yanayotajwa ni ya Kiyahudi. Mazingira yanavyorejelewa ni ya nchi ya Israeli. Mambo haya yote yanasababisha ukinzani wa kitamaduni na kutatiza mawasiliano.

#### **4.4.2 Tafsiri za Nyimbo za Kusifu**

Nyimbo ni sehemu muhimu sana katika ibada yoyote ile kwa maana ibada haiwezi kukamilika pasipo kumsifu Mungu kwa nyimbo za sifa na za kuabudu. Katika kila ibada ya madhehebu tofauti tofauti, mafundisho na shughuli zingine huandamana na nyimbo. Nyimbo huchukuliwa kama njia moja wapo ya kuabudu. Vile vile nyimbo hutumiwa kueneza neno la Mungu ambapo kupitia nyimbo za injili, ujumbe kulingana na neno la Mungu hupitishwa kwa kukariri maandiko matakatifu kwenye nyimbo. Kuna nyimbo zilizoandikwa kwenye vitabu katika lugha tofauti tofauti na ambazo huimbwa makanisani kwa kutumia vitabu hivi. Kwa mfano, kuna vitabu vya Kiswahili vya nyimbo kama ‘Tenzi za rohoni’ na ‘Nyimbo za kusifu’. Idadi kubwa ya nyimbo hizi huwa ni tafsiri kutoka kitabu cha Kingereza kiitwacho ‘Golden bells’. Nyimbo za kusifu za Kiswahili kwenye kitabu kiitwacho ‘Nyimbo za kusifu’ zimeweza kutafsiriwa katika lugha ya Kimaasai kwenye kitabu kiitwacho ‘Isinkoliotin enkisisa’ (Nyimbo za kusifu). Nyimbo hizi zimeweza kuongezwa katika orodha ya nyimbo za Kimaasai na kufaidi na kubariki waumini. Hebu tuangalie baadhi ya nyimbo kama hizi na tafsiri yake.



Kiswahili	Kimaasai
<p>i) USIKU MTAKATIFU (nyimbo za sifa -118)</p> <p>Usiku takatifu  Yesu asifiwe,  Amezaliwa leo mtoto,  Mwana mtakatifu mpole,  Yesu akasifiwa.</p> <p>Usiku takatifu,  Ambayo wachungaji wameona,  Wakaimba kumsifu Mungu kabisa,  Wakaimba wote haleluya,  Yesu amezaliwa,  Kwa upendo wa Mungu.</p> <p>Usiku takatifu,  Siku ya furaha,  Tumefunguliwa,  Sifa ya Baraka,  Kwa kuzaliwa kwake,  Kwa upendo wake.</p> <p>Mungu akapewa,  Shukrani na kusifiwa,  Kwa kupeana kwake,  Ametupa sisi mtoto wake,  Yesu mtakatifu,  Mwokozi.</p>	<p>ENKEWARIE SINYATI (Isinkoloitin  Enkisisa-167)</p> <p>Enkewarie sinyati,  Neisisi enkai,  Etoiouoki duo enkerai,  Enkerai sinyati nabor,  Nerura to sotua,  Neisisi enai</p> <p>Enkewarie sinyati,  Naatoduaa lairritak,  Nerany aasis enkai naleng,  Nerany pooki haleluyia,  Etoiouoki jesu,  Te nyorrata enkai.</p> <p>Enkewarie sinyati ,  Enkolong e nchipai,  Etabolokoki iyiook,  Enkisisa emunyani,  Te inoto enye,  Te nyorrata enye.</p> <p>Neishori enkai,  Enashe neisisi,  Te nkishorunoto enye,  Eishoo iyiook enkerai enye,  Jesu osinyati,  Olaitajeunoni lang.</p>

Kiswahili	Kimaasai
<p>ii) AMINI NA KUTII (nyimbo za kusifu -120)</p> <p>Tukiandamana,  Yesu na mimi,  Upendo wake ni mkuu,  Kwa sababu tunaielewana,  Kwa sababu nimeamini,  Atakayo yeye kabisa.</p> <p>Nikiwa na shauku ,  Ama uvivu,  Nikiangalia uso wake,  Kwa wakati huo mgumu,  kwa hii Baraka,  kwa sababu ya nguvu zake.</p> <p>Eh, sikizeni,  Pendeni,  Hakuna njia nyingine mbinguni,  Utaingia tu kwa kumpitia yesu.</p> <p>Hatuwezi kuujua,  Upendo wake,  Tukikataa kumpa yeye upendo wetu,  Ukitaka manufaa,  Na baraka ya Mungu,  Utapata ukiamini na kumkubali.</p> <p>Wacha akutawale,  Kwa yote ufanyayo,</p>	<p>ENTONING ENTONYOR (Isinkoliotin  Enkisisa-178)</p> <p>Tini kiriamari,  Yesu o nanu,  Ai sapul enyorrata enye,  Amu kiningo,  Amu airuko,  Enaiyieu ninye katukul.</p> <p>Ten aata olngash,  Asho enchalan,  Ten aigor enkomom enye,  Te ina kata nagolu,  Tena maiyianata,  Enkarake engolon enye,  Ai , entoning,  Entonyor,  Metii ai oitoi keper,  Yesu ake limie.</p> <p>Mikindim aataiyiolo,  Tini kiaany kincho ninye enaang,  Tin iyieu murrunei,  O emunyani enkai,  Nitum tin iruk ninyorraa.</p> <p>Incho kintore,  Te pooki ni aas,</p>

<p>Na usipate woga, Mkutane siku za usoni, Mji wa mbiguni, Kisa sababu ya kuamini.</p>	<p>Nimitum enkuretisho, Nitumomo Kenya, Te nkange e keper, Nkaraki enkirukoto.</p>
--	--

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p>iii) HABARI YA FURAHA (Nyimbo za Kusifu -140)</p> <p>Haya ndiyo maneno ya furaha , Yaliyokuja hii nchi yetu, Neno nzuri, Ya huyo mwokozi wetu. Neno nzuri limekuja, Lituambialo sisi sote, Msamaha wake, Upendo wa yesu.</p> <p>Upendo ni mzuri, Mwokozi wetu, Ameacha mbingu, Akaja kutuhurumia.</p> <p>Ametufia , Ndiposa awe kafara, Yesu yeye akaja, Kubeba dhambi zetu.</p> <p>Tumwambie kila mtu,</p>	<p>ILOMON LE NCHIPAI (Isinkoliotin Enkisisa -192)</p> <p>Kulo ilomon le nchipai, Oetuo ena kop ang, Ororei sidai, Elelo aitajeunoni lang. Eewuo ororei supat, Oliki iyiook pooki, Empalakinoto enye, Enyorrata e yesu.</p> <p>Ai sapuk enyorrata, Olaitajeunoni lang, Etunguaiyie iyiook. Etananga apa iyiook, Peiyie eaku olasar, Nelotu ninye yesu, Anap ingok ang pooki.</p> <p>Matoliki pooki ngai, Ilo rorei le yesu, Kintodol iloreren,</p>

<p>Hilo neno la Mungu, Tukionyesha mataifa, Upendo wa yesu.</p> <p>Tuimbe sifa, Kwa haya mataifa yote , Hadi mataifa yote yaache dhambi.</p>	<p>Enyorrata e yesu.</p> <p>Pee kirany enkisisa, Te kuna nkuapi pooki, O metaba anaa Nepal, Iloshon pooki ingok.</p>
--	--

Kama tulivyoona , kupitia tafsiri sekta ya dini imeweza kunufaika kupitia tafsiri za nyimbo haswa kutoka Kiswahili hadi Kimaasai. Waumini wamepata fursa ya kumsifu Mungu kwa nyimbo nyingi na tofauti tofauti. Kutokana na mauzo ya vitabu vya nyimbo hizi za injili pamoja na kanda za CD, sekta hii ya dini na wanaojishughulisha kimuziki wananufaika kiuchumi. Haya yote yamefanikishwa na tafsiri. Licha ya manufaa kutokana na tafsiri za nyimbo hizi, athari yake ya kidini kwa waumini imekuwa chini ikilinganishwa na nyimbo ambazo waumini wamejitungia kupitia lugha yao ya Kimaasai.

#### **4.4.3 Kanisani katika Ibada za Jumapili**

Ibada za Jumapili ni muhimu sana kwa Wakristo. Jumapili ni siku ambayo inachukuliwa kuwa takatifu na hutengwa kwa sababu ya kumuabudu na kumsifu Mungu. Shughuli zingine zote husitishwa na Mungu kupewa nafasi hii ya kwanza na hii inaenda sambamba na amri ya Mungu kuhusu siku ya sabato kulingana na Biblia takatifu. Katika ibada kama hizi wahudhuriaji hutoka maeneo mbali mbali, na jamii tafauti tafauti hujumuika pamoja ili kumuabudu Mungu. Umaasaini, mahubiri aghalabu huhubiriwa kwa lugha ya Kimaasai na Kiswahili na wakati mwingine Kingereza. Katika ibada kama hizi si watu wote waliohudhuria huelewa lugha ya Kiswahili na Kimaasai. Hali hii inapelekea kuwa na tatizo la mawasiliano. Hii ni kwa sababu mahubiri yakiendelezwa kwa lugha ya Kimaasai kuna baadhi ya waumini wasioelewa lugha ya Kimaasai.

Vile vile mahubiri yakiendelezwa kwa lugha ya Kiswahili, kuna baadhi ya waumini wasioelewa lugha ya Kiswahili vizuri haswa waumini kutoka jamii ya Wamaasai. Hali inapakuwa hivi, tafsiri hutumiwa ili kutatua matatizo kama haya ya kimawasiliano.

Kuna baadhi ya waumini ambao wanajimudu vilivyo katika lugha hizi mbili ambazo ndizo hutumika mara kwa mara katika ibada za Jumapili yaani; Kiswahili na Kimaasai. Kwa kutumia ujuzi wa tafsiri, waumini hawa hutumika kama wakalimani. Kama mahubiri yanaendelezwa kwa kutumia lugha ya Kimaasai basi mkalimani ataeleza na kufafanua kwa njia ya usemi kwa lugha ya Kiswahili. Iwapo mahubiri yatakuwa kwa lugha ya Kiswahili basi mkalimani ataeleza na kufafanua kwa lugha ya Kimaasai. Tafsiri imefanikiwa kuimarisha mawasiliano katika ibada za Jumapili. Wote wanaohudhuria hizi ibada wanapokea mahubiri kupitia lugha wanayoielewa vyema na pia wahubiri wasioelewa lugha za Kiswahili na Kimaasai wanaweza kufikisha ujumbe wao kwa waumini kwa usaidizi wa mkalimani.

Tafsiri, hivyo, imewawezesha waumini kutoka jamii mbalimbali kuhudhuria ibada za Jumapili katika makanisa wanayoyapenda, yawe mbali au karibu. Tafsiri vile vile imewawezesha wageni kutoka sehemu mbalimbali kualikwa kwenye makanisa kuhubiri pasipo kujali matatizo ya kimawasiliano. Tafsiri imewawezesha kuongezeka kwa idadi ya makanisa sawa na waumini. Watu wameweza kupokea mafundisho ya kidini popote walipo licha ya misingi tofauti ya kijamii. Ibadat za Jumapili zimeweza kuimarika kimawasiliano kama tulivyoona lakini kuna matatizo ya hapa na pale. Wakati mwingine ujumbe asilia hupata mabadiliko yanapotafsiriwa na mkalimani. Hali hii inapotokea mawasiliano hutatizwa. Tofauti za kiwango cha elimu haswa elimu ya kidini mara kwa mara huathiri mawasiliano wakati wa kukalimani.

#### **4.4.4 Mabango ya Kutangaza Mikutano ya Injili na Vibao vya Kuelekeza Watu.**

Ili kuweza kufikia watu wengi zaidi kuhudhuria mikutano ya injili, mabango hutumika kueneza ujumbe. Mabango kama haya husambazwa maeneo mbalimbali yanayolengwa. Mabango haya hutundikwa kutani, milangoni, kwenye vigingi vya stima na sehemu zingine ambazo mabango yanaweza kuonekana na kusomeka kwa urahisi. Mabango hayahuwa yamelenga watu tofauti tofauti kutoka jamii tofauti tofauti. Ili kufanikisha mawasiliano miongoni mwa jamii tofauti tofauti zinazolegwa, mabango huandikwa, kwa mfano katika lugha ya Kimaasai na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili. Hebu tuangalie baadhi ya jumbe zinazopitishwa kupitia mabango.

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p>TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!  DELIVERANCE MINISTRIES  INTERNATIONAL:  WANAWAALIKA KWA MKUTANO WA  INJILI  WAPI: UWANJA WA SHULE YA MAASAI  GIRLS  LINI: KUENZIA 13/04/2016 HADI  17/04/2016 KILA SIKU KUENZIA:  SAA NNE ASUBUHI HADI SAA KUMI NA  MBILI JIONI  WAIMBAJI NA WAHUBIRI KUTOKA  TANZANIA WAMEALIKWA  NJOO UPOKEE MUJIZA WAKO  NYOTE MWALIKWA KATIKA JINA LA  YESU  MATHAYO 11:28</p>	<p>ORKILIKWAI! ORKILIKWAI!  ORKILIKWAI!  DELIVERANCE MINISTRIES  INTERNATIONAL:  EITOOMON INTAE TE NTUMO LORORI  LENKAI  TIAJI: TENKIWANJA ESUKUUL E  MAASAI GIRLS  ANU: EITERU 13/04/2016 IMPAKA  17/04/2016 INKOLONGI POOKIN EITERU:  SAA ONGWAN ENTEDEKENYA MPAKA  SAA TOMON ENTEIPA  EITONOKI ILARANYAK OLALIKIOROK  LOINGUAA TANZANIA  WOU TANGAMU ENKINGASIA INO  EITOOMONI INTAE POOKI  TENKARNA EYESU  MATAYO 11:28</p>

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p>KANISA LA FOUNTAIN NAROK  LINA FURHA KUKUALIKA KATIKA:  “USIKU MMOJA NA MFALME”  MKESHA WA MAAJABU NA MIUJIZA  APOSTLE JAMES LEWIS TIRA  ATAHUBIRI  WAIMBAJI WA JOY SINGERS  WATAKUBARIKI  NI LEO! LEO! TAREHE 11/2/2016  MAMBO YATABADILIKA IJUMAA HII.  KUMBUKA MKESHA UTAANZA SAA  KUMI NA MBILI JIONI HADI SAA KUMI  NA MBILI ASUBUHI  NYOTE MNAKARIBISHWA</p>	<p>KANISA E FOUNDATAIN NAROK  EETA ENCHIPAI KINTOOMON TE:  “ENKEWARIE NABO O KINGII”  KESHA ENKINGASIA OMBAA SAPUKI  OLAIRITANI JAMES LEWIS TIRA OIBURI  OLARANYAK LE JOY SINGERS  LIKIMAYIAN  NAA TAATA! TAATA! NTARIKINI  11/3/2016  EIBELEKENYA MBAA ENA JUMAA.  TADAMU AJO EITERUNYE KESHA SAA  TOMON ARE ENTEIPA MPAKA SAA  TOMON ARE ENTEDEKENYA  EITOOMONI INTAE POOKI.</p>

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p>FULL GOSPEL CHURCHES OF KENYA  NAROK TOWN:  WANAWATANGAZIA SEMINA YA  AKINA MAMA KUENZIA TAREHE  10/2/2016 HADI 13/2/2016 JIANDIKISHE  NA KSH 500 PEKEE.  JE NENO LINASEMA NINI KUHUSU  NDOA?  AKINA MAMA WOTE MNAALIKWA</p>	<p>FULL GOSPEL CHURCHES OF KENYA  NAROK TOWN:  ELIKINI INTAE SEMINA OONTOMONOK  NAITERU NTARIKINI 10/2/2016MPAKA  NTARIKINI 13/02/2016 NCHOOKI NGERI  TOONCHILIKINI 500 AKE  AMAA KEJO OROREI AA LOPIRTA  KIYAMA?  NTOMONO POOKI EITOOMONI INTAE</p>

Vibao vile vile, hutumika ili kuonyesha mahali ambapo kanisa fulani lipo. Vibao kama hivi pia hutoa maelezo kuhusu utaratibu wa ibada na shughuli zingine za wiki. Maelezo ya Kimaasai huambatanishwa naya Kiswahili kupitia tafsiri kwa lengo la kulenga watu wote. Tazama mfano:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kimaasai</b>
<p>A.I.C ILMASHARIANI</p> <p><u>IBADA ZETU</u></p> <p>JUMAPILI:</p> <p>SAA MBILI HADI SAA TATU ASUBUHI:</p> <p>MAOMBI.</p> <p>SAA TATU HADI SAA NNE ASUBUHI:</p> <p>MAFUNZO YA BIBILIA</p> <p>SAA NNE HADI SAA SITA MCHANA:</p> <p>MAHUBIRI</p> <p>JUMANNE:</p> <p>SAA KUMI NA MOJA NA NUSU JIONI:</p> <p>MAOMBI</p> <p>IJUMAA:</p> <p>SAA MOJA JIONI NA KUENDELEA:</p> <p>MAOMBI</p> <p>KARIBUNI KWA IBADA ZETU</p>	<p>A.I.C ILMASHARIANI</p> <p><u>IBAADA ANG</u></p> <p>JUMAPILI:</p> <p>SAA ARE MPAKA SAA UNI TEDEKENYA:</p> <p>ENKOMONO</p> <p>SAA UNI MPAKA ONGWAN</p> <p>TEDEKENYA:</p> <p>INKITENGENA E BIBILIA</p> <p>SAA ONGWAN MPAKA SAA ILE</p> <p>ENDAMA:</p> <p>OLALIKIORONI</p> <p>JUMAINE:</p> <p>SAA TOMON OBO ONUSU ENTEIPA:</p> <p>ENKOMONO</p> <p>JUMAA:</p> <p>SAA NABO ENTEIPA NEENDELEA:</p> <p>ENKOMONO</p> <p>EITOOMONI INTAE TE IBAADA ANG</p>

Kama tulivyoona ujumbe unapitishwa kupitia kwa mabango na vile vile kupitia kwa vibao.



Tafsiri imeweza kurahisisha mawasiliano kwa kufikia watu wengi kwa lugha wanazozielewa. Jambo hili limefanikisha shughuli za kidini na kunufaisha sekta ya dini kwa jumla. Tafsiri imeweza kufanikisha mawasiliano kupitia mabango na vibao kama ilivyodhihirika. Hata hivyo katika baadhi ya mabango na vibao, kumekuwa na makosa ya kuendeleza na makosa ya kisarufi. Pia tumeshuhudia hali ya kuchanganya ndimi katika jumbe mbali mbali. Hali hizi zote huchangia matatizo ya kimawasiliano.

#### **4.4.5 Mahubiri ya Hadharani na Mikutano ya Wachungaji.**

Mahubiri ya hadharani huandaliwa mara kwa mara katika sehemu mbalimbali. Mahubiri haya huandaliwa ili kuwafikia watu ambao hawapati nafasi ya kuhudhuria ibada za Jumapili na ibada zingine ambazo huandaliwa makanisani. Pia kuna wale ambao hawataki kwenda makanisani hata kama hawana shughuli zozote. Mahubiri haya ya hadharani hulenga maeneo ya makazi ya watu, maeneo ya shughuli za kibiashara kama viwanja vya soko na sehemu zingine ambazo zina idadi kubwa ya watu. Maeneo kama haya hujumuisha watu kutoka jamii mbalimbali katika shughuli zao. Watu hawa huzungumza lugha tofauti tofauti ikiwemo lugha ya wenyeji ya Kimaasai. Kuna wale wenyeji wanaoelewa Kimaasai pekee na kuna wale ambao si wenyeji na hawaelewi lugha ya Kimaasai.

Mara nyingi mahubiri haya ya hadharani huhubiriwa kwa lugha za Kimaasai na Kiswahili. Kutokana na hali tuliyoelezea hapo juu, wakati wa mahubiri haya kunazuka matatizo ya mawasiliano. Ili kukabiliana na matatizo haya ya kimawasiliano kwa kupitia tafsiri mkalimani hutumiwa katika mahubiri. Mkalimani husaidiana na muhubiri. Ikiwa muhubiri anatumia lugha ya Kimaasai kwa mfano, mkalimani hutumiwa kueleza mahubiri kwa lugha ya Kiswahili. Kama muhubiri anatumia lugha ya Kiswahili basi atasaidiwa na mkalimani atakayetumia lugha ya Kimaasai. Jambo hili limefanikisha mahubiri ya hadharani ambapo watu wengi wameweza kufikiwa na jumbe na kwa lugha wanayoelewa. Wachungaji huja pamoja ili kujadili mambo tofauti tofauti kuhusu huduma na jinsi ya kuimarisha huduma hizi. Kwa mfano, katika maeneo yetu ya utafiti wachungaji wamekuja pamoja na kuunda kikundi kiitwacho “Narok Pastors Association” Kundi hili huja pamoja kupanga mikakati ya kuimarisha uhusiano wao, kuimarisha miradi ya makanisa, kufikia watu wengi na kuleta umoja mwingoni mwa wanajamii. Wachungaji hawa ni wakutoka jamii tofauti tofauti, hivyo wanapojadiliana kuhusu mambo mbalimbali wakati mwingine mawasiliano hukatizwa.

Hali hii hupelekea mkalimani kutumika kufanikisha mawasiliano. Mikakati ya wachungaji kama hawa hufanikiwa na kuimarika kutokana na tafsiri. Kama tulivyoona katika sehemu hii, ni dhahiri kwamba sekta ya dini imeweza kunufaika kabisa kwa kupitia tafsiri. Hata hivyo mawasiliano yametatizwa pale ambapo mkalimani hawsa anayetafsiri hadi Kiswahili anaathiriwa na lugha yake ya kwanza.

#### **4.5 HITIMISHO**

Katika sura hii tumeangazia manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Tumeangalia jinsi tafsiri imeweza kuimarisha mawasiliano katika sekta mbalimbali na jinsi sekta hizi zilivyonufaika. Baadhi ya sekta ambazo tumeangazia ni pamoja na sekta ya elimu. Katika sekta hii tumeona jinsi vitengo mbalimbali vya sekta hii vilivyonufaika. Kwa mfano, tumeona jinsi shule za chekechea na shule za msingi haswa madarasa ya chini yalivyoweza kujifunza lugha ya Kiswahili kupitia kwa tafsiri. Tumeona jinsi shule za watu wazima zilivyonufaika kupitia tafsiri. Katika sekta ya elimu pia tumeona jinsi lugha za kwanza zinavyoweza kujikuza kimsamiati na msamiati huu kutumika kufundishia mambo mbalimbali. Katika sekta ya matibabu tumeona jinsi wanaowatembelea wagonjwa wanavyowezeshwa kupata habari muhimu kwa lugha wanayoielewa. Tumeona jinsi kampeni dhidi ya magojwa ya watoto ilivyofanikishwa na tafsiri kwa kuimarisha mawasiliano baina ya wahudumu wa afya na wanajamii. Pia katika sekta hii, ya matiabu tumeona jinsi kliniki za kina mama wajawazito na waliojifungua zilivyonufaika kwa kupitia tafsiri. Kwa kupitia tafsiri tumeona jinsi mawasiliano yalivyoimarishwa na kuwawezesha wahudumu wa afya kuwahamasisha wanajamii kuhusu afya bora na kuwatahadharisha dhidi ya magojwa hatari kama ukimwi, malaria na kipindupindu. Hatimaye tumeona jinsi sekta ya dini ilivyoweza kunufaika kupitia tafsiri. Tumeona jinsi tafsiri ya Biblia kutoka Kiswahili hadi Kimaasai ilivyowanufaisha waumini na wachungaji.

Aidha tumeona jinsi nyimbo zilizotafsiriwa kutoka Kiswahili hadi lugha ya Kimaasai zilivyotumiwa kwa kumsifu na kumuabudu mwenyezi Mungu. Pia tumeona ibada za Jumapili zikiimarika kupitia tafsiri, mawasiliano kupitia mabango na vibao, mahubiri ya hadharani na mikutano ya wachungaji yote zimeimarishwa na kufanikishwa na tafsiri. Kwa jumla tumeona manufaa ya tafsiri.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Katika sura hii ya tano tumeangazia muhtasari wa utafiti wetu kwa jumla; kwa kupitia yale yote tuliyoangazia katika sura ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne. Katika surahii vile vile tumetamatisha kazi yetu kwa kutoa matokeo ya utafiti wetu na kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

#### **5.2 Muhtasari wa Utafiti**

Katika utafiti huu tulidhamiria kutafitia changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika muktadha wa wingilugha na tuliteua maeneo ya Narok Kaskazini kama maeneo ya kufanyia utafiti wetu. Tuliona kwamba watu wanapoletwa pamoja na shughuli tofauti tofauti kutoka maeneo tofauti tofauti mazingira ya wingilugha huibuka. Katika mazingira ya wingilugha hutarajiwa kwamba watu wataweza kutumia lugha zinazowazingira lakini tumeona kwamba uhalisia ni kwamba watu wengi hawafanikiwi kupata ujuzi wa lugha zinazowazingira kikamilifu. Kufuatia jambo hili matatizo ya kimawasiliano huibuka. Ili kukabiliana na tatizo hili tuliona ni sharti pawe na lugha inayoweza kuleta watu pamoja. Katika utafiti wetu tuliona kwamba lugha yenyewe ni lugha ya Kiswahili, na tafsiri nayo, tukaona ndiyo njia ya pekee ya kufanikisha mawasiliano kwa kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza na kinyume chake. Tukaona pia kuwa licha ya tafsiri kufanikisha mawasiliano kuna changamoto katika kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza na kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili. Jambo hili lilitupa msukumo wa kuibuka na mada yetu ya utafiti.

Tuliweza kubainisha malengo yetu ya utafiti yaliyotuelekeza kubainisha changamoto zinazodhihirika katika shughuli za kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha, kudhihirisha manufaa yanayotokana na kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha na kuthibitisha mchango wa tafsiri katika kuimarisha mawasiliano katika miktadha ya wingilugha. Tuliweza pia kutabiri matokeo ya utafiti wetu kulingana na malengo yetu ya utafiti katika maswali ya utafiti wetu. Sababu ya kuchagua mada yetu ilikuwa ni kutaka kuchunguza na kutathmini changamoto na manufaa katika kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha.

Tuliona kwamba pana pengo kwa sababu mada hii haijawai kushughulikiwa vilivyo .Tuliweka upeo na mipaka yetu bayana na kuonyesha maeneo ambayo tumeshughulikia katika utafiti wetu. Tilitumia nadharia ya mawasiliano katika tafsiri kama dira ya utafiti wetu na tukathibitisha ufaafu wa nadharia hii katika utafiti wetu. Tuliweza pia kuangazia yaliyoandikwa na wataalamu wengine kuhusu mada yetu ya utafiti. Tuliangazia mchango wao katika utafiti wetu na pia tuliona mapengo yaliyodhihirika katika kazi za wataalamu hao na tukaangazia jinsi ya kufidia hayomapengo.

Katika utafiti wetu tulichunguza changamoto zinazotokana na kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha. Tuliona miongoni mwa changamoto hizi ni zile zinazotokana na tofauti za kitamaduni. Tuliangazia baadhi ya tofauti za kitamaduni zilizopo kati ya lugha ya Kimaasai na Kiswahili. Tuliona tofauti zinazosababishwa na, kwa mfano, aina ya vyakula, mavazi na mapambo, hali ya kuzawadiana kuimarisha uhusiano katika jamii, majina ya kurejelea wapendwa mwiongoni mwa masuala mengine ya kitamaduni. Tuliangazia pia, changamoto zinazosababishwa na tofauti za miundo ya lugha. Tuliangalia tofauti mbalimbali za kimuundo baina ya lugha za Kiswahili na Kimaasai. Kwa mfano, tuliona kauli ya uambishaji kama changamoto, viambishi vya masharti kama changamoto, muundo wa viunganishi kama changamoto miongoni mwa changamoto zingine. Tuliweza kubainisha jinsi changamoto hizi zinavyotatiza shughuli ya kutafsiri kutoka Kiswahili hadi lugha za kwanza (Kimaasai) na kutoka lugha za kwanza hadi Kiswahili.

Hatimaye katika utafiti wetu, tuliona kwamba licha ya changamoto katika shughuli ya kutafsiri kuna manufaa ya kutafsiri. Tuliangazia sekta kadhaa katika maeneo yetu ya utafiti. Sekta muhimu tulizozingatia ni pamoja na: Sekta ya elimu, katika sekta hii tulibainisha jinsi wanafunzi wa shule za chekechea na shule za msingi wanavyoweza kujifunza lugha ya Kiswahili kupitia tafsiri. Tuliona jinsi masomo ya watu wazima yanavyoimarishwa na tafsiri. Tuliona pia jinsi walimu wanavyoweza kuelezea dhana tofauti tofauti kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kimaasai na lugha ya Kimaasai hadi lugha ya Kiswahili kupitia tafsiri. Katika sekta ya dini tuliangazia manufaa kadhaa yanayotokana na kuimarishwa kwa mawasiliano katika sekta hii, kwa mfano, tafsiri kutumika katika ibada za Jumapili, tafsiri ya Biblia ya Kiswahili hadi lugha ya Kimaasai. Pia katika manufaa ya kutafsiri tuliangazia sekta ya matibabu ama ya afya.

Tuliona manufaa yanayotokana na kuimarishwa kwa mawasiliano katika sekta hii, kwa mfano, tuliona kuimarika kwa kampeni dhidi ya magonjwa hatari kama ukimwi, malaria na kipindupindu. Kwa jumla tuliangazia manufaa katika sekta muhimu katika maeneo yetu ya utafiti.

### **5.3 Hitimisho na Matokeo ya Utafiti**

Utafiti wetu umeweza kubainisha manufaa na changamoto ya kutafsiri Kiswahili katika mazingira ya wingilugha. Katika utafiti wetu, imedhihirika kwamba kuna changamoto katika shughuli ya kutafsiri katika mazingira ya wingilugha. Pia imebainika kwamba kuna manufaa katika kutafsiri na tafsiri inachangia katika kuimarisha mawasiliano katika mazingira ya wingilugha. Uchunguzi umedhihirisha kwamba licha ya kwamba mchakato wa tafsiri unakumbwa na changamoto, manufaa yanayotokana na kutafsiri ni mengi. Uchunguzi huu umeshughulikia changamoto za kutafsiri zinazosababishwa na tofauti za kitamaduni na tofauti za miundo ya lugha. Uchunguzi umeweka wazi manufaa ya kutafsiri yanayopatikana katika sekta ya elimu, ya matibabu na sekta ya dini. Utafiti huu umeonyesha kuwa kuna tofauti kubwa iliyopo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kimaasai - kimuundo na katika misingi ya kitamaduni. Utafiti umeonyesha kutokana na tofauti hizi mawasiliano yanatatizwa. Utafiti umeonyesha kwamba tofauti hizi ni vikwazo vya kutafsiri. Imedhihirika kwamba licha ya tofauti za lugha kimuundo na kitamaduni, tafsiri imeweza kufanikisha mawasiliano na kuleta manufaa katika sekta za elimu, matibabu na dini. Tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba japo kuna matatizo ya mawasiliano katika muktadha wa wingilugha, tafsiri ina uwezo wa kutatua matatizo haya.

### **5.4 MAPENDEKEZO**

Ili utafiti wowote uweze kuwa wa manufaa kwa jamii ni lazima mtafiti aweze kutambua mwanya au pengo ambalo litahitaji kuzibwa na watafiti wa baadaye. Kwa misingi hii tunatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye:

i) Manufaa yanayotokana na shughuli ya kutafsiri ni mengi kiasi kwamba hatukuweza kuangazia maeneo yote muhimu. Tunapendekeza manufaa katika sekta muhimu kama sekta ya biashara ishughulikiwe.

ii)Katika utafiti wetu tumetafitia maeneo ya wilaya ya Narok Kaskazini. Tunapendekeza maeneo mengine yatafitiwe ili kuthibitisha manufaa na changamoto za tafsiri katikahayo maeneo.

iii)Tunapendekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusu tafsiri ili kupendekeza na kuthibitisha umuhimu wa kuanzisha somo la tafsiri katika shule za msingi na za upili. Kauli hii ichukuliwe kama suala nyeti.

iv)Tumetumia nadharia ya mawasiliano katika tafsiri katika utafiti wetu.Tunapendekeza nadharia zingine zitumiwe katika tafiti za baadaye.

## MAREJELEO

- Biguenet, J. & Schulte R (1989) *The Craft of Translation*, Chicago; University of Chicago Press.
- Buliba, A, Gwachi, M, Matinde R, (2011) *Misingi, ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers
- Cartford J.C, (1965) *A Linguistic Theory of Translation*, London: O.U.P.
- Culy, M.M. (1995) “*The top down approach to Translation*” Katika Barnwell K. (Mha) Notes on translation Vol 7 No. 3.
- Duff, A. (1981) *The third language; Recurrent Problems in the Translation of English*, Oxford; Pergamon Press
- Fawcett, P. (1997) *Translation and Language: Translation Theories Explained*, Manchester: St. Jerome
- Kothari C.R. (1985) *Reserch Methodology Methods and Techniques*, New Delhi: Wiley Easton Limited.
- Lefevere v. (1992) *Translation; History and Culture*, London; Routledge.
- Malone (1988) *The Science of Linguistics in the Art of Translation*, New York: Albany State University of New York.
- Moraa L. (2013) *Matatizo yanayo Dhihirika katika Matini Tafhiri za Kimatibabu kutoka Kiingereza hadi Kiswahili*.Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi, Narobi: Haijachapishwa.
- Mshindo, H.B.C (2010) *Kufasiri na Tafhiri*, Zanzibar: Chuo Kikuu cha Chukwani.
- Munday, J. (2001) *Introducing Translation; Theories and Application*, London: Routledge.
- Mwansoko, H.J.M na Wenzake (2006), *Kitangulizi cha Tafhiri; Nadharia na Mbinu*, Dar es salaam: TUKI.
- Newmark, P. (1982) *Approaches to Translation*, Oxford: Pergamon Press.
- Newmark, P (1988) *A Textbook of Translation*, London: Prentice Hall.
- Nida, E. (1975) *Language Structure and Translation*, Stanford: Stanford University Press.
- Saravanavel, P (1987) *Research, Methodology*, New Delhi: Kitab Mahal Agencies.
- Taasisi ya Taaluma za Lugha za Kiswahili (2011) *Kioo cha Lugha*, Dar es salaam; Chuo kikuu cha Dar es salaam.
- Toury, G. (1980) *In Search of Theory of Translation*, Tel Aviv: Porter Institute of Poetics and Semantics.

Wanjala, S.F. (2011) *Misingi ya Ukalimani na Tafisiri*, Mwanza: Serengeti Education Publishers (T).